

**MABADILIKO YA MAUDHUI KATIKA NYIMBO ZA JANDO:
MFANO KUTOKA JAMII YA WAKAMBA**

NAOMI NZILANI MUSEMBI

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTIMIZA MAHITAJI YA
SHAHADA YA UZAMIFU (Ph.D) KATIKA KISWAHILI YA
CHUO KIKUU CHA MOUNT KENYA**

OKTOBA 2016

UNGAMO NA IDHINI

Ungamo la Mwanafunzi

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa na mtu yeyote kutosheleza mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine.

Naomi Nzilani Musembi Sahihi.....Tarehe.....

PhD/00210/2122/18034

Idhini ya Wasimamizi

Tasnifu hii imewasilishwa katika Chuo Kikuu cha Mount Kenya kwa madhumuni ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamifu(Ph.D) katika Kiswahili kwa idhini yetu tuliteuliwa rasmi na Chuo Kikuu kuisimamia.

Dkt. Tom Olali Sahihi.....Tarehe.....

Chuo Kikuu cha Nairobi

Idara ya Kiswahili

Dkt. Pamela Ngugi Sahihi.....Tarehe.....

Chuo Kikuu cha Kenyatta

Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika

TABARUKU

Kwa kumbukumbu ya marehemu wazazi wangu Henry Musembi na Phelis Wanza.

Malezi yenu mema yamekuwa kurunzi ya kunimulikia ulimwengu.

SHUKRANI

Kazi ya utafiti huu si ya mtu mmoja, ni ya kiko. Hivyo basi ningependa kutoa shukrani za dhati kwa watu mbalimbali waliofanikisha kazi hii. Lakini kwanzazaidi ya yote, namshukuru Maulana kwa kunipa uwezo, afya nzuri, ari na ilhamu ya kuendeleza masomo yangu. Aidha, nawashukuru wasimamizi manahodha wa safari hii, Dkt. Tom Olali wa Chuo Kikuu cha Nairobi, Dkt. Pamela Ngugi wa Chuo Kikuu cha Kenyatta na Profesa Mwenda Mukuthuria walionifunza sharuti za unahodha. Kutokana na mwongozo wenye busara pamoja na ushauri wenu, niliweza kuimaliza kazi hii kwa wakati ufaao. Mliweza kufuatilia kazi hii kwa makini hatua baada ya hatua, kunielekeza na kunikwamua nilikokuwa nimekwama pamoja na kuikosoa bila kukawia na kunishirikisha katika mijadala ya kiusomi iliyonipevusha. Mlitenga muda mwingi hata wakati wa likizo na kujinyima mengi ili kuifanikisha kazi hii. Ingawa safari ilikuwa ngumu, mliifanya rahisi kwa mawaidha mliyonipa mara kwa mara. Mlinielekeza kwa mawazo na kuniunganisha na baadhi ya wasomi ambao kazi zao zinahusiana na yangu kwa namna moja au nyingine. Nawashuku kwa kunipa ghera na ilhamu ya kuikamilisha safari hii. Kadhalika, nawashukuru wahadhiri wa idara ya Kiswahili na lugha za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Kenyatta na Moi kwa kuwa dira maridhawa katika kunihimiza niendeleo na kazi yangu. Dkt. Masinde na Dkt. Maitaria, nawashukuru kwa wingi wa shukrani kwa kunihimiza kila mara nisikate tamaa. Kwenu nyote nawatolea shukrani za pekee kwa kunipa fursa kushirikiana nanyi.

Shukrani ziwaendee wanavijiji na maafisa wa utawala katika Tarafa ya Tseikuru walionielekeza kwa magwiji wa fasihi simulizi ya Wakamba na kuniarifu wakati

kulipokuwa na sherehe za jando. Siwezi kuwasahau Titus Mutui, chifu wa Tseikuru na Annah Musyoka naibu wake kwa kuniruhusu kutangamana na wanavijiji kutafuta data ya kazi hii.

Nawashukuru wahojiwa wangu kwa mijadala na mahojiano ambayo imejenga kazi hii. Mzee Kivuvo Mwololo na mzee Peter Mulwa walinielimisha si haba kuhusu utamaduni mila na itikadi za jamii ya Wakamba. Kwa wanavijiji ambao niliweza kufanya kazi nao kuhusiana na suala la utafiti, mlinipokea kwa taadhima kubwa wakati wa kurekodi nyimbo za jando katika awamu mbalimbali. Kwa hakika, nilipata msaada kutoka kwa watu mbalimbali. Ingawa sikuweza kuwataja kwa majina, sijawasahau. Kwenu nyote nasema shukrani.

Shukrani zangu za dhati pia ziwaendee watafiti wangu wasaidizi Bw. Maw na Bw. Muendo ambao walinisaidia kuwahoji baadhi ya wahojiwa. Mlifanya kazi hii kwa moyo mmoja bila kuchoka. Mungu awabariki. Shukrani kwa wakutubi wa maktaba za Vyuo Vikuu vya Kenyatta, Egerton, Nairobi, Moi na Mount Kenya kwa kuniruhusu kutumia sehemu zote za maktaba za Vyuo hivyo.

Nawatolea kongole akraba zangu Musembi, Okoa, Mukii, Katile (kwa sasa ni marehemu), Nthenya, Ndinda na Izak kwa kuwa chachu ya yale ninayoyafanya. Radhi zenu ndiyo kinga yangu. Kwa wanangu Carol na Steve, nawashukuru kwa kunivumilia nilipokuwa nikishughulikia kazi hii, hamtajuta. Mwisho nawashukuru Bi. Anne Kimotho na Steve Mutevu kwa kuipiga chapa kazi hii kwa makini katika awamu mbalimbali bila kukawia. Steve alijaribu sana kuipitia kazi hii na kuikosoa ilipombidi kufanya hivyo.

Asante sana Steve na Anne.Kwa wale niliowataja na wengine ambao sijawataja, daima mpo moyoni mwangu.Asanteni sana na Mungu awabariki.

HATILINZI

Haki zote zimehifadhiwa. Hauruhusiwi kuiga, kurudufisha, kupiga chapa, kutafsiri, kuhifadhi kwa mfumo wowote ule au kutoa hata sehemu ndogo ya tasnifu hii kwa njia yoyote ile bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Mount Kenya.

IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za jando za jamii ya Wakamba kabla na baada ya ukoloni, kwa matlaba ya kufafanua sababu zilizoleta mabadiliko hayo. Kadri hali ya maisha inavyoendelea kubadilika, ndivyo nayo fasihi simulizi inavyobadilika. Kabla ya ukoloni, utamaduni wa jamii ya Wakamba ulikuwa imara na kila shughuli ya kijamii ilifanywa kulingana na utamaduni wao. Baada ya ukoloni, maisha yalibadilika na utamaduni wa Wakamba ukapata athari za kimagharibi, hivyo kusababisha kubadilika kwa maudhui ya nyimbo hizi. Eneo lililolengwa na utafiti huu ni kata za Nzyiitu, Kalimbui, Ngalande, Mwangea, Nzanzeni na Kaluilaakatika kaunti ndogo ya Tseikuru kaunti ya Kitui. Utafiti ulichagua sehemu hii kwa matlaba kuwa ni eneo ambalo mpaka kufikia sasa, wanapatikana masogora ambao wanashiriki jando hizi. Vilevile, ni eneo ambalo wakaaji wake wangali wanashikilia utamaduni wa kiasili na lina historia asili ya utamaduni wa tohara. Utafiti huu uliongozwa na nadharia tatu: Nadharia ya mwanaethnografia Dell Hymes (1974) ya Ethnografia ya Mawasiliano. Nadharia ya Ethnografia ya mawasiliano inazingatia mtazamo wa kiisimu-jamii ambao unajishughulisha na miktadha, utamaduni na mazingira mbalimbali katika jamii ili kuainisha lugha na matumizi yake. Nadharia ya pili ni ya Uamali kama ilivyotumiwa na wafuasi wake Levinson (1983) na Horn (1990) inayosisitiza kwamba, muktadha na matumizi ya lugha ni vipengele muhimu katika mawasiliano. Nadharia ya tatu iliyoongoza utafiti huu ni nadharia ya Uhalisia iliyowekewa msingi na mwanafalsafa Hegel (1975). Nadharia hii inashikilia kwamba, hali zote za maisha ya kijamii huelezwa katika uhalisi wake kama inavyoonekana katika mazingira halisi. Utafiti huu ulichanganua nyimbo thelathini, kumi na tanokutoka kila kipindi. Ili kupata misingi ya nadharia zilizotumika kuongoza utafiti huu, pamoja na usuli wa Wakamba na fasihi simulizi yao, hasa nyimbo; maktaba, tovuti na makavazi mbalimbali zilitembelewa. Kwa kutumia mbinu za uchunguzi shirikishi, hojaji na mahojiano ya kibinafsi, data asilia ilikusanywa. Kwa kutumia mbinu ya makusudi, wahojiwa 27 ambao ni magwiji wa fasihi simulizi ya Wakamba kutoka kila Kata walishiriki katika utafiti huu. Data asilia iliyokusanywa ilirekodiwa kwenye sidii na utepe wa video, kuandikwa kwa Kikamba na kutafsiriwa kwa Kiswahili. Maneno yalifasiriwa kimuktadha ili kupata maana katika maudhui yanayodhihirika katika nyimbo hizo. Mabadiliko kimaudhui ya nyimbo za jando yalihakikiwa kwa mujibu wa misingi ya nadharia zilizotumika katika utafiti. Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza inatoa utangulizi wa tasnifu huku ikiorodhesha malengo na umuhimu wa utafiti. Sura hii pia imeshughulikia sababu za kuchagua mada, upeo na misingi ya kinadharia iliyoongoza utafiti. Katika sura ya pili, utafiti unaelezea yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti. Sura ya tatu inafafanua mbinu za utafiti. Vilevile, inafafanua sababu za kuchaguliwa kwa sehemu ya utafiti. Sura ya nne imebainisha tohara za Wakamba na mabadiliko yaliyokumba jamii hii. Katika sura ya tano, utafiti umechanganua maudhui ya nyimbo za jando za Wakamba kabla nabaada ya ukoloni huku utafiti ukibainisha mabadiliko yake. Hitimisho na mapendekezo ya utafiti yametolewa katika sura ya tano.

ABSTRACT

This study investigated thematic changes in Kamba circumcision songs with the aim of finding out how they change. As the daily lifestyles change, oral literature has consequently been changing. These themes have been categorized into two distinct categories, the pre-colonial and post-colonial period. The two categories highlight two different lifestyles. During the pre-colonial period, the Kamba tradition was stable, and every community function was conducted in accordance to their traditions. During the post-colonial period, lifestyles changed and the Kamba traditions were influenced by the western culture, thereby changing the themes of these songs. The research was carried out at Nzyiitu, Kalimbui, Kaluilaa, Ngalange, Mwangea and Nzanzeni. These villages are found in Kaluilaa sub-location, Tseikuru sub county in Kitui county. The research was conducted in this area because the Kamba people living here still hold on to the practice of circumcision rites in the ever changing society. The research was guided by three theories: The Ethnography of communication whose proponent is Dell Hymes (1974). This theory emanates and inclines on sociolinguistics approach. Ethnography of communication is concerned with people's culture, situations, uses of language and its patterns and the functions of speaking. The second theory is the Pragmatics theory as advanced by Levinson (1983) and Horn (1990). Pragmatics theory was useful in this research in analysing the language used in the context of initiation songs, and the users of the language. The third theory which guided this research was Realism theory as advanced by Hegel (1975). This theory stresses on the depiction of contemporary life and society as it exists. To arrive at the above stated aim, thirty Kamba circumcision songs sung in different epochs in history were used as a yardstick of evaluation. Two epochs in history were selected purposively namely, before colonialisation and after colonialisation. These two periods represented other periods in the history of Kenya. Thirty songs were analysed, fifteen from each period. To get background information on the theories used by the study, and the Kamba oral literature, libraries, websites and archives were visited. By use of participant observations, interviews and discussions, primary data was collected from the 6 sub-locations in Tseikuru Sub County, Kitui County. Using purposive sampling technique, 27 experts on Kamba male initiation songs participated in the study. The recorded data was transcribed from the CD and video cassette in Kikamba followed by literal translation to Kiswahili. The words were interpreted contextually to get the meaning in the change of themes evident in the songs. The change in themes were analysed based on the theories used. This thesis is divided into five chapters. Chapter one introduces the thesis giving background information on the topic of study, objectives and reasons for choosing the topic. It also introduces the theories used in the study. Chapter two deals with literature review. Chapter three explains research methods used in the study. Chapter four analyses the change of themes in the Kamba male circumcision songs, and the changes which the society has undergone between the two periods of study as chapter five concludes the study by giving recommendations based on the findings.

MAELEZO YA ISTILAHU MUHIMU

- Ada:** Ada ni mila na desturi za jamii ya Wakamba.
- Baada ya wakoloni:** Maneno haya yametumiwa kumaanisha athari zilizopatikana katika utamaduni wa Wakamba baada ya maingiliano yao na wakoloni.
- Jando:** Chuo cha wavulana baada ya tohara wanakopata mafunzo kuhusu mila na tamaduni za jamii yao.
- Kabla ya wakoloni:** Maneno haya yametumiwa kumaanisha kipindi ambacho utamaduni wa jamii ya Wakamba ulikuwa imara bila athari za kimagharibi.
- Nyimbo za jando za kimapokeo :** Nyimbo za kiasili za jando ambazo zilipokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
- Nyimbo za jando za kisasa:** Nyimbo za kisasa za jando ambazo huimbwa katika sherehe za jando za kisasa.
- Ubabedume:** Ni mfumo wa kijamii ambao humtukuza mwanamume, na kumdhaliisha mwanamke.
- Unyago:** Chuo kinachohusu wanawake. Wanawali hufunzwa kuhusu unyumba, mahusiano yao na wanaume, uzazi, ulezi na namna ya kuishi maisha ya ndoa na kuyamudu.
- Wakoloni:** Utafiti huu unatumia istilahi hii kumaanisha wazungu waliosababisha utamaduni wa Wakamba kupata athari za kimagharibi.

YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI	iv
HATILINZI	vii
IKISIRI	viii
ABSTRACT	ix
MAELEZO YA ISTILAHU MUHIMU	x
SURA YA KWANZA	1
1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti	1
1.2 Suala la Utafiti	3
1.3 Lengo La Utafiti.....	4
1.4 Madhumuni ya Utafiti.....	4
1.5 Maswali ya Utafiti.....	4
1.6 Sababu za Kuchagua Mada.....	5
1.7 Upeo wa Utafiti.....	7
1.8 Misingi ya Kinadharia.....	8
1.8.1 Nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano.....	9
1.8.2 Nadharia ya Uamali	13
1.8.3 Nadharia ya Uhalisia.....	17
SURA YA PILI	22
YALIYOANDIKWA KUHSU MADA YA UTAFITI	22
2.0 Utangulizi.....	22
2.1 Historia ya Jamii ya Wakamba	22
2.1.1 Jamii ya Wakamba Kabla ya Ukoloni	27
2.1.1.1 Mpangilio wa Jamii.....	28
2.1.1.2 Dini	31

2.1.1.3 Mfumo wa Kiuchumi	33
2.1.1.4 Mahusiano ya Kiuana	36
2.1.1.5 Tohara ya Wakamba	38
2.1.1.5.1 Tohara ndogo (<i>Nzaiko nini</i>)	39
2.1.1.5. 2 Tohara kubwa (<i>Nzaiko nene</i>)	41
2.1.1.5. 3 Tohara ya Kucheza (<i>Nzaiko ya Ngingo</i>)	42
2.1.2 Jamii ya Wakamba Baada ya Ukoloni	45
2.2 Maandishi kuhusu Utanzu wa Nyimbo.....	47
2.3 Tafiti kuhusu Nyimbo kwa Jumla.....	52
2.4 Tafiti Kuhusu Nyimbo za Wakamba.	65
SURA YA TATU	71
MBINU ZA UTAFITI	71
3.1 Njia za Utafiti.....	71
3.1.1 Utafiti wa Maktabani	71
3.1.2 Utafiti katika Mtandao	72
3.1.3 Utafiti wa Nyanjani.....	72
3.2 Eneo la Utafiti	73
3.3 Walengwa wa Utafiti	73
3.4 Sampuli lengwa na Mbinu za Uteuzi wa Sampuli	73
3.5 Vifaa Vya Utafiti.....	75
3.6 Ukubalifu na Utegemeo wa Vifaa vya Utafiti	76
3.6.1 Kalamu na Karatasi.....	76
3.6.2 Rununu.....	77
3.7 Mbinu za Ukusanyaji Data.....	77
3.8 Uchanganuzi wa Data	79
3.9 Maadili ya Utafiti.....	79
3.9.1 Maadili ya Utafiti yanayohusu Mtafiti.....	79
3.9.2 Maadili ya Utafiti yanayohusu Watafitiwa.....	80
3.9.3 Maadili ya Utafiti yanayohusu Mchakato wa Utafiti.....	81

SURA YA NNE	82
UCHANGANUZI WA MAUDHUI YA NYIMBO ZA JANDO ZA WAKAMBA KATIKA KIPINDI CHA KABLA NA BAADA YA UKOLONI.....	82
4.0 Utangulizi.....	82
4.1 Maudhui ya Nyimbo za Jando za Wakamba katika Kipindi cha Kabla ya Ukoloni....	82
4.1.1 Umuhimu wa Tohara	83
4.1.2 Kupongeza Ujasiri	87
4.1.3. Kukejeli Tabia Zilizoenda Kinyume na Matarajio ya Jamii	92
4.1.3.1 Woga wa Kisu.....	92
4.1.3.2 Kukashifu Uchoyo	94
4.1.3.3 Mazoea ya Mwanamke ya Kutorokea kwao Baada ya Ugomvi na Mumewe	95
4.1.4 Kupongeza Wazazi wa Mtahiriwa	96
4.1.5 Kusifia Ngariba.....	97
4.1.6 Kushauri Watahiriwa kuhusu Ngonzo za Kwanza	98
4.1.7 Matarajio ya Jamii kwa Watahiriwa	100
4.1.8 Nafasi ya Mwanamke katika Jamii	101
4.1.9 Majukumu ya Kiuana.....	106
4.1.10 Migogoro ya Kijamii.....	108
4.1.11 Ushirikiano wa Kijamii.....	109
4.1.12 Kuelezea Historia ya Jamii ya Wakamba	111
4.2 Maudhui ya Nyimbo za Jando za Wakamba katika kipindi cha baada ya Ukoloni...	113
4.2.1 Umuhimu wa Elimu Mpya ya Kisasa	114
4.2.2 Tahadhari Dhidi ya Ukimwi	116
4.2.3 Ubaguzi wa Mwanamke	121
4.2.4 Ushirikiano wa Kijamii.....	125
4.2.5 Ushoga na Ndoa za Jinsia Moja.....	129
4.2.6 Umuhimu wa Upangaji Uzazi.....	132
4.2.7 Kulalamikia Mabadiliko katika Majukumu ya Kiuana.....	134
4.2.8 Athari za Uchumi wa Pesa.....	138
4.2.9 Matatizo katika Ndoa za Kisasa.....	140

4.2.10	Shutuma dhidi ya Tohara za Hospitalini.....	145
4.2.11	Nafasi ya Dini ya Kisasa katika Maisha ya Wanajamii.....	146
4.3	Mabadiliko ya Maudhui ya Nyimbo za Jando za Wakamba kutoka Kipindi cha Kabla ya Ukoloni hadi Kipindi cha Baada ya Ukoloni.....	151
SURA YA TANO		164
MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO		164
5.1	Muhtasari wa Tasnifu	164
5.2	Matokeo ya Utafiti	166
5.3	Mapendekezo Yanayotokana na Utafiti Huu	172
5.4	Mapendekezo ya Maeneo ya Kufanyiwa Utafiti Zaidi	173
5.5	Changamoto za Utafiti	174
MAREJELEO		176
Kiambatisho Cha 1 : Ufafanuzi wa Istilahi za Kikamba.....		190
Kiambatisho Cha 2 : Nyimbo za Jando za Wakamba.....		192
Kiambatisho Cha 3 : Nyimbo Zingine Jadiiya za Wakamba.....		201
Kiambatisho Cha 4 : mwongozo Wa Hojaji		205
Kiambatisho Cha 5 : Maelezo ya Wahojiwa.....		208
Kiambatisho Cha 6 : Ramani ya Sehemu za Utafiti		213
Kiambatisho Cha 7 : Ramani ya Wilaya ya Mwingi		214
Kiambatisho Cha 8 : Ramani ya Kaunti ya Kitui		215
Kiambatisho Cha 9 : Ramani ya Kenya ikionyesha Kaunti ya Kitui na Kaunti Zingine.....		216
Kiambatisho Cha 10 : Picha Zilizopigwa na Mtafiti Wakati Wa Utafiti.....		217
Picha ya 1		217
Picha ya 2.....		218
Picha ya 3.....		219
Picha ya 4.....		220
Picha ya 5.....		221
Picha ya 6.....		222

Picha ya 7	223
Picha ya 8.....	224
Picha ya 9.....	225
Picha ya 10.....	226
Kiambatisho Cha 11 : Utendaji wa Nyimbo za Jando katika Utepe wa Video	227
Kiambatisho Cha 12 : Barua ya Idhini ya Kufanya Utafiti Nyanjani	228

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi

Katika sura hii, tasnifu ilishughulikia masuala ya kimsingi yanayofaa kuzingatiwa. Masuala haya ni pamoja na usuli, suala la utafiti, malengo na maswali yaliyoongoza utafiti pamoja na sababu za kuchagua mada. Aidha, sura hii ilishughulikia upeo wa utafiti na misingi ya kinadharia iliyoongoza utafiti huu.

1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Fasihi simulizi ni utanzu muhimu wa fasihi katika jamii kwani utamaduni wa jamii inayohusika hujidhihirisha kupitia utanzu huu (Wamitila, 2003). Wakamba ambao ndio watafitiwa katika uchunguzi huu, hueleza hali ya maisha yao, utamaduni wao, imani na mila zao kupitia tanzu za fasihi simulizi. Wanaeleza maoni na mitazamo yao kupitia tanzu mbalimbali za fasihi simulizi kama vile nyimbo, ngano, methali miongoni mwa nyingine. Nyimbo hutumia lugha ya kitamathali kueleza maudhui mbalimbali yanayoibuliwa na nyimbo hizo.

Katika jamii ya Wakamba, fasihi simulizi ni fasihi hai inayoelezea mielekeo na falsafa kuhusu maisha ya watu (Ndeti, 1972). Kama ukumbusho wa maadili ya watu, fasihi simulizi hutoa mwonoulimwengu wa jamii na kutokana nayo, hali ya maisha ya kila siku huendelezwa. Fasihi simulizi ina dhima muhimu katika jamii (<http://gwabata.hpage.co.in/fasihi-na-umuhimuwake-katika-jamii>). Inachangia katika kuendeleza na kudumisha historia na utamaduni wa jamii husika. Finnegan (1970)

anasema kuwa, katika muundo wa maisha ya jamii za Kiafrika, nyimbo za kitamaduni zilikuwa na majukumu muhimu kadha wa kadha. Waafrika walikuwa na nyimbo ambazo ziliambatana na matendo mbalimbali ya maisha yao. Takriban jamii zote za Waafrika zilikuwa na nyimbo ambazo maudhui yake yaliegemea ushindi wa vita, kuzaliwa, kupashwa tohara, harusi, maombolezi, kulima, kupumzika, kulisha mifugo, kumlea mwana, kuliwaza, na takriban shughuli zote za binadamu (King'ei 1982). Aidha, nyimbo hizi huwa na maudhui na mitindo yake inayohusiana na shughuli inayotekelezwa. Hata hivyo, maudhui na mitindo hii hubadilika na wakati na husawiri historia na mwelekeo wa jamii (Nandwa na Bukenya,1983).

Fasihi simulizi huibuka na kujengeka katika hali halisi ya maisha ya kila siku. Kulingana na Simiyu (2007), nyimbo kama utanzu wa fasihi simulizi huendelea kupata mabadiliko ya kijamii kadri jamii inavyoendelea kubadilika. Fasihi simulizi ya jamii fulani huweza kuathiriwa na mabadiliko yanapotokea. Mabadiliko yanaweza kutokana na uhamiaji, maingiliano na mahusiano ya kijamii kikabila, kidini, kisiasa, au kiuchumi. Mabadiliko ya maudhui ya nyimbo katika jamii za Kiafrika yanatiliwa mkazo na Nandwa na Bukenya (1983) pale wanaposema kwamba, kazi yoyote ya fasihi haiibuki katika ombwe tupu lakini hujikita katika maudhui kutoka kwa jamii. Kadri hali ya maisha katika jamii inavyobadilika, ndivyo fasihi simulizi inavyobadilika. Mabadiliko haya hudhihirika katika nyimbo kwa sababu ni mojawapo wa fani za fasihi simulizi ambayo ni hai hivi kwamba hubadilika kadri hali ya maisha inavyobadilika.

Ni muhimu, hivyo basi, kuzitafiti nyimbo za jando ili kubainisha mabadiliko kimaudhui ya nyimbo hizi na dhima yake katika jamii ya Wakamba inayobadilika. Kutokana na mantiki hii, utafiti huu ulichunguza mabadiliko kimaudhui ya nyimbo za jando miongoni mwa jamii ya Wakamba ukiwa na lengo la kubainisha kuwa, nyimbo hizi zimeathiriwa na mabadiliko ya kijamii.

1.2 Suala la Utafiti

Ni kweli kwamba fasihi kwa jumla ni kipengee cha utamaduni kinachoathiriwa na hali halisi ya maisha ya jamii husika. Mabadiliko yanayoikumba jamii kwa njia moja au nyingine hujidhihirisha katika fasihi. Matukio makuu ya muongo fulani yanaweza kutambulika kutokana na fasihi ya muongo huo, hasa kupitia kipengele cha maudhui ambacho hubadilika kiwakati kadri jamii inavyozidi kukumbwa na mabadiliko. Ari ya kufanya utafiti huu ilitokana na madai ya tafiti za awali za Kilauni (2007) na Wathome (2009) zilizodai kuwa, nyimbo jadiya za Wakamba zimedidimia na kusahaulika kutokana na mabadiliko ya kijamii. Madai haya yalichangia msukumo wa kufanya utafiti huu ili kubatilisha mielekeo ya watafiti hawa kwa kubainisha kuwa, nyimbo za jando za jamii ya Wakamba ni hai, na zinabadilika kulingana na mabadiliko ya kijamii ili ziendeleo na utendakazi wake muhimu katika jamii. Hata hivyo, haijulikani ni kwa jinsi gani mabadiliko katika jamii ya Wakamba yameziathiri nyimbo hizi suala ambalo lilishughulikiwa na utafiti huu. Mabadiliko hayayalichunguzwa katika misingi ya vipindi viwili bainifu ambavyo jamii ya Wakamba imepitia hususan; kipindi cha kabla ya ukoloni na baada ya ukoloni.

1.3 Lengo La Utafiti

Utafiti huu ulilenga kubainisha kwambamaudhui ya nyimbo za jando za Wakamba yamebadilika kulingana na mabadiliko ya kijamii kimpito wakati. Hili ni kutokana na sababu kwamba, Mabadiliko yanayoikumba jamii kwa njia moja au nyingine hujidhihirisha katika fasihi kipera cha wimbo kikiwemo.

1.4 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu ni:

- a) Kuchunguza maudhui ya nyimbo za jando za Wakamba kabla ya maingiliano yao na wakoloni.
- b) Kubainisha jinsi kipindi cha baada ya ukoloni kilivyoathiri maudhui ya nyimbo za jando za Wakamba.
- c) Kuainisha matukio ya kijamii yanayoathiri maudhui katika nyimbo za jando za Wakamba.
- d) Kuchunguza mbinu za kisanaa zinazotumika na watunzi wa nyimbo za jando katika jamii ya Wakamba ili kubadilisha maudhui kwa mujibu wa wakati.

1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

- a) Je, nyimbo za jando za Wakamba zilikuwa na maudhui yapi kabla ya maingiliano yao na wakoloni?
- b) Maudhui hayo yamebadilika vipi baada ya ukoloni?

- c) Ni matukio yapi ya kijamii yanayoathiri maudhui katika nyimbo za jando za Wakamba?
- d) Je, ni mbinu zipi za kisanaa zinazotumiwa na watunzi wa nyimbo za jando katika jamii ya Wakamba kubadilisha maudhui kwa mujibu wa wakati?

1.6 Sababu za Kuchagua Mada

Fasihi simulizi ni fani hai ambayo inaendelea kutekeleza majukumu muhimu katika jamii (Wamitila, 2003). Maadili yalikuwa na hata sasa yanakuzwa kupitia kwa nyimbo na haswa za jando miongoni mwa jamii ya Wakamba. Licha ya ukiukaji wa maadili na kuacha mila miongoni mwa vizazi vya leo, nyimbo huchangia katika kujaribu kuwaelimisha wanajamii umuhimu wa kuwa na maadili. Uchunguzi wa maudhui ya nyimbo unaweza kueleza itikadi ya jamii, utamaduni pamoja na matarajio ambayo hupatikana katika jamii. Nyimbo katika jamii ya Wakamba ni utanzu wa fasihi simulizi ambao hufungamanishwa na historia, utamaduni, amali, mielekeo, imani na dini yao. Mfumo mzima wa kidini, kiuchumi, kijamii na kiutawala wa jamii ya Wakamba unaweza kuchunguzwa kwa kuhakiki nyimbo zao za jando. Utafiti huu ni dira ya kueleza mabadiliko ya maudhui yanayobainika katika nyimbo hizo.

Vilevile, jamii zetu zinakumbwa na matatizo mengi kama magonjwa, uraibu wa dawa za kulevya, vita vya wenyewe kwa wenyewe, unyanyasaji wa wanawake na watoto, ukame miongoni mwa matatizo mengine. Ili kupambana na hali hizi ngumu, ni muhimu kuwa na nyenzo za mawasiliano zinazoweza kutumiwa kufahamisha wanajamii jinsi ya

kukabiliana nazo. Nyimbo za jando ni miongoni mwa njia hizi kwani kupitia kwazo, ujumbe unaweza kuwasilishwa kuhusiana na namna ya kukabiliana na matatizo haya ya kijamii. Pia, uchaguzi wa mada hii ulikuwa na lengo la kuendeleza nadharia ya Craig (1975) kwamba, matukio makuu ya muongo fulani yanaweza kutambulika kutokana na fasihi ya muongo huo, hasa kupitia kipengele cha maudhui ambacho hubadilika kiwakati kadri jamii inavyozidi kukumbwa na mabadiliko.

Aidha, nyimbo za jando zinatishia kuangamia na kutoweka kabisa kutokana na mabadilikokatika jamii yanayotukuza jando za hospitalini (Mutwiri, 2005). Mabadiliko ya kitamaduni yaliyosababishwa na elimu na dini za kimagharibi barani Afrika yamepunguzia fasihi simulizi hasa nyimbo za jando rutuba ya maendeleo. Hali ya maisha inaendelea kubadilika kutokana na wanajamii kuhamia mijini katika harakati za kuzalisha mali, na kutafuta riziki. Wengine wanahamia nchi nyingine kwa ajili ya kazi na masomo. Hali hii imepelekea kuipunguzia fasihi simulizi mashiko na maendeleo. Hivyo basi, utafiti huu ulilenga kutafiti nyimbo za jando na kuzihifadhi kama mojawapo ya hifadhi za tamaduni za jamii ya Wakamba. Kumbukumbu hizi zitawasaidia Wakamba na wasio Wakamba kuelewa utamaduni wa Mwafrika katika ulimwengu huu unaobadilika.

Vilevile, matokeo ya utafiti huuyatachangia tafiti zinazohusiana na umuhimu wa nyimbo hasa za jandokwa vijana katika ulimwengu wa leo. Pia, utafiti huu umetoa mchangowa kitaaluma pale ambapo baadhi ya nyimbo za jando katika jamii ya Wakamba zimehakikiwa na kuandikwa kwa Kiswahili.

Matokeo ya utafiti huu yatakuwa hazina kwa wakuza mitalaa, wahadhiri na walimu katika ufunzaji wa fasihi simulizi, somo ambalo hufunzwa katika viwango vyote vya elimu hapa nchini. Pia, tasnifu hii itakuwa juhudi za kuongezea utafiti na maandishi kuhusu fasihi simulizi na nyimbo za jando katika jamii. Hatimaye, kazi hii itachapishwa ili kuwafaidi wataalamu watakaofanya tafiti za baadaye kuhusu nyimbo za jando za Wakamba.

1.7Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulishughulikia mabadiliko ya maudhui pekee katika nyimbo za jando za jamii ya Wakamba. Kazi hii haikushughulikia nyimbo za unyago kutokana na sababu kwamba, Baada ya ukoloni, tohara za wanawake zilipigwa marufuku hapa nchini Kenya na serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali dini ya kikristo pamoja na makundi ya kutetea haki za watoto (Kaname 2001). Nyimbo zilizohakikiwa ni zile ambazo ziliimbwa katika vipindi bainifu ambavyo jamii ya Wakamba imepitia hususan, kabla na baada ya ukoloni. Vipindi hivi viwili vinaangazia hali mbili za kimaisha.

Jamii ya Wakamba inaaina nyingi za nyimbo zilizotumika na bado zinatumika kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kijamii. Utafiti huu ulijifunga katika nyimbo za jando pekee kutokana na sababu kwamba, kipera cha nyimbo za jando hulenga vijana ili kupitia kwacho, mafunzo kuhusiana na maadili, mila na tamaduni za jamii huweza kupitishwa kwao vyema zaidi. Utafiti huu ulikusanya nyimbo za jando nyingi, ilimbidi mtafiti kuzichuja na kuteua nyimbo thelathini (30) ambazo zinalenga mada ya utafiti.

1.8 Misingi ya Kinadharia

Nadharia ambazo ziliupa mwelekeo utafiti huu ni nadharia ya mwanaethnografia Dell Hymes (1974), nadharia ya Uamali kulingana na Levinson (1983) na Horn (1990) pamoja na nadharia ya Uhalisia iliyowekewa msingi na mwanafalsafa Hegel (1975). Nadharia hizi zilitumiwa kimwingiliano. Mihimili yanadharia ya Ethnografia ya mawasiliano ilitumika katika kuchanganua muktadha, hadhira, utamaduni na mazingira mbalimbali katika jamii ya Wakamba ili kuainisha lugha na matumizi yake katika nyimbo za jando. Kadhalika, haja ya kushughulikia mada ya utafiti huu katika misingi ya kiuamali ilitokana na ugunduzi kuwa, utafiti huu haungeweza kufanya uchunguzi wa kina wa nyimbo za jando bila kuhusisha maana ya maneno yaliyotumiwa katika nyimbo hizo na muktadha mahususi. Hii ni kwa sababu nadharia ya Ethnografia ya mawasiliano ina upungufu fulani katika kushughulikia matumizi ya lugha katika fasihi. Hivyo basi, nadharia ya Uamali imetumiwa ili kushirikisha matumizi ya lugha kama nyenzo ya kufaulisha mawasiliano.

Aidha, utafiti huu uligundua kuwa, watu hufasiri ishara kwa njia tofauti kutegemea tajriba zao. Nadharia ya Uamali huchunguza lugha kwa kuihusisha na mtumiaji, hasa kwa kuzingatia uchaguzi wa miundo ya maneno anaoufanya, vikwazo na athari za kijamii anazokumbana nazo katika kutumia lugha hiyo. Nadharia ya Uamali ilitumika ili kuhusisha lugha inayotumiwa katika nyimbo za jando za Wakamba na watumiaji wake, hasa kwa kuzingatia uchaguzi wa miundo ya maneno, viziada lugha na ishara. Nayoa nadharia ya Uhalisia ilitumika kama kigezo cha kupimia uhalisi katika nyimbo za jando

za Wakamba, na usanii wa matukio katika maisha ya kila siku ya jamii hii. Utafiti huu ulitumia mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za jando za Wakamba kama kielelezo cha kumulikia uhalisi huo ambao, ulipimwa kulingana na vigezo vya nadharia ya Uhalisia. Kimsingi, nadharia zilizoongoza utafiti huu huwiana na kukamilishana kwa ambavyo huzieleza, huzichanganua na huzifasiri kazi za fasihi kwa kuzingatia muktadha wa utamaduni, lugha, hadhira lengwa na uhalisi wa maisha ya watu katika jamii.

1.8.1 Nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano

Nadharia ya Ethnografia ya mawasiliano ya Dell Hymes (1974) kulingana na Hudson (1980), na Fasold (1990) iliasisiwa na Hymes (1964). Ethnografia hasa ya mawasiliano ni uchanganuzi wa lugha na jukumu lake katika jamii husika. Nadharia hii ni mtazamo wa isimu-jamii unaojikita katika vipengele vikuu vitatu hususan muktadha, utamaduni na mazingira mbalimbali katika jamii ili kuainisha lugha na matumizi yake. Mtazamo huu huchunguza namna tukio fulani katika jamii linavyoibua matumizi maalum ya lugha ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa. Aidha, huchunguza jinsi wahusika wa lugha fulani wanavyoitumia lugha hiyo kwa kutekeleza majukumu yao ikiwa ni pamoja na kushauri, kuonya, kutia moyo, kukashifu, kubembeleza, kuliwaza, kukejeli tabia mbovu, kuelezea hisia mbalimbali, kuhifadhi utamaduni, kuwasiliana na hata kuburudisha.

Katika miaka ya 1960, wanaathropolojia, wanasosholojia na wanaisimu walitafiti matumizi ya lugha katika jamii mbalimbali na walizingatia namna ambavyo wanajamii wanavyotumia lugha kama kiini chao katika uchunguzi. Wakiongozwa na wataalamu

kama Hymes (1964), walichunguza matumizi ya lugha katika miktadha mahsusi ya kijamii kwa kutumia utaratibu mpya uliohusisha lugha na utamaduni. Hymes alikuwa mstari wa mbele kuupa mtazamo huu mpya jina Ethnografia ya mawasiliano hasa baada ya kuwasilisha makala aliyoyaita Ethnografia ya uzungumzi mwaka wa 1962. Pia, walieleza kuwa, matumizi ya lugha hayawezi kutenganishwa na utamaduni wa jamii yaani mila, desturi na itikadi za jamii hiyo. Nadharia hii ina misingi yake katika jamii lugha na inapotumiwa huchunguza jinsi mawasiliano yanayotumia lugha huendesha.

Kwa mujibu wa Crystal (1977), mada inayozungumziwa ni kipengele muhimu katika mawasiliano. Maudhui ya ujumbe unaowasilishwa yanakuwa nguzo muhimu katika kuteua maneno mwafaka katika mawasiliano. Kulingana na Crystal (aliyetajwa), kinachovutia katika kuibua maana katika sanaa ni muktadha wa maongezi. Muktadha huchukua wajibu mkuu katika kubainisha jinsi maneno mahususi yanavyofafanuliwa katika tukio lolote. Gregory na Carroll (1978) wanasema kwamba, maneno huibua maana yao kulingana na muktadha husika. Maana ya maneno yanaweza kuzingatiwa kulingana na vile yanavyotumiwa kimuktadha. Kulingana nao, muktadha ni muhimu katika kufasiri matukio ya kijamii na pia katika kuwasilisha ujumbe kwa wanajamii. Aidha, kwa mujibu wao, miktadha ya kijamii ambapo mawasiliano hufanyika huchangia pakubwa uteuzi wa aina ya lugha ifaayo kutumiwa kuwasilisha ujumbe miongoni mwa wanajamii. Matumizi ya muktadha kama kitengo kikuu cha nadharia ya mawasiliano katika utafiti huu, kiliwezesha utafiti huu kutafsiri na kufafanua mbinu za sanaa zilizotumiwa kulingana na muktadha wa jando.

Akichangia kuhusu umuhimu wa lugha katika mawasiliano, Halliday (1964) anasema kwamba, tamko la lugha haliwezi kueleweka ipasavyo ikiwa litafasiriwa pekee pasipo kuhusishwa na maswala mengine ya muktadha, hadhira na mahusiano yao, mada inayozungumziwa, mazingira yaliyomo na maswala mengine ya mawasiliano

Kwa mujibu wa Swingerwood (1991), lugha huleta maana ikiwa maneno yanaangaliwa katika muktadha yalimotumiwa. Hali hii inaonyesha kuwa, lugha haiwezi kutenganishwa na muktadha na mahali ilimotumiwa. Naye Firth (1968) anasema kuwa, muktadha ni muhimu katika kuibua mawasiliano. Maoni yake yanajitokeza katika mihimili ya Ethnografia ya mawasiliano ya Hymes (1962, 1964, na 1974). Maoni haya yanaufanya muktadha kuwa kitengo mahususi cha nadharia ya Ethnografia ya mawasiliano. Saville – Troike (1982); Wardshaugh (1986, 2010) na Fasold (1990) walipambanua vipengele mbalimbali vya Ethnografia ya mawasiliano kama vilivyopendekezwa na Hymes (1962,1964, 1974) hususan mada, ujumbe, lugha, muktadha, wahusika, na mazingira. Vipengele hivi ndivyo mihimili ya nadharia hii.

Nadharia hii pia imeshadidiwa na mawazo ya Dundes (1965,1980). Hoja zake ni kwamba, miundo mbalimbali ya matini zinazowasilishwa kwenye sherehe hudhihirisha thamani na imani ambazo ni muhimu katika kundi- jamii. Kulingana na Dundes (1965), katika sherehe hizo kuna ishara za kitamaduni ambazo hueleweka tu kupitia muktadha na utamaduni wa jamii husika. Dundes (aliyetajwa) ameeleza dhana ya muktadha kwa kujumuisha utamaduni, kundijamii na ishara kuhusu mada inayojadiliwa. Amesema kuwa wataalamu wanaoshughulikia elimu ya jando wana imani kwamba, ili kuelewa

vizuri ishara za mawasiliano, ni lazima kufanya uchunguzi kuhusu muktadha, mazingira na utamaduni ambapo tukio fulani linapatikana.

Kulingana na Hymes (1974) na Ngara (1982), mawasiliano huwepo na kukamilika miongoni mwa wanajamii kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo, ambavyo ndivyo mihimili ya nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano:

- i) Muktadha.
- ii) Hadhira lengwa.
- iii) Utamaduni na lugha ya jamii husika.

Mihimili hii ilitumika katika utafiti kuchunguza na kufafanua watumiaji lugha, na namna wanavyoitumia lugha katika utunzi wa nyimbo za jando ili kupitisha ujumbe unaokusudiwa kupitia kwa maudhui. Nyimbo za jando za Wakamba huimbwa katika muktadha maalumu ili kutekeleza wajibu wake. Watunzi na waimbaji walibadili nyimbo kuakisi na kusawiri tofauti za kimuktadha. Kwa mujibu wa Hymes (1974), Ethnografia ya Mawasiliano ni nadharia inayotuwezesha kutambua iwapo tukio la mawasiliano limeafiki lengo lake. Hali hii huelekezwa na mila na tamaduni za jamii husika. Nadharia hii ilichangia utafiti huu kwa kiasi kikubwa kwa sababu mbali na kuchunguza aina ya lugha iliyotumika katika nyimbo hizi, utafiti huu uliweza kubainisha maana ya ndani ya maneno yaliyotumika kimuktadha ili kuweka bayana maudhui ya nyimbo hizi.

1.8.2 Nadharia ya Uamali

Wafuasi wa mtazamo huu kama vile Levinson (1983), Leech (1983) na Horn (1990) walisisitiza kwamba, nadharia ya Uamali huchunguza kanuni za kimsingi zinazotawala matumizi ya lugha. Nadharia ya Uamali kulingana nao ni uhusiano baina ya lugha na muktadha. Wanasisitiza kwamba, kwa kuzingatia muktadha, maana inayokusudiwa na matumizi fulani ya lugha hasa ya tamathali za usemi hujitokeza kwa njia inayoeleweka vyema zaidi, hivyo basi kuathiri hadhira zaidi. Kwa mujibu wao, lugha, hasa ya kifasihi, haiwezi kutoa maana kamili bila ya kuihusisha na muktadha maalumu.

Maoni ya Levinson (1983) ni kwamba, Uamali ni nadharia inayojihusisha na uhusiano baina ya maneno, matumizi yake na fasiri inayofanyiwa lugha husika. Kulingana na Horn (1990), licha ya maneno huru kuwa na maana, kuna uwezekano wa kupata maana pana zaidi pale maneno hayo yanapohusishwa na matumizi ya maneno mengine katika mazingira yanamotokea. Maoni ya Horn (1990) kama yalivyo ya Levinson (1983) na Leech (1983) ni kwamba, muktadha ni muhimu katika kuyapa maneno maana katika tukio la mawasiliano. Nadharia ya Uamali kwa mtazamo huu iliupa utafiti huu mwelekeo kwa kuhakiki matumizi ya lugha hasa tamathali za usemi katika nyimbo za jando za Wakamba ili kufaulisha mawasiliano.

Nadharia ya Uamali huchunguza kazi ya kifasihi katika muktadha wa mawasiliano. Wimbo hufungamana na muktadha na hadhira (Mulokozi,1989). Nyimbo za tohara za Wakamba huimbwa katika muktadha maalum ili kuwasilisha ujumbe fulani kwa hadhira.

Kaplan (1989) anafafanua uamali kama maelezo ya kwa nini neno linapewa maana fulani badala ya maana nyingine. Ihali Goodman (2005) anasema uamali hufafanua jinsi sentensi zinavyotumiwa katika usemi kuwasilisha ujumbe kimuktadha. Kwa mujibu wa Grice (1989), uamali hujumuisha vipengele vinavyofaulisha mawasiliano hususan; nia ya mwasilishaji, matumizi ya lugha yanayolandana na nia yake, na mikakati inavyotumiwa na msimbuaji ujumbe kuelewa kusudi la mwasilishaji ujumbe.

Carston (1988) anasema uamali huchunguza matumizi ya lugha kimuktadha. Kulingana naye, uamali huchunguza ni vipi sentensi moja sawa inaweza kuwasilisha ujumbe tofauti katika miktadha mbalimbali. Anaendelea kusema kwamba, tunapozungumzia uchanganuzi wa kiuamali huwa tunajihusisha na maswala ya nje ya isimu. Uamali kulingana naye hujumuisha vipengele vyote vinavyohusu usimbaji na usimbuaji ujumbe kama mazingira, wahusika, kinachoendelea wakati huo na sababu zilizofanya mtunzi wa ujumbe autunge.

Kwa mujibu wa Yule (1991), uamali unahusu uhusiano baina ya ishara na wachanganuzi wa ishara hizo. Yule (aliyetajwa) anasema kuwa uamali hujumuisha matukio ya kisaikolojia, kibayolojia na maswala ya kijamii yanayotokea katika uamilifu wa ishara. Vilevile, kulingana na Yule (1991), nadharia ya Uamali inashikilia kuwa kila kazi ya fasihi ina muktadha wa kijamii. Muktadha huo na jamii husika zina mahusiano yanayoingiliana. Aidha, Yule (1991) anatoa hoja kuwa, uamali unajihusisha na uhusiano baina ya maneno na matumizi yake. Anasema licha ya maneno huru kuwa na maana; kuna uwezekano wa kupata maana pana zaidi pale maneno yale yanapohusishwa na

matumizi ya maneno mengine katika mazingira yanamotokea. Mhimili huu ulitufaa katika uchunguzi wa jamii ya Wakamba iliyozalisha nyimbo za jando katika mahali na muktadha maalumu. Aidha, kwa mujibu wa nadharia ya Uamali, muktadha wa chimbuko la kazi ya fasihi husika huathiri ufasili wa kazi hiyo. Nyimbo za jando katika jamii ya Wakamba huimbwa katika muktadha maalumu ili kuwasilisha ujumbe fulani kwa hadhira.

Nadharia ya Uamali huhusisha athari ipatikanayo kutokana na matumizi ya lugha katika muktadha maalum (Kobia, 2008 ; Mosha, 2011). Kulingana Kobia (aliyetajwa), hakuna mtu anayeweza kujadili fasihi bila kuzingatia kuwa kuna matumizi maalum ya lugha. Aidha, wanashikilia kuwa kuelewa maudhui ya kifasihi kunategemea kuelewa lugha kwa kuzingatia maana zinazoibuliwa na lugha hiyo.

Kwa mujibu wa nadharia ya Uamali, viziada lugha vina umuhimu katika kufaulisha mawasiliano yanayokusudiwa kupitia kazi za kifasihi (Horn, 1990; Kobia, 2008; Mosha, 2011). Viziada lugha huchangia katika kuelewa maana katika nyimbo za jando. Vizianda lugha vinavyotumiwa katika nyimbo za jando hususan miondoko ya mwili, mikunjo ya uso na urushaji wa mikono husaidia katika kufanikisha kueleweka kwa maana ya maneno ili maudhui ya nyimbo yaweze kuibuliwa ipasavyo. Kwa mujibu wao , uamali ni nadharia ambayo huchunguza mfumo unaotawala uwezo wa hadhira kufasiri matumizi ya lugha katika muktadha maalumu, ili kufanikisha mawasiliano. Naye Barry (1993) anasema kwamba, katika nadharia ya Uamali, lugha huchukuliwa kama chombo cha kudhihirisha ukweli pamoja na kueleza. Kulingana na Barry (aliyetajwa), lugha ina

dhima kubwa katika kufanikisha kazi ya fasihi kupitia matumizi ya tamathali za usemi. Lugha katika mtazamo huu inaonekana kama kigezo muhimu cha kupimia ufanisi wa kazi ya fasihi.

Akieleza kuhusiana na nadharia ya uamali, Bacon (2012) anaona uamali kuwa uchunguzi wa lugha unaotilia maanani watumiaji lugha na miktadha ambamo lugha hiyo hutumiwa. Uamali haujihusishi na ukweli wala usarufi. Bacon (aliyetajwa) anaeleza kuwa, ili kupata maana kiuamali, ni sharti maswali kama kwa nini mwasilishaji ujumbe amesema hivi badala ya vile? Ni nini kilichomsukuma kusema hivyo? Ni nini kinaendelea maishani mwake? Na mengine mengi yaulizwe.

Kutokana na fafanuzi hizi, uamali ni mtazamo wa kifalsafa unaochunguza matumizi ya lugha kwa kuzingatia muktadha ambamo lugha fulani inatumiwa. Nadharia hii inasisitiza umuhimu wa muktadha katika uchunguzi wowote unaohusu matumizi ya lugha. Tunapochunguza mawasiliano kupitia maudhui ya nyimbo za jando yanayobadilika kiwakati, swala la matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali linaibuka. Lugha iliyotumiwa katika nyimbo za jando za Wakamba zilizochanganuliwa iliweza kufafanuliwa kutegemea wahusika, tamaduni za wahusika na uhusiano wa wahusika hao. Nadharia ya Uamali imetoa mwongozo wa kushughulikia mawasiliano kupitia kwa nyimbo za jando za Wakamba. Ili kuyaelewa mawasiliano haya, utafiti huu ulichunguza maudhui ya nyimbo za jando za Wakamba kama nyenzo ya mawasiliano kwa kujikita katika jamii zinamotumiwa.

Kwa muhtasari, nadharia ya Uamali ilitumika katika utafiti huu ili :

- i) Kushirikisha matumizi ya lugha kama nyenzo ya kufaulisha mawasiliano.
- ii) Kufasili maana ya maneno, ishara na vizianda lugha kulingana na muktadha.

1.8.3 Nadharia ya Uhalisia

Nadharia hii ilianza kutumika katika fasihi kule Ufaransa katikati mwa karne ya kumi na tisa. Miongoni mwa waasisi wake ni pamoja na Gustave Flaubert 1855 (Wamitila, 2002; Wafula na Njogu, 2007; Masinde, 2003; Lomatoro, 2014). Waandishi wengine wanaohusishwa na tapo hili ni Honore de Balzac na Emile Zola (Wamitila, 2002; Wafula na Njogu, 2007). Baadaye nadharia hii ilisambaa kule Uingereza, Urusi na Marekani. Chanzo cha nadharia hii kilikuwa matokeo ya misukosuko ya mapinduzi yaliyotokea mwaka wa 1848 huko Ulaya, hasa yale mapinduzi ya kisiasa na kiuchumi. Nadharia hii ilizuka kama njia mojawapo ya kupinga ulimbwende. Matamano ya kilimbwende yalikuwa ya kinjozi na yalikuwa yakihusu mambo yasiyowezekana (Wamitila, 2002; Wafula na Njogu, 2007).

Mbali na waasisi waliotajwa hapo juu, Wamitila (aliyetajwa) anaongezea kuwa tapo hili liliwekewa msingi na mwanafalsafa Hegel katika kitabu chake kinachojulikana kama *Aesthetic*. Hegel (1975,1979) alipendekeza matumizi ya neno uhalisia kuelezea kazi ya fasihi ambayo, inauwasilisha ulimwengu wa maisha ya kijamii ambako, kuna wahusika wanaotenda mambo kwa jinsi inayochochewa waziwazi na hali waliomo. Wamitila (2002) anasema kwamba, uhalisia humanisha kazi ya sanaa iliyo na wahusika ambao

matendo yao yanachochewa na hali ya kisaikolojia iliyowazunguka. Wamitila (aliyetajwa) anasema kuwa, msingi mkubwa wa tapo hili ni ‘usimulizi wa kimuhakati’ unaosimulia matukio kama yanavyotokea katika ulimwengu halisi. Kulingana naye, msanii anapaswa kutunga kwa kuyaakisi maisha ya kijamii katika ngazi za kijamii, kiuchumi, kitamaduni na kisiasa. Mtazamo huu unatilia mkazo uwasilishaji wa mambo ambayo yanaonekana katika jamii. Msanii anatarajiwa kutoa picha za matukio na mazingira ambayo yanaonekana kwa kiasi kikubwa ili kuchora maisha kama yalivyo. Kulingana na Wamitila (aliyetajwa), uhalisia unapinga aina ya majaribio. Msanii analazimika kuteua maudhui yenye uhalisia ambayo yatamwezesha kuyawasilisha maisha kwa usahihi.

Qusby (1988) akinukuliwa na Momanyi (1991), Wamitila (2002) na Masinde (2003) anasema kwamba, nadharia ya uhalisia ilianza kutumiwa kwa mara ya kwanza huko Ufaransa katika mwaka wa 1850 na waandishi kama Flaubert kueleza kazi za sanaa zilizojikita katika kuusawiri ulimwengu kama ulivyo, wala sio kama unavyofikiriwa kuwa. Naye Chiari (1960) anasema nadharia hii ilianza kutumiwa katika fasihi kwa sababu waasisi wake waliona kwamba, kuna uhusiano baina ya kazi ya sanaa na mtazamo wa msanii kuhusu mazingira. Aidha, anasema kazi ya sanaa hufumwa pamoja na ukweli wake ili kumsaidia binadamu kuelimika. Kwa mujibu wa Chiari, uhalisia huzingatia namna ukweli unavyosawiriwa katika nyakati mbalimbali. Jinsi ya kuusawiri na kuuelewa uhalisia hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Huu ndio msingi wa Wamitila (2002) kwamba, kila kizazi huwa na uhalisia wake na ndiyo sababu uhalisia katika kazi ya fasihi huwa ni swala la kijamii.

Naye Abrams (1988) anasema kwamba, uhalisia ni ukweli kama ulivyo katika mazingira halisi. Kulingana naye, kazi inayotungwa kwa misingi ya kihalisia yapaswa kuiga kwa karibu hali ilivyo katika ulimwengu halisi. Abrams (aliyetajwa) anashikilia kuwa, uhalisia huu unahusu uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu. Ana maoni kuwa, kazi za kisanaa zilizojikita katika mtindo wa uhalisia zinapaswa kuusawiri ulimwengu kama ulivyo wala sio kama unavyofikiriwa kuwa.

Aidha, Momanyi (1991) anashikilia kuwa, uhalisia humaanisha vitu thabiti vinavyohisika na mishipa ya fahamu ya binadamu pamoja na ukweli unaodhihirika katika kazi ya fasihi. Uhalisia wa kifasihi unaashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali, kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha. Kwa mujibu wa Momanyi (aliyetajwa), wahusika na wahakiki wengi waliotumia nadharia ya uhalisia waliamini kwamba, dhima ya msanii ni kuonyesha ukweli jinsi ulivyo, na kuchora taswira ya mazingira ambamo jamii inapatikana, bila kuidunisha wala kuipiga chuku. Kwa mujibu wa nadharia ya Uhalisia, msanii huchagua mambo anayotaka kuyazungumzia. Anachanganua na kutenganisha anayozungumzia ili aweze kusuta maovu ya kijamii. Baadhi ya wasanii huonyesha misimamo yao juu ya kile wanachokizungumzia. Hapa ndipo nadharia hii husawiri uhalisia hakiki, ambapo pamoja na msanii kujizatiti kuchora hali halisi ya maisha kupitia mabadiliko ya maudhui, hutetea watu fulani na kuwashambulia wengine kutegemea msimamo wake.

Kulingana na Ntarangwi (2004), nadharia ya uhalisia katika upana wake humaanisha uwakilishi wa uhalisi wa mambo katika fasihi. Kulingana na mwanafasihi huyu, nadharia

hii ilizuka katika karne ya kumi na tisa kwa lengo la kupinga mkondo wa ulimbwende. Anaendelea kusema kuwa, mhalisia huamini katika matokeo ya mambo na ukweli anaouzingatia ni ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa kwa tajriba. Hivyo basi, uhalisia hujikita katika mambo yaliyopo, tukio mahususi na matokeo yanayoweza kuthibitika. Imani ya mhalisia ni kwamba, kazi ya fasihi yapaswa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida wa kweli na halisi. Kwa mujibu wa Ntarangwi (2004), msanii hudhihirisha uhalisi wa mambo katika maudhui aliyoyazingatia, matukio, mazingira na wahusika aliowasawiri katika wakati maalum.

Wakichangia kuhusu nadharia ya uhalisia, Wafula na Njogu (2007) wanasema kwamba, nadharia hii inashikilia kuwa chimbuko la fasihi ni harakati za maendeleo ya binadamu kihistoria. Aidha, inasisitiza kuwa binadamu amepewa kipawa cha lugha na inafaa atumie lugha ili kuhamasisha jamii yake. Wanafasihi hawa wanatueleza kwamba, historia haiwezi kutenganishwa na fasihi. Fasihi nayo haiwezi kutenganishwa na masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Nao Wellek na Warren (1965), Lukacs (1972), Larkin (1977) na Njogu (1987) wanasema kazi yoyote ya fasihi hubadilika na wakati kusadifu uhalisia wa jamii husika. Nadharia inayofungamanisha fasihi na jamii ndiyo iliyoshika sana hasa katika 'ulimwengu wa tatu' chambilecho Njogu (1987). Hii ni kwa sababu inaonyesha kuwa, fasihi ni kielelezo cha hali halisi na inachukuliwa kama zana mojawapo ya kujihami dhidi ya mazingira makali. Nadharia ya uhalisia inaweza kutumiwa kama kifaa cha kuleta mabadiliko katika uhalisia ulioko.

Mihimili ya nadharia ya Uhalisia iliyoongoza utafiti huu ni kama ifuatayo:

- i) Hali zote za maisha ya kijamii huelezwa kupitia uhalisi wake kama unavyoonekana wala sivyo unavyofikiriwa kuwa.
- ii) Kazi ya msanii inapaswa kuwasilisha ukweli kama ulivyo katika mazingira halisi.
- iii) Msanii huzingatia matatizo ya jamii na kuchunguza chanzo chake.

Nadharia mseto zilizotumika katika utafiti huu zilichangiana pale ambapo nadharia moja ilishindwa kutekeleza majukumu yake.

SURA YA PILI

YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI

2.0 Utangulizi

Kuna tafiti zilizofanywa na maandishi yaliyoandikwa ambayo yanahusiana na mada ya utafiti. Kupitia sura hii, mtafiti ameonyesha mchango uliotoka kwa kazi hizo huku akibainishatofauti iliyopo na utafiti huu. Utafiti huu ulidurusu aina mbalimbali za maandishi kama ifuatavyo:

- a) Maandishi kuhusu historia ya Wakamba na mifumo yao ya kijamii.
- b) Maandishi kuhusu utanzu wa nyimbo.
- c) Tafiti kuhusu nyimbo kwa ujumla
- d) Tafiti kuhusu nyimbo za Wakamba

2.1 Historia ya Jamii ya Wakamba

Kulingana na Senkoro (1987), historia huipa sanaa uhai na mwelekeo. Ili kuielewa fasihi ya jamii yoyote ile, inabidikufahamu historia yake. Maoni ya Senkoro (aliyetajwa) yalitupa msukumo wa kuchunguza historia ya jamii ya Wakamba ili kuelewa nyimbo zao za jando na mabadiliko yaliyozikumba kulingana na mabadiliko ya kijamii.

Kikamba ni lugha inayozungumzwa na watu waitwao *Akamba* na katika umoja *Mukamba*. Wakamba wanaishi katika kaunti za Kitui, Machakos na Makueni.

Mahaliwanapoishi panaitwa Ukambani (Ndeti, 1972). Kulingana na Ndeti, neno *Mukamba* lilitokana na neno *amba* lenye maana ya kusema. Mwanzo wa Wakamba kuitana hivi ni wakati walipokuwa wakigawanyika kutoka sehemu walimokaa huko sehemu ya milima ya Kyulu (King’ei, 1982; Musyimi, 2011). Walipotoka sehemu zile, walianza kubishana wao wenyewe wakiulizana “*inywi mwiamba ata? Ko mwi andu ma kuamba kuamba*”? (sasa nyinyi mnasema nini? Kwani mmekuwa watu wa kusema sema tu?Hivyo, neno *Kikamba* lilitokana na mabishano hayo(King’ei, 1982; Musyimi, 2011).

Wakamba ni jamii moja katika makundi kadha ya Wabantu (Nurse & Spear, 1984;King’ei, 1982). Kundi la Bantu ndilo kundi kubwa nchini Kenya na lililo na makabila mengi yaliyo na uhusiano wa karibu. Kwa mujibu wa wavuti (<http://www.kenya-information-guide.com/kamba-tribe.html>), Wabantu wamo katika makundi mawili. Wanaoishi Magharibi mwa Kenya na wale wanaopatikana Mashariki mwa Kenya. Wabantu wanaopatikana Magharibi mwa Kenya ni pamoja na Abakuria, Abaluyia, Abagusii na Abasuba. Makundi ya Bantu yanayoishi maeneo ya Mashariki mwa Kenya ni Wakamba, Wataita, Agikuyu, Aembu, Ameru, Pokomo na Mijikenda.Guthrie (1967) anawaeleza Wakamba kama kundi la jamii ya Wabantu wanaopatikana Mashariki mwa Kenya.

Kulingana na Nurse & Spear, (1984), makazi ya kwanza ya Wabantu yanaelezwa kupitia nadharia kadha. Mojawapo ya nadharia hizi ni ile inayosema kuwa, maeneo yaliyo katikati mwa Nigeria na Cameroon ndiyo makazi ya awali ya Bantu. Kutoka maeneo ya Cameroon, kundi hili la Bantu lilihamia misitu ya Kongo ambako baadaye lilihamia

maeneo ya Afrika Mashariki kupitia maeneo ya ziwa Victoria, milima ya Taita na mlima Kilimanjaro. Kwa mujibu wa Nurse & Spear (1984), jamii ya Wakamba ilihamia sehemu zilizo karibu na mlima Kilimanjaro kati ya miaka 1400 na 1600. Wakamba walikuwa wakiita mlima huo *Kiima Kya Kyeu* (Mlima Mweupe).

Wakamba walikuwa wakifuga mifugo na pia walikuwa wawindaji. Walikuwa wakitumia mitego kuwatega wanyama wadogo ili kupata chakula. Kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na sita, Wakamba wakaanza kuhama kutoka sehemu zilizokuwa karibu na mlima Kilimanjaro kutokana na uvamizi wa *Akavi* (Wamasai) waliojulikana kama *Iloikop* (Nurse & Spear, 1984; Andrew & Salvadori, 1980). Kulingana na Nurse & Spear (waliotajwa), sehemu hii ilikuwa jangwa. Haikuwa na miti ya kuwasetiri kutoka kwa Wamasai wakati wa vita vya kuviziana. Kwa hivyo, Wakamba wakahamia sehemu za Kyulu([http://www.amazon.org/traditional african names.](http://www.amazon.org/traditional%20african%20names)).

Sehemu waliyoamia ya Kyulu ilikuwa na mawe makubwa na haikuwa na maji yakutosha kwa mifugo wao (Ndeti,1972). Kufikia karne ya kumi na saba, Wakamba wakahama sehemu ya Kyulu hadi Kibwezi ambapo pia walikumbana na ukavu kutokana na ukosefu wa mvua. Kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na saba, Wakamba wakahamia sehemu iliyoko karibu na Nzau. Kwa mujibu wa Andrew & Salvadori (1980), sehemu ya Nzau ilikuwa kavu na yenye mawe makubwa. Wakamba hawangeweza kulisha mifugo wao kutokana na ukosefu wa lishe na maji.

Kulingana na Ndeti (1972) na Nzioki (1982), ongezeko la jamii hii na matatizo mengine kama uvamizi wa jamii la Wamasai, uliwapelekea Wakamba kuhamia sehemu nyingine za Kaunti ya Machakos na wengine kuingia Kaunti ya Kitui walipohama Nzau. Kufikia mwanzoni mwa karne ya kumi na nane, wakahamia Milima ya Mbooni wakitafuta lishe ya mifugo wao. Milima ya Mbooni ilikuwa na misitu mikubwa, mito, mvua ya kutosha na mchanga wenye rotuba kwa hivyo, Wakamba wakaanza kilimo pamoja na ufugaji (<http://www.kenya-information-guide.com/kamba-tribe.html>). Vilevile, walikuwa wakiwinda nyati ambao walikuwa wengi sehemu hii. Baada ya kuishi Mbooni kwa mda wa karibu karne moja, baadhi ya Wakamba walihama sehemu za Mbooni kuanzia karne ya kumi na tisa wakaelekea sehemu za Wamunyu, Iveti na Kitui kutokana na ongezeko la watu (Ndeti, 1972; Musyimi, 2011).

Katika maeneo haya, Wakamba wakaanza kufanya biashara na watu kutoka pwani, Wagikuyu, Watharaka, Wambeere, Wasamburu na Wataita. Walikuwa wakibadilishana bidhaa zao kama mishale iliyokuwa na sumu, vibuyu vya ugoro miongoni mwa bidhaa nyingine nao wakapata wimbi, mtama maharangwe na mahindi (Ndeti, 1972; Andrew & Salvadori, 1980; King'ei, 1982; Nurse & Spear, 1984).

Nadharia nyingine kuhusu chimbuko la Wakamba ni kupitia fasihi simulizi yao inayoeleza kwamba, Wakamba walichimbuka katika mlima *Ngai* ulioko kaunti ya Machakos (Kimilu, 1962). Kisa asili hiki kinakubalika na Wakamba wa Machakos na Kitui. Kulingana na Kisa asili hiki, jamii ya Wakamba ilitokana na ndugu wawili

waliooana na kupata watoto. Watoto wakazaana na kuwa koo na mbari mbalimbali (Kimilu, 1962).

Nadharia nyingine inaeleza asili ya Wakamba, pamoja na jamii zingine za Kibantu wanazopakana nazo. Nadharia hii huhusishwa na baadhi ya wanahistoria na misitu ya Kongo (Nurse na Spear, 1984; Andrew& Salvadori, 1980). Kulingana na nadharia ya Kongo, inadaiwa kuwa Wakamba, Wakikuyu, Waembu, Wameru, Wapokomo, Mijikenda na jamii zingine zinazohusiana, zilihama kutoka Kongo na Kuingia nchini Kenya kupitia katikati ya ziwa Victoria na milima ya Taita. Baadaye, jamii hizo zilihamia pwani ya Kenya na kukusanyika mahali palipoitwa Shungwaya kati ya karne ya kumi na mbili na kumi na tano. Baada ya kuishi Shungwaya kwa karne mbili mkusanyiko huu ulivunjika kufuatia ongezeko la idadi ya watu, ambalo lilisababisha ukosefu wa chakula. Wakamba walitawanyika kuelekea sehemu za milima ya Kyulu, Mbooni, Kitui na Machakos kati kati ya karne ya kumi na sita na kumi na tisa.

Kwa sasa, Wakamba wanaishi katika kaunti za Kitui, Machakos na Makueni nchini Kenya. Eneo hilo lote hujulikana kama Ukambani. Hata hivyo, Kieti na Coughlin (1990) wanasema kwamba, kuna Wakamba ambao wanapatikana katika sehemu zingine kama Mwea katika Kaunti ya Embu, sehemu za pwani hasa Shimba hills katika wilaya ya Kwale, sehemu za Taita Taveta na Mombasa kisiwani.

Baadhi ya maeneo wanapoishi Wakamba huwa ni kavu na hupata mvua ya kiwango cha mililita 700 kwa mwaka na wakati mwingine mvua ikipungua hadi kiwango cha mililita 400 kwa mwaka kulingana na Kavyu (1980).

2.1.1 Jamii ya Wakamba Kabla ya Ukoloni

Kulingana na watafiti wa fasihi simulizi ya Wakamba kama vile (Mbiti, 1969; Kimilu, 1962; Ndeti, 1972; Nzioki, 1982; Kavyu, 1980; King'ei, 1982; Kieti, 1999), kipindi kilichotangulia wakoloni kilikuwa kabla ya mwaka wa 1906. Katika kipindi hiki, tamaduni za Wakamba zilikuwa zimekita mizizi katika nyanja zote kwani, hapakuwa na mwingiliano na kuathiriana na tamaduni zingine.

Hiki kilikuwa kipindi cha ujamaa katika jamii ya Wakamba (Mbiti, 1969). Watu waliishi kwa ushirika na walitekeleza shughuli zao za kitamaduni kwa mshikamano. Kulingana na Mbiti (1969), kila mwanajamii alikuwa ndugu wa mwingine. Mila na desturi zilizingatiwa na kila mwanajamii. Kila shughuli ilikuwa na nyimbo zake (Nzioki, 1982). Nyimbo hizi zilikuwa na maudhui na mitindo iliyodhihirika. Mitindo hii iliweza kusaidia katika kuwasilisha maudhui yaliyokusudiwa. Maudhui ya nyimbo zikiwemo za jando yalisawiri maisha katika uhalisia wa jamii hii.

Nyimbo zilitekeleza majukumu muhimu katika utamaduni wa Wakamba. Majukumu haya yalikuwa ni kuabudu Mungu, (*Mulungu*), kufariji, kukosoa, kuelekeza na kuhifadhi mila na desturi za jamii miongoni mwa majukumu mengine muhimu. Hiki ni kipindi ambacho tamaduni za Wakamba zilikuwa zimekita mizizi katika nyanja zote. Katika

sherehe kama za tohara, harusi, mazishi, miongoni mwa nyingine, wanajamii walifanya kazi pamoja kwa ushirika. Walisaidiana kulingana na koo zao. Waliabudu Mungu kupitia kafara na matambiko mbalimbali. Aidha, walikuwa na vita vya kuviziana vya mara kwa mara kati yao na jirani zao kama vile Wamasai na Wagikuyu.

2.1.1.1 Mpangilio wa Jamii

Katika jamii ya Wakamba, ukoo ulikuwa ni taasisi muhimu. Wanajamii waliokuwa katika koo mbalimbali walitegemeana kwa hali zote za maisha. Ukoo ulihusu watu ambao walikuwa wa nasaba moja kutoka kwa mzazi mmoja wa jadi (Kimilu, 1962). Wanaukoo fulani walikuwa na uhusiano wa karibu kiasi kwamba, waliitana kaka na dada. Koo kumi na mbili zilikuwa zimebainika vyema katika jamii hii mathalan: Atangwa, Aanziu, Auani, Atwii, Aombe, Ambua, Amuunda, Akitutu, Aiini, Akitondo, Amuui na Amwitu. (Nzioki, 1982; King'ei, 1982; Kieti na Coughlin, 1990). Koo za Wakamba zilihakikisha mshikamano wa kijamii na kuwapa Wakamba nafasi ya kujitambulisha kama jamii. Ni katika mfumo huu ambao yeyote katika jamii aliegemea wakati wa tatizo lolote lile. Ni dhahiri kwamba, mfumo wa kiukoo uliwapa wanajamii mshikamano ambao uliwawezesha kukabiliana na baadhi ya matatizo kama jamii moja (Kimilu, 1962).

Jamii ya Wakamba vilevile ilikuwa na mafunzo ya kijamii ambayo yalikuwa muhimu. Mafunzo haya yalipitishwa kupitia fasihi simulizi yao kama hadithi, vitendawili, methali, nyimbo zikiwemo za tohara miongoni mwa fasihi simulizi pana ya Wakamba. Umuhimu wa fasihi katika kupitisha mafunzo ya kijamii unaungwa mkono na wataalamu kama

Njogu na Chimerah (1999) na Wamitila (2003) ambao wanashikilia kuwa, fasihi ni zao la jamii na hutungwa ili kuelimisha, kuonya, kukosoa na kuburudisha jamii miongoni mwa dhima nyingi fasihi simulizi ya Wakamba ilichukua nafasi muhimu katika mafunzo ya kijamii ambayo yalipitishwa kutoka kizazi hadi kingine kwa njia ya mdomo (Kimilu, 1962; Mbiti, 1969).

Jamii ya Wakamba ilihusika katika kumwanda kila mwanajamii kulingana na mfumo wa maisha na maadili ya kijamii. Kwa mujibu wa Kimilu (1962), kupotoka kwa wanajamii hususan kuasi mila na tamaduni kulitokana na kutopata mafunzo kuhusu maadili ya jamii ya Wakamba. Kutopata mafunzo ya kimaadili chambilecho Mbiti (1969) kulisababisha kubadili dini kutoka dini ya Mwafrika na kupapia dini ya kigeni kama dini ya Kikristo. Kutokana na kupapia huku, wengi wa Wakamba wakakengeuka na kuwa *Asomba* (Wakamba wasomi wanaotumia lugha ya Kiingereza).

Uongozi katika jamii ya Wakamba ulilenga misingi ya ukoo. Wazee (*atumia*) ndio waliotwikwa jukumu la kuiongoza jamii na kushughulikia mambo ya kidini kama vile matambiko ya kijamii na kafara miongoni mwa mengine mengi (Nzioki 1982). Kulingana na King'ei (1982), umri, ndoa na uadilifu ndivyo vigezo vilivyotumiwa kuwateua viongozi. Wanaume katika jamii ya Wakamba walianza kutwikwa majukumu kadha baada ya kupashwa tohara (Mbiti, 1969). Pindi vijana walipofuzu sherehe za jando, waliitwa *anake*. Kundi hili lilitwikwa jukumu la kulinda jamii ya Wakamba. Mbele yao palikuwa na kundi lingine la *nthele* ambao walitwikwa majukumu ya uongozi. *Nthele* ni mwanamme ambaye amepitia sherehe ya tohara na kutiwa jandoni, ameo na ana watoto.

Nthele, alihitajika kupitia sherehe ya mpito ijulikanayo kama *kukula* ili awe *nthele* anaye tambulika na wanajamii (Kimilu, 1962; King'ei, 1982). Jamii ya Wakamba ilitegemea *atumia na nthele* katika uongozi na maamuzi ya kesi zozote zile za kijamii. Chifu naye aliteuliwa na baraza la *atumia ma kivalo*(taz. kiambatisho 1). Aliteuliwa kutokana na sifa kama *nthele* aliyeonyesha sifa za kuikimu familia yake vizuri bila misukosuko, aliyelimbikiza mali hususan mifugo na mashamba, mwaminifu, shujaa na aliyekuwa na busara.

King'ei (1982) anasema *atumia ma kivalo* walikuwa wazee wenye umri wa kuanzia miaka 50 na ambao walikuwa na tajriba kuhusu maisha ya wanajamii. Walipewa majukumu ya kuamua mambo yaliyopitishwa kwao na baraza la *nthele* pamoja na majukumu mengine. Waliongoza sherehe za kidini kama kutoa kafara pamoja na uongozi wa sherehe za tohara na mazishi katika jamii. Baraza la juu kabisa la uongozi lilikuwa kundi la *atumia ma kisuka*. Hawa ni wazee waliokuwa na umri wa kuanzia miaka 60. Walikuwa wamestaafu katika shughuli nyingi za kijamii. Waliachiwa hasa shughuli za kuongoza sherehe za kidini hususan utoaji wa kafara na sherehe za utakasaji.

Aidha, waliongoza sherehe za ulaji wa viapo maarufu kama *ithitu*(taz. kiambatisho 1) katika jamii hii. Vilevile,waliamua kesi nyeti kama vile mauaji na kesi za uchawi. Kesi nyingine ambazo hazikuwa nyeti sana kama vile za wizi wa mifugo, utovu wa nidhamu katika ndoa, kesi za kuamua mipaka ya mashamba miongoni mwa nyingine, ziliamuliwa na baraza la wazee la kiwango cha chini yaani *atumia ma kivalo*.

Jamii ya Wakamba haikuwa ya kitabaka. Waliendeleza ujamaa wa kiafrika. Shughuli kama kilimo hususan upanzi wa mimea, kupalilia, kuvuna, kuwinda ndege miongoni mwa nyingine zilifanywa kwa ushirikiano. Wakati wa kukaribisha mtoto, tohara, harusi na mazishi kila mwanajamii alihusika.

2.1.1.2Dini

Imani katika miungu ni tukio la kiulimwengu (Mbiti, 1969), kwa hivyo, jamii ya Wakamba ilikuwa na dini yao kama Waafrika wengine. Walikuwa na imani katika miungu kabla ya majilio ya wakoloni. Wakamba walikuwa wakitoa safara kwa miungu wao kwenye *mathembo* (Mbiti 1969, Kimilu, 1962). Walikuwa na imani na itikadi zao ambazo walizingatia. Walishiriki katika dini yao kufuatana na mafunzo waliyoyapata kutoka kwa mababu zao. Wakamba walilinda na kudumisha heshima zote za dini na utamaduni wao kwa kuweka miiko na ushirikina. Jamii ya Wakamba iliwafunza watoto dini yao wakiwa wadogo na mafunzo haya yaliendelea hadi uzeeni. Kila mwanajamii alishirikishwa katika sherehe tofauti za kidini ambazo zilikuwa sehemu ya maisha yao (Mbiti, 1969; Kieti na Coughlin, 1990).

Wakamba waliamini kuwepo kwa Mungu mmoja ambaye walikuwawanamwabudu. Mungu alipewa majina kadhaa. Baadhi ya majina haya yalielezea utendakazi wake hususan; *Mulungu* (Mungu), *Mumbi* (muumbaji), *Mwatuangi* (anayetenga vidole vya binadamu) na *Ngai* (anayegawa) (Mbiti, 1969; Kieti na Coughlin, 1990).

Katika jamii ya Wakamba, imani kwamba Mungu mkuu yuko kila mahali ipo kama ilivyokuwa tangu enzi za mababu zao. Matukio yote ulimwenguni yaliaminika kuwa na uhusiano na Mungu. Iliaminika kuwa, tokeo lolote baya lilitokana na adhabu ya Mungu kwa binadamu kutokana na vitendo vyao vya uasi. Jamii hii haikuwa na wakati maalum wa kuomba. Popote walipokuwa walikuwa wakitoa maombi yao kwa Mungu (Mbiti 1969). Utoaji wa kafara ulifanywa wakati wa shida na mema. Mbali na Mungu mkuu kulikuwa na miungu wadogo na pepo wabaya ambao waliathiri maisha ya watu. Miungu midogo iliaminika kuwa ndiyo iliwasaidia watu katika mambo yao ya kila siku.

Pepo wabaya nao waliaminika kuishi katika sehemu fiche kama pangoni, misituni na hata mahame (Kimilu 1962, Kavyu 1980, Kieti na Couglin 1990). Wakamba waliogopa sana pepo wabaya na athari zake. Watu waliogopa kwenda katika sehemu hizi haswa katika nyakati za usiku. Pepo wazuri nao waliaminika kuishi katika *ithembo* (mahali pa kutolea kafara) ambapo palikuwa ni chini ya mti ujulikanao kama *kiumo* (mgumo). Pepo wazuri waliaminika kuishi katika mti huo na ilikuwa mwiko kuukata (Mbiti 1969). *Atumia ma kisuka* na *awe* (waganga) walitwika jukumu la kuunganisha binadamu na Mungu. Aidha, waliongoza sherehe za kafara.

Vilevile, katika jamii ya Wakamba, mababu wa zamani waliheshimiwa. Wakamba waliamini na mpaka sasa wanaamini kuwa watu waliokufa bado wana mchango katika matukio ya watu walio hai (Somba 2000). Wanaheshimiwa, kusujudiwa na kuogopwa. Hili lilidhihirika kutokana na sherehe za mazishi anazopewa mwanajamii akiaga dunia iwapo alikuwa mtu mwema. Inaaminika kwamba hata mtu akifa hasa wazazi, wao

huendelea kuishi na aila yao na kuwakinga kutokana na mikosi. Utoaji wa kafara ulikuwa mojawapo wa njia za kumshukuru au kumtuliza Mungu. Wakati wa mvua nyingi na mavuno, kafara ilitolewa. Aidha, wakati wa mikasa kama vita, ukame, mafuriko, njaa, maradhi, mitetemeko ya ardhi au majanga yoyote yale, wanajamii walitoa kafara ili kuomba msamaha kwa Mungu (Nzioki, 1982).

Kulingana na Nzioki (aliyetajwa), mbuzi au kondoo wa rangi moja bila madoadoa yoyote ndiye aliyetolewa kafara kwa sababu alidhihirisha usafi. Sehemu mbaya za kondoo huyu zilitengewa pepo wabaya. Mababu walipewa kiwango fulani cha chakula au kinywaji kabla ya kila mwanajamii kuanza kula au kunywa. Hii ilikuwa ishara ya kuwatambua mababu. Kitendo hiki kiliitwa *kuthemba*. Ikiwa mtu yeyote alikula bila *kuthemba*, iliaminika angenyongwa na chakula hicho kama ishara ya kutotambua mababu.

Ingawa Wakamba wanaamini kuwepo kwa Mungu na wanamwabudu, kuenea kwa dini ya Kikristo na Kiislamu kumeathiri pakubwa dini asilia ya Wakamba. Wakristo waliozieneza dini hizi za kigeni waliwaogofya Wakamba kwa kuwaambia kuwa wataenda motoni kwa kufuata mila, desturi, utamaduni na itikadi zao. Mafunzo haya yalisababisha kupotea kwa baadhi ya mila nzuri kama za jando (Nzioki 1982).

2.1.1.3 Mfumo wa Kiuchumi

Kwa mujibu wa Chacha (1997), kuna uhusiano mkubwa kati ya uchumi na fasihi. Kulingana naye, hali ya uchumi huathiri sanaa iliyopo. Mfumo wa uzalishaji mali ukibadilika nayo fasihi hubadilika katika harakati za kudhihirisha mabadiliko hayo. Hivi

ni kumaanisha kwamba hali ya uchumi huelekeza fasihi. Kulingana na Senkoro (1987), chimbuko la sanaa ni mazingira halisi ya jamii; kwa hivyo, sanaa ni zao la mazingira. Mwanzoni, kabla ya majilio ya wakoloni, jamii ya Wakamba ilikuwa ni wawindaji na wakusanyaji matunda na mazao mengine ya mwituni. Walitegemea sana nyama kutoka wanyama wa porini kama vile paa, nguruwe wa mwituni, nyati miongoni mwa wanyama wengine. Pia, walikula matunda ya mwituni na mizizi.

Baadaye wakaanza kuwa wafugaji wa kuhamahama labda kwa sababu ya athari za Wamasai waliokumbana nao katika shughuli zao za kila siku. Kadri miaka ilivyokwenda Wakamba wakaanza kulima kama njia moja ya kuongezea uchumi wao. Kwa sasa, Wakamba ni wakulima na wafugaji. Walipanda na bado wanapanda mahindi, mtama, viazi vitamu na mihogo huku wakifuga ng'ombe, mbuzi, kuku na punda.

Kila shughuli ya kijamii ilikuwa na nyimbo maalum zilizoandamana nayo. Nyimbo hizo na ngoma walizocheza ziliwapunguzia makali ya maisha kwa kuwaburudisha (Nzioki, 1982). Katika jamii ya Wakamba, tajiri (*muthwii*) alikuwa yule ambaye alikuwa na ng'ombe wengi, wanawake na watoto wengi (Kieti, 1999; Nzioki, 1982). Ng'ombe na mbuzi walithaminiwa sana kwa sababu walitumiwa katika shughuli ya ulipaji mahari. Aidha, wanyama hawa walitumiwa katika utoaji kafara ili kutuliza au kushukuru miungu wao (Mbiti, 1969). Vilevile, wakati wa sherehe zozote zile kama za tohara, harusi, na mazishi, ng'ombe au mbuzi walichinjwa ili wanajamii washerehekee pamoja.

Mbali na ufugaji na ukulima, Wakamba walishiriki katika shughuli nyingine za kiuchumi kama uchongaji, utengezaji wa mizinga ya nyuki, utengezaji wa mapambo wakitumia madini ya aina ya chuma na pia biashara ya uhunzi (Kimilu, 1962; Nzioki, 1982; Andrew&Salvadori, 1980). Wakamba wangali wanashiriki katika shughuli hizi za kiuchumi na wanatambulika kwa biashara ya uchongaji katika sehemu ya Wamunyu katika Kaunti ya Machakos. Uchongaji na utengenezaji wa vinyago ulishika kasi baada ya vita vya kwanza vya dunia. Walijifunza uchongaji huu kutoka kwa Wamakonde wa nchi ya Tanganyika (Nzioki,1982).Uhunzi na uchongaji ilikuwa kazi ya wanaume nao wanawake wakifinyanga vyungu na kusuka vikapu (*syondo*)shughuli ambayo mpaka sasa inaendelea katika jamii hii.

Jamii ya Wakamba, kama vile utafiti huu ulivyotaja hapo juu, ilikuwa na uhusiano mkubwa na jamii nyingine kabla ya majilio ya Wakoloni. Kabla ya majilio ya wakoloni, Wakamba walikuwa wakifanya biashara na jamii za pwani na Waarabu.Walisafiri kutoka Kitui na Machakos hadi pwani ambapo waliwauzia Waarabu pembe za ndovu na vifaru, vinyago walivyovichonga, asali, ngozi za chui, mishale yenye sumu miongoni mwa bidhaa nyingine (Kavyu, 1980). Waarabu nao waliwauzia nguo, mapambo na nyaya za shaba walizotumia kutengenezea mitego ya wanyama na mapambo (Kimilu,1962). Vilevile, walishiriki biashara na jamii nyingi jirani hasa Wakikuyu, Wamasai, Waambu na Wambeere kama utafiti ulivyotaja awali. Biashara hii ilihusu kubadilishana mazao ya shambani na vifaa vya uchongaji.

Wanawake ndio walioshiriki katika biashara hii kwa sababu kulingana na Nzioki (1982), hawakuchukuliwa kuwa mahasimu na jamii jirani kama wanaume. Hivi sasa, Wakamba wanategemea kilimo cha mseto kikiwa ndicho uti wa mgongo wa uchumi wao. Vyakula vya kitamaduni kama vile kunde, mbaazi, maweale, mtama, viazi vitamu bado vinakuzwa. Mahindi na maharagwe pia ni maarufu katika jamii hii. Mbali na kuwa wakulima, Wakamba wanafuga wanyama kama mbuzi, ngombe na kuku. Ng'ombe na mbuzi bado wanatumiwa katika shughuli ya ulipaji mahari kama ilivyokuwa katika jamii hii kabla na baada ya majilio ya wakoloni.

2.1.1.4 Mahusiano ya Kiuana

Jamii ya Wakamba ilikuwa ni ya kibabedume. Mwanamume ndiye aliyekuwa kiongozi wa familia na ndiye aliyekuwa mmiliki wa mali. Urithi ulikuwa ni kwa mwanaume pekee hata ingawa siku za hivi karibuni, wanaume wengi wameanza kuona umuhimu wa kuwarithisha mabinti zao. Taasisi zilizodumisha sheria na utangamano kama vile utafiti huu ulivyobainisha awali zilisimamiwa na wanaume. Wanawake katika jamii ya Wakamba wana hadhi duni. Hali hii inaendelea kubadilika kadri maendeleo katika jamii yanavyozidi kupatikana.

Mwanamke alipaswa kumnyenyekea mumewe na pia alipaswa kuwa na heshima kwa wanaume wote kwa jumla. Mwanamke huwa amenyimwa uhuru. Akikosewa na mumewe, imani za kijamii hazimkubalii kukabiliana na mumewe moja kwa moja. Anapaswa kutumia mtu ambaye anaweza kuwa ni mavyaa na marika na mumewe ambao huwa na haki ya kumwadhibu kwa niaba ya mumewe kama itabainika kwamba

bibi hana heshima. Sifa za mwanamke mzuri katika jamii ya Wakamba ni pamoja na unyenyekevu, uvumilivu, subira na utiifu kwa wanaume kama ilivyo katika jamii nyingi za Kiafrika.

Ndoa ilimpelekea mwanamke kuwa mali ya mumewe. Kulipa mahari kunaashiria kwamba mwanamke sasa amemilikiwa na mwanaume aliyemlipia mahari na hapasi kurudi kwao baada ya mahari kulipwa hata kama atateswa kiasi gani. Kiwango cha mahari aliyolipiwa mwanamke katika jamii hii ni ng'ombe watatu na mbuzi kumi na wawili. Mahari haikulipwa mara moja mbali ililipwa polepole kulingana na uwezo wa jamii fulani. Jukumu la kimsingi kabisa mke akiolewa ni kupata watoto. Anatarajiwa kupata watoto haswa wa kiume ili kuendeleza kizazi cha mwanaume na ukoo mzima. Mwanamke ambaye alishindwa kupata watoto alidharauliwa na wanajamii kwa kuitwa *nthata*(tasa). Mumewe aliruhusiwa kuoia tena ili kupata mtoto wa kiume. Mke huyu tasa alinyimwa haki za kimapenzi na mumewe na hakuwa na ruhusa ya kurudi kwao au kuolewa tena. Lazima akae kwa mumewe huku akiwa anahudumu kama kijakazi au mtumwa (Nzioki, 1982).

Miongoni mwa jamii ya Wakamba, wanawake walitwikwa majukumu mengi kuliko wanaume. Wao ndio hugawiwa kazi nyingi. Wanaume hutekeleza majukumu kama ujenzi wa nyumba, Kuchunga mifugo na majukumu mengine kama kulima. Wanawake nao huezeka nyumba kwa nyasi, hupanda, hupalilia, huwinda ndege, huvuna na kuhifadhi mavuno hayo. Aidha, huakikisha kuwa ng'ombe wamekamwa. Kazi za nyumbani kama

kupika, kulea watoto ni majukumu ya wanawake katika jamii ya Wakamba (King'ei, 1982).

2.1.1.5 Tohara ya Wakamba

Tafiti mbalimbali zimeonyesha kwamba, tohara katika jamii ya Wakamba zilianza zamani na ziliambatanishwa na nyimbo katika awamu mbalimbali (Kingei, 1982; Nzioki, 1982; Kavyu, 1980; Somba, 2000; Watuma, 2001; Wathome, 2009). Wasichana walipashwa tohara punde tu walipovunja ungu nao wavulana walipashwa tohara baada ya kubaleghe. Umuhimu wa tohara haukuwa katika kitendo cha kutahiri pekee, bali ulikuwa katika mafunzo ambayo watahiriwa walipewa ili kuwatayarisha kwa utu uzima katika utamaduni wao.

Kipindi cha tohara kilikuwa ni wakati wa kuwatayarisha vijana ili kuchukua wajibu wa uhalisia wa maisha ya utu uzima na ulikuwa wakati wa kufungamanisha vijana na utamaduni wa jamii yao. Vijana walifundishwa kuhusu utamaduni na maadili ambayo yalikubalika katika jamii. Aidha, sherehe ya tohara ilikuwa ni mojawapo ya mifumo ya kuunganisha jamii ya Wakamba.

Kulingana na Kimilu (1962), tohara katika jamii ya Wakamba iliwezesha vijana kuwa na maadili licha ya kuwatoa kutoka ujana hadi utu uzima. Jamii ya Wakamba ilikuwa na aina tatu za tohara:

- (i) Tohara ndogo (*Nzaiko nini*)

- (ii) Tohara kubwa (*Nzaiko nene*)
- (iii) Tohara ya kucheza (*Nzaiko ya ngingo*)

Kwa mujibu wa Kavyu (1980), watahiriwa walipaswa kupitia tohara hizi tatu kwa nyakati tofauti ili wawe wanajamii kamili.

2.1.1.5.1 Tohara ndogo (*Nzaiko nini*)

Tohara hii kulingana na King’ei (1982) ilifanywa kati ya mwezi wa Juni hadi Septemba kila mwaka. Hii ni kutokana na sababu kwamba, huu ni wakati wa kiangazi katika sehemu za ukambani. Wakamba, kwa mujibu wa King’ei waliamini kwamba, wakati wa kiangazi ndio mwafaka kwa sherehe za jando kwani vijana walipona haraka wakati wa jua kali kuliko wakati wa mvua. Kulingana na Wathome (2009), siku chache kabla ya tohara hii, pombe (*kaluvu*) ilikuwa inaandaliwa na chakula kingi kupikwa na wazazi wa watahiriwa na kupelekwa mahali pa kufanyia tohara maarufu kama *nzaikoni*(taz. Kiambatisho, 1). Chakula hiki kililiwa na kila mwanajamii aliyehudhuria sherehe ya tohara. Ilikuwa ni njia moja ya kuleta wanajamii pamoja.

Pombe ilikuwa ya ngariba (*mwaiki*), wasaidizi wake (*avwikii*) pamoja na wazee wa *kivalo* na *kisuka* walioongoza sherehe hizi. Pombe ilimwagwa chini kiasi kidogo kabla ya kunywa ili mizimu washiriki pia. Iliaminika kwamba kwa kufanya hivyo, waliwasaidia watahiriwa kupona haraka. Hadi leo katika sehemu ya utafiti, tambiko hili hufanywa na wanavijiji hivi huamini kwamba watahiriwa hupona haraka kutokana na baraka za miungu wao.

Sherehe za tohara zilifanywa na bado hufanywa katika sehemu tatu: nyumbani kwa mtahiriwa, nyumbani kwa ngariba au nyumbani kwa msaidizi wa ngariba marufu kama *Muvwikii*. Kwa mujibu wa Kavyu (1980), siku tatu kabla ya tohara ndogo, wazazi wa watahiriwa walihitajika kufanya tambiko la ngono maarufu kama *kwaika mwana* yaani kutahiri mtoto. Wanajamii waliamini kwamba, tambiko hili lisipofanywa, watahiriwa wanaweza kufa au kuchukua muda mrefu kupona. Wakati wa ‘kukata’, ngariba alitumia kisu kilicho na makali maarufu kama *wenzi* (taz. *Kiambatisho 1*). Katika jamii ya Wakamba, watahiriwa na ngariba pamoja na wasaidizi wake walipewa zawadi (Wathome, 2009). Zawadi hizi zilitolewa na kila mwanajamii haswa watu wa ukoo wa watahiriwa. Zilikuwa pamoja na mbuzi, ng’ombe, kuku, asali na shanga. Kwa watahiriwa, zawadi hizi zilichukuliwa kama mali ya kwanza na ilijulikana na bado inajulikana kama *ngulukilyo* yaani kufukuza utoto na kuingia utu uzimani. Zawadi hizi ziliashiria umuhimu wa tohara kwani, ikiwa mtu hajatahiriwa, alichukuliwa kama mtoto na hakurithishwa mali wala kuwa kiongozi wa jamii ya Wakamba.

Kabla ya sherehe, watahiriwa waliimba nyimbo ili kuashiria hamu yao kubwa ya kutahiri ili waruhusiwe kufanya mapenzi kama vile mishororo hii katika wimbo *Ningukuna vilingi* (Nitapiga filimbi, Na,1) inavyohibitisha:

<i>Ningukuna vilingi</i>	Nitapiga filimbi
<i>Niiliila yiima</i>	Natamani shimo
<i>Yiima ya mundu muka!</i>	Shimo la mwanamke

Wimbo huu licha ya kuwa na lugha ya utusani una ujumbe. Unaashiria tamaa ya watahiriwa kutahiriwa ili waweze kuoza na kutenda kitendo cha kujamiiana na wake zao. Lugha ya utusani ilikubaliwa katika muktadha wa sherehe za tohara. Wakingoja siku ya

tohara, watahiriwa walielimishwa kuhusu ugumu wa maisha na shida za kifamilia ambazo wangekumbana nazo pindi wapatapo jiko. Baada ya tohara ndogo, watahiriwa walikaa pamoja na wakati huu ndipo walipopewa zawadi zao. Kukaa pamoja kulizidisha umoja na ushirikiano wao na kujenga msingi thabiti wa undugu.

2.1.1.5.2 Tohara kubwa(Nzaiko nene)

Madhumuni ya tohara hii yalikuwa ni kuwaelimisha watahiriwa kuhusu mambo mengi hususan siri za jamii, mila na tamaduni, majukumu ya kiuana, mambo ya unyumba, historia ya jamii na mawaidha kuhusu utu uzima. Sherehe hizi ziliongozwa na wasimamizi wao maarufu kama *avwikii* na kusimamiwa na *atumia ma kivalo*. Sherehe hizi kulingana na Kavyu (1980) zilifanywa wakati wa kiangazi kati ya mwezi wa Agosti na Septemba. Zilichukua kati ya siku sita na kumi. Vijana waliruhusiwa kuo baada ya kupitia sherehe ya tohara kubwa. Nyimbo ziliimbwa katika sherehe hizi ili kuwaelimisha watahiriwa kuhusu maisha ya ndoa na majukumu mengine. Kila siku, nyimbo mahususi ziliimbwa ambazo zililingana na muktadha wa jamii hii. Mfano wa nyimbo zilizoimbwa wakati wa jando kubwa ni kama wimbo Na. 9 *Nitilwe mindo* (Nikatwe kitu). Sehemu ifuatayo inaonyesha hamu ya watahiriwa ya kurithi mali baada ya tohara:

<i>Ninitilwe mindo</i>	Nikatwe kitu
<i>Ninitilwe oyu</i>	Nikatwe sasa
<i>Mundu utemutile mindo</i>	Mtu ambaye hajakatwa kitu
<i>Ti mundu</i>	Si mtu
<i>Nithi ngasunge mbui sya nau</i>	Niende nikatunze mbuzi wa baba

Wimbo huu unasheheni maudhui ya umuhimu uliopewa tohara katika jamii ya Wakamba. Shughuli hii ilichukuliwa kama ngazi muhimu katika ukuaji wa mwanajamii kutoka

utotoni na kuingia utu uzimani. Sherehe ya jando katika jamii ya Wakamba ilitumiwa kama tambiko la upisho. Wimbo huu unaonyesha majukumu ambayo yaliandamana na tohara. Mtahiriwa anasema *nitilwe mindo, nitilwe oyu* (nikatwe kitu, nikatwe sasa) katika mshororo wa 1 na wa 2 kuonyesha hamu yake kubwa ya kutahiriwa. Katika mshororo wa 5 anasema *nithi ngasunge mbui sya nau* (niende nikatunze mbuzi wa baba) kumaanisha kurithi mali ya babake.

2.1.1.5.3 Tohara ya Kucheza (*Nzaiko ya Ngingo*)

Tohara hii ilifanywa baada ya tohara kubwa. *Asingi* (watahiriwa) walipelekwa msituni ili kufunzwa ulengaji shabaha. Walitumia mti kama window. Sherehe hii ilikuwa kama kujiburudisha na kuwafunza namna ya kukinga jamii yao. Tohara hii ilikuwa maarufu kama *kuatha mbusya* yaani kuwinda kifaru. Kifaru katika muktadha wa tohara hii alikuwa wa kidhahania. Kilikuwa kipande cha mti ambacho kilitengenezwa kwa njia maarufu ili kitumike kwa shughuli ya kuwinda kifaru. Kilikuwa na shimo ndani ambapo kiongozi mmoja wa sherehe hii angeingia na kutoa sauti ya kifaru Kieti (1999). Watahiriwa walipaswa kukabiliana na mnyama huyo bila kuonyesha woga. Kumwinda na kumuua kifaru huyo kuliashiria kwamba, watahiriwa wako tayari kurudi makwao na kulinda jamii kutokana na uvamizi wowote ule. Aidha, tohara hii ilikuwa na dhima ya kuwaelimisha watahiriwa kuhusiana na matarajio ya jamii kwao kama inavyosisitizwa katika wimbo wa *mwaikwa ndaneenaa na kivetu kyeene* (Na. 2) kupitia mishororo hii:

<i>Mwaikwa ndaneenaa na kivetu kyeene</i>	Mtahiriwa hatongozi mke wa wenyewe
<i>Mwaikwa kua mbusya tuthi</i>	Mtahiriwa ng'oa kifaru twende
<i>Ula unuukia akome</i>	Anayeogopa alale
<i>Ula waikitwe ndaneenaa na kivetu kyeene</i>	Aliyetahiriwa hatongozi mke wa mwingine

Wimbo huu uliimbwa siku ya mwisho ya tohara yaani siku iliyotangulia kwenda nyumbani kutoka msituni. Madhumuni ya wimbo huu ilikuwa kuwashauri watahiriwa kuhusu mambo ya mapenzi. Watahiriwa walionywa dhidi ya kutongoza wake wa wenyewe. Hii ilikuwa ni kwa sababu, jamii hii ilishikilia msimamo wa kudumisha maadili ya jamii. Watahiriwa walipaswa kuwaheshimu wanawake ambao wameolewa na hawakupaswa kufanya ngono nao. Maneno ‘ng’oa kifaruru twende’ (*kua mbusya tuthi*) yametumiwa kulingana na muktadha wa tohara hii. Yana maana kuwa, yule aliyesemekana kuwa ni kifaruru si kifaruru halisi mbali ni kinyago tu kilichomwakilisha kifaruru wa kawaida. Watahiriwa wanaambiwa wamg’oe waende nyumbani kwa sababu sherehe imefikia kikomo. Ili kuelewa maana na maneno hayo, itabidi tuelewe muktadha wa tohara hii. Hymes (1974) anasema kuwa muktadha ni muhimu katika mawasiliano. Kulingana naye, yaliyosemwa katika nyimbo za jando yalitendeka kwa sababu yalisemwa katika muktadha wa jando.

Siku ya mwisho katika tohara hii, watahiriwa walikatwa *nthoo* (taz. Kiambatisho 1) katika sehemu zao za siri na kupakwa dawa (Wathome, 2009). Mkato huu uliashiria baraka ili wapate watoto wengi wakioa. Baadaye, walifumkana na kuenda nyumbani ambapo walipewa zawadi ziiwazo *ngulukilyo* kuashiria kwamba, sasa wazazi wao wamehitimisha jukumu lao kwao na kuanzia wakati huo, wangukuwa wakijitegemea Mbiti (1969).

Wakitoka msituni, walipaswa kufuatana kwa safu moja huku wakiimba wimbo *Nau niwandila* (Baba amenitahiri, Na. 3). Mishororo ya wimbo huu ifuatayo inaashiria dhima ya kutiwa jandoni:

<i>Aliili! Nau niwandila</i>	Aliili! baba amenitahiri
<i>Niwambumya utunduuni</i>	Amenitoa ujingani
<i>Aliili ! Nau niwandila</i>	Aliili! baba amenitenga

Wimbo huu unaashiria furaha ya mtahiriwa. Anasifia babake kwa kumpeleka kwa tohara ambapo sasa amekuwa mtu mzima kulingana na utamaduni wa tohara katika jamii ya Wakamba. Vilevile, babake amemtoa ujingani na kumtenga. Kumtenga katika mshororo wa 3 kuna maana kuwa, mtahiriwa ametengwa na kundi la wavulana ambao hawajatahiriwa. Kuondolewa ujingani katika muktadha huu ina maana ya kuvuka ngazi ya utotoni hadi utu uzima ambapo, watahiriwa wanaelimishwa kuhusu, majukumu yao ya utu uzima, mambo ya unyumba, siri za jamii, masuala kuhusu mapenzi miongoni mwa mengine.

Tohara ni mila ambayo huthaminiwa sana na jamii za Kiafrika zinazotekeleza desturi hii (Mwaniki, 1986). Mwaniki anaeleza kuwa katika jamii nyingi za Kiafrika, ni lazima mtu kupitia katika tambiko la tohara afikishapo umri fulani. Mtu ambaye hajashiriki katika tambiko hili katika jamii zilizoendeleza utamaduni huu alichukuliwa kama mtoto hata kama ni mzee (Nang'oli, 2000; Kobia, 2008a). Kutokana na umuhimu wa tambiko hili, wavulana walionyesha hamu kubwa ya kuipitia pindi tu walipofikisha umri wa kutahiriwa ili wawe wanajamii kamili.

2.1.2 Jamii ya Wakamba Baada ya Ukoloni

Baada ya wakoloni kuingia Kenya na kuingia katika jamii ya Wakamba, vikorombwezo vya kitamaduni viliporomoka na athari ya mshikamano, mila na desturi za jamii ya Wakamba zikaanza kubadilika (Kimilu,1962; Mbiti, 1969;Kavyu,1980;Nzioki, 1982 Kieti na Coughlin, 1990).Kuathirika huku kulianza kuonekana baada ya mafunzo ya dini haswa ya Kikristo. Mafunzo haya yalibadilisha mwelekeo wa maisha ya jamii. Shughuli mbalimbali za kitamaduni zilibadilika hususan ndoa zikaanza kufungwa kanisani, tohara za wasichana zikaanza kupigwa marufuku kutokana na mafunzo ya dini ya Kikristo na tohara za wavulana zikawa zinafanyiwa hospitalini. Nyimbo za jando zikachukuliwa kuwa dhambi kwa madai kuwa zinaeneza ushetani (Kieti, 1999; Wathome, 2009). Kufuatia hali hii, nyimbo za jando za Wakamba zikaanza kupata mwelekeo mpya. Mitindo na maudhui yazo yakaanza kubadilika kusawiri mabadiliko haya ya kijamii.

Kipindi cha baada ya majilio ya wakoloni kilikuwa kipindi cha misukosuko na vita ambacho kilivuruga umoja wa Wakamba, na kuuvunja ugwe uliokuwa umeiunganisha jamii hii (Mbiti, 1969). Utamaduni wa Wakamba ukaanza kupata athari za kimagharibi. Majilio ya wamishenari yalileta mabadiliko makubwa katika mifumo na harakati zote za maisha ya jamii. Wamishenari walileta dini ya Kikristo ambayo ilikita mizizi kwa kasi mno na kusababisha kuporomoka kwa mfumo wa kuabudu na imani zote walizokuwa nazo za kidini.

Mipangilio na taratibu za maoni na maombi zikabadilika (Nzioki, 1982; Kieti na Couglin, 1990). Mabadiliko ya kidini na kuanzishwa kwa elimu ya kizungu kulisababisha kukengeuka kwa Wakamba. Walianza kuiga mienendo ya wazungu hususan kupapia elimu ya kujua kusoma na kuandika pamoja na dini ya wazungu haswa Ukristo. Fasihi simulizi iliyokuwa muhimu katika kupitisha mafunzo ya kijamii ilianza kudidimia. Maswala mengi ya kijamii kama vile tohara, harusi, na mazishi miongoni mwa mengine yakaanza kutekelezwa kwa kuzingatia imani na dini ya kikristo. Kipindi cha pili kinajumuisha kile cha baada ya uhuru. Kipindi hiki kilikuwa kati ya mwaka 1963 na 1980. Katika kipindi hiki, Kenya ilikuwa imepata uhuru na Wakenya walikuwa wameanza kujenga taifa jipya lenye maono na maazimio tofauti. Baada ya uhuru, mifumo ya uongozi ilibadilika. Watawala wavya wakaendeleza utaratibu wa uongozi wa wakoloni. Mabadiliko haya yalivuruga na kuathiri uongozi miongoni mwa jamii ya Wakamba (Nzioki, 1982; Somba, 2000; Watuma, 2001).

Jamii ya Wakamba hii leo imebadilika pakubwa. Mabadiliko haya yamesababishwa na mfumo wa uongozi, msisimko wa teknolojia mpya ya mawasiliano, elimu ya kizungu, kukua kwa miji na viwanda, maendeleo ya nyanja mbalimbali za kiuchumi, dini ya Kikristo miongoni mwa mabadiliko mengine (Kavyu, 1980; Kieti, 1999; Kilauni, 2007; Watuma, 2001; Wathome, 2009). Wakamba wengi kama ilivyo katika jamii nyingi za Kiafrika wamehama mashambani na kwenda kuishi mijini. Mabadiliko haya yameathiri kwa kiwango fulani fasihi simulizi yao. Nyimbo na ngoma za kitamaduni zimeathiriwa na mabadiliko haya na zingine kusahaulika (Kilauni, 2007; Wathome, 2009). Kubadilika huku kunatokana na sababu kwamba, ngoma na nyimbo ni kipengele cha utamaduni wa

watu ambao kila siku unaendelea kuzaliwa, kuathiriwa na kubadilika jinsi maisha yanavyobadilika.

2.2Maandishi kuhusu Utanzu wa Nyimbo

Nyimbo ni kipera cha fasihi simulizi ambacho hutekeleza majukumu muhimu katika jamii zaidi ya kipera kingine chochote kile cha fasihi simulizi (Wamitila, 2002).Kwa mujibu wa Mbarwa (1989), nyimbo zina dhima muhimu katika jamii hasa katika kuwasilisha maoni, mitazamo na mielekeo ya watu kuhusu masuala kadha yakiwemo ya kijamii. Mbarwa (aliyetajwa) anashikilia kuwa nyimbo ni ala muhimu za mawasiliano ambazo hutumia maneno katika tamathali za usemi ili kupitisha ujumbe kwa walengwa wake.

Wataalamu wengi wameshughulikia utanzu wa nyimbo. Miongoni mwao ni pamoja na Finnegan (1970). Finnegan alijihusisha na aina za nyimbo hususan nyimbo za wawe, nyimbo za sifa za mashujaa vitani na za wasasi mawindoni huku akionyesha jinsi wimbo ulivyotumika katika maisha ya kila siku.Amedhihirisha jinsi wimbo ulivyotumika katika maisha ya kila siku. Aidha, amedhihirisha jinsi wimbo ulivyotumikakutetea haki za wafanyakazi waliojikuta katika mazingira ya unyanyasaji hasa katika nchi zilizotawaliwa na wakoloni. Amebainisha kuwa, nyimbo zinaweza kutumiwa kama chombo cha kujitetea.Vilevile, Finnegan (1970)aliainisha umuhimu wa nyimbo katika jamii za Kiafrika na jinsi dhima ya nyimbo hizi inavyobainika. Anasema nyimbo ni chombo mwafaka cha fasihi simulizi kinachoongoza jamii kufikia malengo ya ufanisi. Anaendelea kubaini kuwa,nyimbo huchukua jukumu kubwa la kuelimisha,

kutahadharisha, na kuburudisha jamii inayohusika. Kazi ya Finnegan iliweka wazi maoni kwamba, umuhimu wa nyimbo hupatikana kupitia maudhui na mtindo wa nyimbo hizo. Kazi ya Finnegan (1970) ilichangia utafiti huu kupitia maudhui ya nyimbo aliyofafanua pamoja na majukumu ya nyimbo aliyoshughulikia japo, alijifunga katika nyimbo jadii ya kwa jumla.

Kazi nyingine iliyokuwa muhimu kwa utafiti huu ni ya Kipury (1983). Alishughulikia nyimbo za tohara za Wamasai. Katika kazi yake, Kipury alianisha nyimbo za tohara za Wamasai zilizoimbwa wakati wa tohara katika vipindi tofauti. Aidha, alibainisha kuwa nyimbo za jando za Wamasai huweza kueleweka kupitia mitindo ya lugha iliyotumiwa katika utunzi wa nyimbo hizo. Katika kazi yake, alianisha mitindo ya lugha inayotumiwa kupitisha ujumbe unaokusudiwa kupitia nyimbo za jando za Wamasai. Kazi yake ilichangia hii kupitia vipengele vya kimtindo alivyoshughulikia. Vilevile, maelezo aliyotoa Kipury kuhusiana na dhima ya nyimbo katika kuchunguza uhalisia wa kijamii yalichangia utafiti huu. Utafiti huu pia ulinufaika kupitia majukumu ya nyimbo za jando aliyobainisha Kipury (1983).

Watafiti wengine walioandikia utanzu wa nyimbo ni Nandwa na Bukenya (1983). Wasomi hawa wana maoni kuwa, nyimbo za kisasa zinazingatia maswala ya kisasa lakini zina sifa za fasihi simulizi. Waimbaji wana ubunifu mkubwa wa maneno na lugha wanayoitumia ni teule. Nyimbo hizi huimbiwa hadhira lengwa. Kulingana nao, nyimbo za kisasa zina maudhui ya kisasa na hubadilika kadri jamii inavyobadilika. Kazi ya Nandwa na Bukenya (1983) ilikuwa muhimu kwa utafiti huu kupitia vipengele

walivyovichanganua hususan lugha, maudhui na hadhira lengwa ya nyimbo za kisasa. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ya Ethnografia ya mawasiliano inasisitiza umuhimu wa lugha na hadhira lengwa ili wimbo uweze kuwa na utendakazi muhimu katika jamii.

Aidha Mbiti (1991) anasema kwamba, nyimbo, methali na hekaya zinapatikana katika jamii nyingi za Kiafrika. Fani hizi huwa zinatokea katika kipindi maalum na huwa na ujumbe unaobainika. Aidha, huwa na maudhui maalum kuhusu nyanja fulani ya maisha. Maudhui ya nyimbo aliyoyashughulikia Mbitiyalinufaisha utafiti huu kwani yanafafanua kuwa,nyimbo hutokea katika kipindi mahususi na huwa na maudhui maalum kuhusu nyanja fulani ya maisha. Maudhui ya nyimbo kwa mujibu wa Mbiti (aliyetajwa) hubadilika mara kwa mara dai ambalo utafiti huu ulinua kubainisha. Ingawa Mbiti (1991) alishughulikia mabadiliko ya maudhui, alijishughulisha na tanzu mbalimbali za fasihi simulizi tofauti na utafiti huu ambao ulijifunga katika mabadiliko ya maudhui katika nyimboza jando za jamii ya Wakamba.

Wakisisitiza kuhusu umuhimu wa nyimbo katika jamii, Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa, nyimbo na mashairi simulizi ndiyo yalikuwa vitabu na magazeti ya wanajamii ambao hawakuwa na maandishi. Wanaendelea kusema kuwa, nyimbo na mashairi yalitumiwa kuhifadhi sheria, historia, jiografia na sosholojia kwa kurithishana kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kulingana na Njogu na Chimerah (waliotajwa),mambo muhimu kama majukumu ya kiuana, kashfa, ndoa, na maswala ya kimapenzi yalihifadhiwa katika nyimbo. Kazi yao ilifaa utafiti huu kwa kutoa data muhimu kuhusu nyimbo katika jamii za Kiafrika.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), nyimbo husheheni mawazo na huonyesha uhusiano wa kijamii. Kulingana naye, nyimbo huchukua sehemu kubwa ya maisha ya binadamu. Mwanafasihi huyu anasema takriban shughuli zote za maisha ya binadamu kama kulima, kujenga, kumbembeleza mtoto, kupasha tohara na kuvuna, huandamana na nyimbo. Vilevile, Wamitila (aliyetajwa) ameeleza dhana ya nyimbo na kufafanua dhima ya utanzu huu wa fasihi simulizi katika jamii. Aidha, ameanisha nyimbo mbalimbali kulingana na dhima zake. Kuhusu nyimbo za tohara, anasema zinatumika katika shughuli ya kutahiriwa kwa wavulana na wasichana. Kwa mujibu wake, nyimbo za tohara hupitisha maswala muhimu kuhusu jamii kwa watahiriwa na wanajamii wengine. Aidha, anasema kwamba nyimbo za tohara hutumiwa kumjua mwanajamii matarajio ya jamii, kumpa maelekezo kuhusiana na majukumu yake katika jamii, kuonya na kutahadharisha miongoni mwa majukumu mengine ya nyimbo za tohara. Kazi ya Wamitila (2002) iliufaa utafiti huu kupitia majukumu na maudhui ya nyimbo za tohara aliyoshughulikia.

Kadhalika, Ngure (2003) amefafanua sifa za nyimbo pamoja na vipengele vinavyozingatiwa na watunzi wa nyimbo ili kupitisha ujumbe kwa walengwa wao. Kulingana naye, nyimbo hubeba mawazo, fikra, falsafa na hisia za msanii katika kuziwasilisha kwa hadhira yake. Ngure (aliyetajwa) anashikilia kuwa wimbo unaweza kuhusiana na maisha, utamaduni, siasa, dini, elimu na mazingira. Vipengele hivi ni muhimu katika uchanganuzi wa ujumbe wa mwimbaji. Lengo moja la utafiti huu lilikuwa kuchunguza namna ambavyo msanii wa nyimbo za jando za Wakamba hubadilisha maudhui kwa mujibu wa wakati, ili kuibua mawasiliano anayokusudia. Kazi ya Ngure (2003) ilichangia utafiti huu kulitimiza lengo hilo.

Kwa mujibu wa King'ei na Kisovi (2005), nyimbo zimeenea miongoni mwa jamii mbalimbali na huimbwa kuambatana na shughuli tofauti. Kulingana na wanafasihi hawa, nyimbo za jandoni na unyangoni zinapatikana katika jamii nyingi hata zile haziwapashi wasichana tohara lakini zilikuwa na mila kama hizo zamani. King'ei na Kisovi (waliotajwa) wameainisha nyimbo katika makundi mawili makuu. Nyimbo za kimapokezi na zile za kisasa. Nyimbo za kimapokeo wanasema hupokezwa kizazi hadi kingine. Lengo kuu la nyimbo za kisasa kulingana nao ni kuchuma mali. Wanasema nyimbo za kisasa zina uwazi mwingi, maneno hayana adabu na midundo yao ina ucheshi mkubwa.

Sifa hizi zilitufaa katika kuchanganua mabadiliko katika nyimbo za jando za kisasa katika jamii ya Wakamba. Vilevile, King'ei na Kisovi (2005) wanaeleza kwamba, mwimbaji huteua mambo kadha muhimu yanayoathiri jamii nzima ya binadamu na kuyaendeleza kama maudhui ya jamii yake. Wanaongezea kwamba, si kila mara mtunzi wa kazi ya sanaa huchukua maudhui moja kwa moja kutokana na matukio ya kijamii bali, huweza kutunga kwa kutaka kulifurahia tukio maalum lililomsibu yeye peke yake. Kipengele cha maudhui walichoshughulikia King'ei na Kisovi (2005), pamoja na mambo yanayomsukuma mtunzi wa nyimbo kutunga, kulingana na uhalisia wa maisha kiliufaa utafiti huu.

Isitoshe, M'Ngaruthi (2008) ameweka nyimbo katika makundi mbalimbali likiwemo kundi la nyimbo za tohara zilizochunguzwa na utafiti huu. Kuhusiana na nyimbo za tohara, M'Ngaruthi anarai kwamba, nyimbo hizi hupatikana katika makabila yote ya

Kibantu. Anaongeza kusema kuwa,nyimbo za tohara hulenga kuwakusanya pamoja watahiriwa ili kuwasifu na kuwapa moyo,kuukejeli woga, kuwatayarisha watahiriwa katika majukumu yao ya kiutu uzima na kuwatayarisha kukabiliana na kisu cha ngariba bila woga. Kazi ya M'Ngaruthi (2008) ilichangia utafiti huu kupitia vipengele vya maudhui na majukumu yanayotekelezwa na nyimbo aliyoyashughulikiaambavyo utafiti huu ulivichunguza.

2.3 Tafiti kuhusu Nyimbo kwa Jumla

Mbali na maandishi kuhusu nyimbo, kuna tafiti mbalimbali ambazo zimeshughulikia mada ya nyimbo kwa kuongozwa na nadharia tofauti. Kwa mfano Mkimbo (1981) alishughulikia nyimbo za kisiasa za Kiamu wakati wa uchaguzi wa mwaka 1974/5. Alichunguza jinsi ambavyo nyimbo zinaweza kutumiwa kueleza matumaini na matarajio ya watu. Alidhihirisha kuwa, kuna uhusiano wa karibu kati ya nyimbo na masuala ya kisiasa. Kulingana na Mkimbo (aliyetajwa), nyimbo ni kama silaha ya kisiasa na zina uwezo mkubwa wa kubadilisha mkondo wa siasa katika jamii. Katika utafiti wake, Mkimbo (aliyetajwa) anashikilia kuwa, nyimbo zina nguvu za kutekeleza majukumu ambayo maneno hayawezi kutekeleza vilivyo. Kazi yake iliongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamaa na ilifanikiwa kubainisha kuwa, nyimbo ni utanzu muhimu wa kisanaa unaoweza kusababisha mabadiliko katika jamii. Utafiti huu ulinufaika na kazi ya Mkimbo kupitia majukumu ya nyimbo aliyoyashughulikia. Aidha, nadharia ya uhalisia wa kijamaa aliyotumia katika utafiti wake ilichangia utafiti huu kupitia mihimili yake ambayo inakaribiana na ya nadharia ya uhalisia iliyoongoza utafiti huu. Hata hivyo,

utafiti wa Mkimbo (1981) ni tofauti na huu kwani utanzu wa nyimbo alioshughulikia ni tofauti na uliolengwa na utafiti huu.

Aidha Mwaniki (1986) alifanya utafiti kuhusu tamaduni za Waembu. Katika utafiti wake, alisawiri nyimbo kama kipengele muhimu cha fasihi simulizi katika jamii ya Waembu. Kulingana naye, nyimbo hutumika katika kila hafla ya kijamii hususan tohara, ndoa na mazishi. Utafiti wake ulilenga kubaini nyimbo zinazotawala shughuli za kijamii ukiwemo utaratibu wa tohara katika jamii ya Waembu. Vilevile, alishughulikia maudhui yaliyomo katika nyimbo hizi. Utafiti wa Mwaniki uliufaa utafiti huu kupitia maudhui ya nyimbo aliyoshughulikia hata ingawa ametafitia jamii tofauti na inayolengwa na kazi hii. Hata hivyo, utafiti wake unatofautiana na huu kwa sababu lengo lake kuu lilikuwa kuchunguza utamaduni wa jamii ya Waembu, ambapo utanzu wa nyimbo unajitokeza kama kipengele muhimu cha utamaduni huo. Alishughulikia utanzu wa nyimbo kwa jumla huku akibainisha umuhimu wa nyimbo katika kila sehemu ya utamaduni wa Waembu. Mwaniki hakulenga kubainisha kuwa mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za jando huakisi mabadiliko ya kijamii kama vile utafiti huu ulivyofanya.

Kazi ya Nkonge (1988) ilijishughulisha na mtindo na maudhui katika nyimbo za Joseph Kamaru ambapo, alijaribu kuchunguza jinsi Kamaru anavyochota maudhui yake kutoka matukio ya kijamii na yale ya kisiasa nchini Kenya. Nkonge (aliyetajwa) alibainisha kuwa, nyimbo za Kamaru zinabadilika kulingana na matukio ya kijamii ya kisiasa yakiwepo. Fauka ya hayo, Nkonge amedhihirisha jinsi baadhi ya vipengele vya miundo ya lugha vilivyoweza kutumika katika kuibua maudhui ya nyimbo za Kimaru. Maelezo

hayo yalichangia utafiti huu kupitia vipengele vya lugha alivyoainisha na jinsi vinavyoweza kuibua maudhui ya nyimbo kimpito wakati. Zaidi ya hayo, utafiti wa Nkonge ulikuwa muhimu kwa huu kupitia uanishaji wa matukio ya kijamii yanayochangia kubadilika kwa maudhui ya nyimbo za Kamaru. Lengo moja la utafiti huu lilikuwa kuchunguza matukio ya kijamii yanayochangia mabadiliko ya maudhui ya nyimbo za jando za Wakamba. Aidha,kipengele cha maudhui alichochunguza kiliufaa utafiti huu hata ingawa utanzu wa nyimboalioshughulikia ni tofauti na uliolengwa na utafiti huu.

Mtafiti mwingine aliyeshughulikia utanzu wa wimbo ni Mbarwa (1989). Katika kazi yake, Mbarwa alibainisha kuwakatika jamii nyingi za Kiafrika, nyimbo zina dhima muhimuhasa katika kuwasilisha mitazamo, maoni na mielekeo ya watu kuhusu maswala ya kijamii. Kulingana na Mbarwa (aliyetajwa),nyimbo hutumia tamathali za usemi mathalan jazanda, taswira, tashbihi, tashihishi miongoni mwa tamathali nyingine za usemi ili kuibua maudhui. Ameainisha nyimbo katika makundi kadha hususan nyimbo za sifa, ukaribisho, maombi, kutoa shukrani, za kishujaa, bembelezi, nyimbo za kukashifu, nyimbo za malalamiko na nyimbo za ushauri.Mbarwa alibainisha kuwa, nyimbo zina utendakazi muhimu katika shughuli za kijamii. Kupitia kwazo,mielekeo ya watu katika jamii hubainika. Utafiti wa Mbarwa (aliyetajwa) ulikuwa na manufaa katika utafiti huu kupitia maudhui na majukumu ya nyimbo aliyoshughulikia.Hata hivyo, hakujiunga katika kipengele cha mabadiliko ya maudhui katika nyimbo kama vile utafiti huu ulivyofanya, kupitia nyimbo za jando za Wakamba.

Maudhui ya utetezi yametafitiwa na Ntarangwi (1990) katika nyimbo za Remi Ongala. Mwanafasihi huyu anabainisha kuwa,nyimbo zina dhima kubwa katika kutetea maslahi ya wanajamii. Kulingana naye, nyimbo zenye maudhui ya utetezi hutoa malalamiko kwa niaba ya mtu au watu fulani dhidi ya hali ya maisha isiyoridhisha. Utafiti wa Ntarangwi uliongozwa na nadharia ya uyakinifu wa kijamaa. Utafiti wa mwanafasihi huyu unarai kwamba,maudhui ya wimbo huonyesha uhalisia wa kijamii katika historia ya wakati wake, jambo ambalo utafiti huu ulilenga kubainisha kupitia nyimbo za jando za jamii ya Wakamba.Kazi yake ilikuwa muhimu katika utafiti huu kwa sababu amechunguza uhalisia wa jamii unaomulikwa na wasanii kupitia nyimbo zao suala ambalo lilizingatiwa katika utafiti huu kupitia nyimbo za jando za jamii ya Wakamba. Vilevile, Ntarangwi (1990) ameshughulikia kipengele cha maudhui sawia na utafiti huu ulivyofanya. Tofauti iliyoko baina ya utafiti wa Ntarangwi (1990) na huu ni kwamba, alishughulikia nyimbo za kisasa za mtunzi Remi Ongala ilhali huu ulishughulikia nyimbo za jando miongoni mwa jamii ya Wakamba.

Akitafiti kuhusu umuhimu wa nyimbo katika jamii, Chesaina (1991) alidhihirisha kuwa, nyimbo kama utanzu wa fasihi simulizi zinaweza kutumiwa kama chombo cha kuwazindua wanajamii waliokandamizwa na utamaduni wa kijadi. Chesaina anarai kuwa, wimbo kama utanzu wa fasihi simulizi ni chombo muhimu cha kuelezea hisia wakati wa kuingia sherehe ya mpito miongoni mwa wanawake. Aidha, alidhihirisha kuwa nyimbo huweza kutumiwa kama jukwaa la kupinga udhalimu wowote unaoendelezwa na utamaduni. Chesaina (aliyetajwa) aligundua haya kupitia utafiti wake kuhusu nyimbo kama chombo cha kuelezea umoja wa kijinsia miongoni mwa wanawake

Waembu na wanawake Wambeere. Utafiti wa Chesaina ulikuwa muhimu kwa kazi hii kupitia majukumu ya nyimbo za unyago aliyobainisha ambayo yana ukuruba na majukumu yanayotekelezwa na nyimbo za jando. Pia utamaduni wa Waembu na Wambeere una ukuruba na utamaduni wa Wakamba; kwa hivyo, kazi hii ilinufaika kutoka kwa kazi yake. Hata hivyo, utafiti wa Chesaina ni tofauti na huu kwa sababu alijifunga katika sherehe ya unyago ilhali utafiti huu ulishughulikia nyimbo za jando za Wakamba.

Kazi ya Yalwala (1991) ilishughulikia maudhui katika nyimbo za John Mwale ambapo alitathmini maudhui haya kwa mujibu wa muktadha uliyoazalisha. Maudhui yaliyojadiliwa ni yale ya siasa, umoja, uzalendo na maadili katika jamii. Yalwala amechunguza namna maudhui ya nyimbo yanavyoweza kuathiri jamii na jinsi nyimbo hizo zinavyoleta ufahamu na umoja katika jamii yake. Utafiti wa Yalwala uliufaa huu kupitia kipengele cha maudhui alichoshughulikia sawa na utafiti huu. Vilevile, alifafanua umuhimu wa kipengele cha muktadha katika utunzi wa nyimbo kama vile utafiti huu ulivyolenga kubainisha. Hata hivyo, kazi yake ni tofauti na hii kwa kuwa alijifunga katika nyimbo za msanii John Mwale ilhali huu ulijifunga katika nyimbo za jando za jamii ya Wakamba.

Utafiti mwingine uliochangia huu ni wa King'ei (1992). Mwanafasihi huyu amechunguza nafasi ya nyimbo za taarabu nchini Kenya kati ya miaka ya 1963 hadi 1990. Utafiti wake ulizingatia lugha, utamaduni na mawasiliano. King'ei amebainisha chanzo, maendeleo na msambao wa nyimbo za taarabu. Pia, utafiti wake umegusia

mtindo wa nyimbo za taarabu. Amebainisha namna watunzi wa nyimbo za taarabu wanavyoathamini usanifu wa kiisimu na uelewa kisanaa. King'ei(aliyetajwa) ameeleza kuwa,ingawa nyimbo za taarabu ni maarufu kama njia ya kueleza matukio ya kijamii miongoni mwa Waswahili, bado nyimbo hizi zinasawiri taswira hasi za wanawake ambao hawajajikomboa katika jamii. Utafiti wa King'ei unaelekea kuwarai watunzi wa nyimbo za taarabu wabadilisha maudhui ya nyimbo zao ili ziibue taswira halisi ya mwanamke Mswahili aliye huru kulingana na mabadiliko ya wakati.Vilevile, King'ei (1992)amefafanua maudhui ya nyimbo za taarabu pamoja na utendakazi wake katika jamii. Umuhimu wa utafiti wa King'ei kwa huu ni kupitia kipengele cha maudhui ya nyimbo alichochunguza hata ingawa alishughulikia utanzu wa nyimbo za taarabu tofauti na utafiti huu, uliojifunga katika nyimbo za jando za Wakamba. Pia, kazi ya King'ei iliongozwa na nadharia ya Ethnografia ya mawasiliano. Utafiti wake uliufaa huu kupitia maelezo na mihimiliya nadharia ya Ethnografia ya mawasiliano iliyotumiwa na utafiti huu. Aidha, kazi yake iliupa utafiti huu msukumo kuhusiana na utendakazi wa nyimbo aliofafanua katika utafiti wake.

Mtafiti mwingine aliyeshughulikia nyimbo za tohara katika jamii za Kiafrika ni Matti (1996). Matti alishughulikia sanaa za maonyesho za Kiafrika za jadi akitumia mfano wa tohara ya Watharaka. Katika kazi yake, Matti amefafanua sifa muhimu ambazo hutambulisha nyimbo za tohara katika jamii ya Watharaka hususan, hakuna idadi ya mishororo inayowekwa ya urefu wa wimbo. Hii ni kwa sababu urefu wa wimbo hutegemea msanii na hadhira. Pia, aligundua kuwa msanii wa nyimbo ana uwezo wa kuubadilisha wimbo na kuufanyia marekebisho ili uweze kukidhi mahitaji ya jamii. Licha

ya kubainisha sifa za nyiso, Matti alishughulikia utendakazi wa nyiso katika jamii husika akiongozwa na nadharia ya utendaji. Utafiti wake ulinufaisha huu kupitia majukumu yanayotekelezwa na nyiso kipengele ambacho utafiti huu ulishughulikia ukirejelea nyimbo za jando za jamii ya Wakamba.

Utafiti kuhusu nguvu na uwezo wa nyimbo kwa wanawake wa Waswahili ulishughulikiwa na Mwai (1997). Katika utafiti wake, Mwai amegundua kuwa ingawa wanaume wa jamii za Waswahili wana uwezo uliokithiri katika ndoa, wanawake wamebuni njia zao za kueleza hasira zao, maumivu na mateso yao wakitumia nyimbo na ngoma zilizotungwa na kuimbwa na wanawake. Hisia za wanawake Waswahili kulingana na Mwai (aliyetajwa) hudhihirika kupitia maudhui katika nyimbo. Mwai alilenga kubainisha kuwa, nyimbo zina utendakazi muhimu katika jamii ya Waswahili. Kupitia kwa nyimbo, wanawake wanapitisha hisia zao kwa wanaumme ili mabadiliko yaweze kupatikana. Utafiti wa Mwai uliufaa huu kupitia kipengele cha maudhui alichoshughulikia, na pia utendakazi wa nyimbo aliochunguza hata ingawa utanzu wa nyimbo alioshughulikia, pamoja na jamii aliyoitafitia ni tofauti na utanzu wa nyimbo za jando ulioshughulikiwa na utafiti huu.

Kazi ya Obote (1997) ilishughulikia wajibu wa nyimbo katika ujenzi wa mahusiano ya nguvu za kiuana katika jamii ya Karachuonyo, kwa kuzingatia masuala ya itikadi na kijamii. Obote alizingatia mbolezi, nyimbo za kusifu na nyimbo zinazoangazia masuala ya kijamii kuhakiki mahusiano ya kiuana katika jamii ya Waluo. Obote anarai kuwa, nyimbo zilizokusanywa na kuhakikiwa zinadhihirisha kuwa, ubaguzi wa kiuana

unadidimia polepole na mahali pake kuchukuliwa na itikadi inayotambua uwezo wa mtu binafsi. Obote (1997) alidhihirisha kuwa, nyimbo ni makisio ya watu kuhusu tajriba zao za kijamii, kisiasa na kiuchumi na hutumiwa na watu katika jamii kuwasilisha maoni na msimamo wao. Utafiti wa Obote ulilenga kubainisha kuwa, nyimbo hutumiwa na wanajamii kuwasilisha maoni na msimamo wao kuhusu maswala fulani ya kijamii. Hata ingawa kazi ya Obote ilikuwa na lengo tofauti na utafiti huu, utafiti wake ulikuwa na manufaa kwa kazi hii kwakurejelea kipengele cha maudhui alichoshughulikia ili kufikia lengo lake.

Akichunguza uhusiano wa kiuana katika sherehe ya tohara miongoni mwa Wamaragoli, Indangasi (1997) anatoa rai kuwa, pana haja ya tafiti zaidi kufanywa kuhusu mielekeo inayobadilika kuhusiana na sherehe ya tohara katika jamii tofauti za Kiafrika. Kupitia utafiti wake, aligundua kuwa sherehe ya kutahiri, miongoni mwa Wamaragoli, ni njia muhimu ya kueleza uhusiano wa kiuana. Kupitia nyimbo za tohara, wanaume Wamaragoli hupata kijisababu cha kuwadhulumu wanawake kupitia kwa matumizi ya lugha ya matusi. Kwa vile kazi ya Indangasi imeshughulikia utanzu wa nyimbo uliotafitiwa na kazi hii, utafiti wake uliupa huu msukumo kuhusiana na utendakazi wa nyimbo za jando kipengee kilichotiliwa maanani katika utafiti huu.

Kadhalika, Kanake (2001) alishughulikia mabadiliko na maendeleo ya tohara ya wanawake katika jamii ya Wameru kutoka Tharaka. Kanake kupitia utafiti wake alibainisha kuwa, sherehe ya unyago na nyimbo zinazoandamana na sherehe hii zinasahaulika kutokana na sababu kwamba, mila hii inapigwa vita na serikali, makanisa,

mashirika yasiyo ya kiserikali na vikundi vinavyotetea haki za watoto. Utafiti wa Kanake ulinufaisha huu kupitia dhima ya nyimbo za tohara alizoainisha.

Utafiti wa Mutwiri (2005) ulitathmini utendakazi wa nyiso katika jamii ya Watigania na kubainisha mitazamo inayozuka kuhusiana na utendakazi wa nyiso hizo. Aidha, ulichunguza dhima ya nyiso na mabadiliko ya dhima ya nyiso hizo katika jamii ya Watigania. Utafiti wake uligundua kwamba, ingawa kuna mabadiliko ya maisha kama vile athari ya ukoloni, ubepari, dini, sayansi na elimu ya kisasa, nyiso zinaendelea kuimbwa katika jamii ya Watigania. Mutwiri aligundua kuwa, hii ni kwa sababu majukumu yaliyokuwa yakitekelezwa na nyiso bado ni muhimu. Ingawa majukumu mengine yamebadilika, nyiso nazo zimebadilika ili kutosheleza mahitaji ya wakati wake. Lengo lingine la Mutwirilikuwa kuchunguza jinsi majukumuyaliyotekelezwa na nyiso yalivyoathiriwa na mapisi. Mutwiri aliongozwa na nadharia ya uamali hasa kipengele cha utendi-unenaji cha Austin (1962). Utafiti huu ulinufaishwa na ufafanuzi wa Mutwiri kwamba, maudhui katika nyimbo huweza kubadilika kutokana na mabadiliko ya utamaduni yanayotokea katika jamii. Zaidi ya hayo, alishughulikia nyimbo za tohara sawia na utafiti huu japo alichunguza jamii tofauti na iliyolengwa na utafiti huu. Aidha, Mutwiri alichunguza utendakazi wa nyiso katika jamii ya Watigania kipengele kilichoupa utafiti huu msukumo. Vilevile, utafiti huu ulinufaika na kazi yake kuhusiana na ufafanuzi wa mihimili ya nadharia ya Uamali iliyoongoza utafiti huu. Hata hivyo, utafiti wa Mutwiri ulikuwa na lengo tofauti na utafiti huu. Alilenga kubainisha mitazamo ya utendakazi wa nyiso katika jamii ya Watigania, ilhali huu ulilenga kubainisha mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za jando za Wakamba.

Akichunguza nyiso za Waluhya kuhusiana na maudhui na lugha, Simiyu(2007) alilenga kubainisha kuwa, matumizi ya lugha ni muhimu katika uwasilishaji wa ujumbe katika kazi ya fasihi. Aidha, katika kazi yake, Simiyu anarai kuwanyimbo hutungwa kwa kuiga mifumo ya zamani na kuimbua mifumo mipya kutokana na mambo yanayotokea katika maisha ya wanajamii. Umuhimu wa utafiti wa Simiyu ni kwamba, alishughulikia kipengele cha maudhui ya nyimbo za tohara sawia na utafiti huu. Kazi hii ilinufaishwa na ufafanuzi wa Simiyu kwamba, maudhui katika nyimbo huweza kubadilika kutokana na mabadiliko ya kijamii. Aidha, aliongozwa na nadharia ya ethnografia ya mawasiliano sawa na utafiti huu. Ufafanuzi aliofanya wa mihimili ya nadharia ya ethnografia ya mawasiliano uliufaa utafiti huu. Hata hivyo, Simiyu alikuwa na malengo tofauti na utafiti huu jambo ambalo liliweza kutoa matokeo tofauti kati ya utafiti wake na huu. Aidha, jamii iliyolengwa na utafiti wa Simiyu ni tofauti na jamii ya Wakamba iliyolengwa na utafiti huu.

Matumizi ya lugha kitamathali huweza kufanikisha ujumbe unaotolewa kupitia nyimbo. Hoja hii inaungwa mkono na Malenya (2008), kutokana na uchunguzi wake wa matumizi ya lugha na jazanda katika nyimbo za Jacob Luseno. Malenya (aliyetajwa) anarai kuwa, fasihi simulizi ni sanaa inayochochewa na hali halisi katika mazingira ya kijamii hususan yale ya kitamaduni. Alijaribu kubainisha kwamba, lugha na jazanda alizotumia Luseno zinaafikiana na matukio katika vipindi vyote vya utawala nchini Kenya. Aidha, Malenya alishikilia kuwa, nyimbo huathiri maisha ya watu kihisia na kimaudhui kuliko tanzu nyingine. Hii ni kutokana na jinsi zinavyowasilishwa katika jamii kwa njia ya moja kwa moja au kupitia kanda mbalimbali za nyimbo.

Utafiti wake ulibainisha kuwa, nyimbo hutungwa kulingana na mazingira hasa ya kisiasa na hubadilika kimaudhui na kilugha kulingana na utawala uliomo. Kwa mujibu wa Malenya (2008), Luseno alitunga nyimbo wakati wa vipindi vitatu katika utawala wa Kenya hususan wakati wa hayati mzee Kenyatta, mstaafu rais Moi na kipindi cha utawala cha rais mstaafu Mwai Kibaki. Katika vipindi hivi vitatu, mabadiliko ya nyimbo yalitokea ambapo mtunzi alilazimika kutumia mbinu za lugha kama jazanda ili kusitiri ujumbe wake mzito. Malenya aliongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamaa kufikia malengo yake. Ufafanuzi aliolea kuhusiana na nadharia ya uhalisia wa kijamaa, pamoja na mihimili ya nadharia hiyo aliyoainisha ilinufaisha utafiti huu ambao uliongozwa na nadharia ya uhalisia ambayo ina ukuruba na nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Utafiti huu pia ulinufaishwa na ufafanuzi wa Malenya kwamba, maudhui katika nyimbo huweza kubadilika kutokana na mabadiliko ya kijamii yakiwemo ya kisiasa yanayotokea katika jamii. Tofauti ya utafiti wa Malenya na huu ni kwamba, alishughulikia nyimbo za msanii Luseno tofauti na utanzu wa nyimbo za jando za Wakamba uliochunguzwa na utafiti huu.

Akichunguza taswira za kiuana, Kobia (2008) amehakikimajukumu, itikadi na mahusiano ya kiuana katika jamii ya Waigembe kupitia uchunguzi wa nyimbo za tohara. Taswira za kiuana katika nyimbo za tohara za wanaume zimehakikiwa ili kuibuka na mwonoulimwengu unaokubalika katika jamii ya Waigembe kuhusu mwanamume na mwanamke katika jamii hii. Utafiti wa Kobia (aliyetajwa) umebainisha kuwa, nyimbo za tohara katika jamii ya Waigembe hutumia taswira kisani ili kudhihirisha itikadi ya kiuana ya Waigembe, kukemea maovu ya kijamii, kufichua na kuwakejeli waliopotoka

kimaadili katika jamii. Kobia aliongozwa na nadharia za Uana, Utendaji na Uamali ili kufikia malengo yake. Anatoa rai kupitia utafiti wake kwamba, fasihi simulizi ya Kiafrika itumike kama chombo cha maendeleo kinachotambua wanaume na wanawake kama washiriki katika maendeleo. Umuhimu wa utafiti wa Kobia ni kwamba, alishughulikia nyimbo za tohara za Waigembe ambao wana utamaduni sawa na jamii ya Wakamba iliyoshughulikiwa na utafiti huu. Aidha, kazi yake imetilia mkazo vipengele vya lugha, mazingira, wahusika na utamaduni ambavyo vilitiliwa maanani na utafiti huu kuchanganua maudhui ya nyimbo za jando za Wakamba. Vilevile, utafiti huu ulinufaika na kazi yake kuhusiana na ufafanuzi wa mihimili ya nadharia ya Uamali kwani ilitumika katika kuongoza utafiti huu. Tofauti iliyopo kati ya kazi ya Kobia (2008) na utafiti huu ni kwamba, alilenga kuchunguza taswira za kiuana katika nyimbo za tohara za Waigembe ilhali huu, ulilenga kubainisha mabadiliko ya kimaudhui ya nyimbo za jando za Wakamba.

Wakichunguza wajibu wa nyimbo pendwa katika siasa, Mwamzandi na Nkichabe (2008) wamebainisha kuwa, nyimbo pendwa zinadhihirisha hali ya utaiifa nchini Kenya katika kipindi cha baada-ukoloni. Katika kazi yao, wametumia nadharia ya udenguzi wa maana katika diskosi ya kisiasa nchini Kenya. Wanasema kuwa wameongozwa na madai kwamba, nyimbo kama sehemu ya fasihi pendwa hutekeleza wajibu maalumu wa kimawasiliano. Aidha, wanashikilia kuwa kazi yoyote ile ya fasihi hubadilika kutokana na swala la wakati, dai ambalo lilichunguzwa na utafiti huu kupitia nyimbo za jando za Wakamba.

Kazi ya Rajwayi (2009), ilichunguza maudhui na mtindo katika nyimbo za msanii Faustin Munishi. Rajwayi aliangazia mabadiliko kimaudhui yaliyotokea katika nyimbo za kidini za Munishi kimpito wakati. Pia, alibainisha lugha iliyotumiwa katika uwasilishaji wa ujumbe wa msanii Munishi. Rajwayi alishughulikia nyimbo za msanii huyu zilizoimbwa kati ya kipindi cha kati ya mwaka 1980 hadi 1995. Utafiti wake ulitufaa hasa kuhusu uchanganuzi wa maudhui na lugha. Hata hivyo, Rajwayi alishughulikia nyimbo za kidini tofauti na utanzu wa nyimbo za jando zilizotafitiwa na utafiti huu. Vilevile, alitumia nadharia ya maadili tofauti na nadharia zilizoongoza utafiti huu jambo ambalo liliweza kuibua matokeo tofauti kati ya tafiti hizi mbili.

Utafiti mwingine uliozingatiwa ni wa Mutegi (2010). Huyu alichunguza suala la maigizo kama sehemu ya shughuli zinazojitokeza katika sherehe za tohara za jamii ya Wameru. Kulingana naye, *Kirarie*, katika nyimbo za tohara za Wameru ni aina ya sanaa ya maigizo kinyume na maoni ya baadhi ya wasomi wa kimagharibi na wa Kiafrika kuwa, Afrika haijakuwa na sanaa ya maigizo. Mtafiti huyu alilenga kubainisha kuwa, madai ya kutokuwa na sanaa ya maigizo barani Afrika hayana mashiko yoyote. Kazi yake ilitilia maanani dhima ya maigizo ya *kirarie* katika jamii ya kisasa ya Wameru. Utafiti wake uligundua kwamba, *kirarie* katika nyimbo za tohara za Wameru ina sifa za sanaa ya maigizo. Umuhimu wa kazi ya Mutegi ni kwamba, alishughulikia dhima ya nyimbo za tohara katika jamii ya Wameru kipegele ambacho kilitufaa. Hata hivyo, malengo yake ni tofauti na yaliyolengwa na utafiti huu, hivyo matokeo ya kazi yake na hii ni tofauti.

Utafiti wa Mue (2013), kuhusu maudhui na matumizi ya lugha katika nyimbo za kidini za Rose Muhando ulikuwa na mchango kwa huu. Katika kazi yake, Mue alilenga kuchunguza namna ambavyo matumizi ya lugha yanavyochangia ujumbe katika nyimbo za Rose Muhando. Aidha, alilenga kuchunguza vile uteuzi wa kisarufi unavyodhihirika katika nyimbo za msanii huyo. Utafiti wake ulitumia nadharia ya maadili ili kudhihirisha uwiano kati ya ujumbe wa nyimbo za Muhando na mbinu za lugha zinazotumika. Kazi ya Mue (aliyetajwa) ililenga kubainisha kwamba, matumizi ya lugha huchangia kuibua maudhui katika nyimbo sawa na vile utafiti huu ulivyolenga kubainisha kupitia nyimbo za jando za Wakamba. Hivyo basi, uchanganuzi wake wa maudhui ulinufaisha utafiti huu hata ingawa utanzu wa nyimbo alioshughulikia wa nyimbo za kidini ni tofauti na utanzu ulioshughulikiwa na utafiti huu wa nyimbo za jando.

2.4 Tafiti Kuhusu Nyimbo za Wakamba.

Kuna watafiti ambao wametafitia utanzu wa nyimbo katika jamii ya Wakamba. Miongoni mwao ni Kimilu (1962). Kimilu alifanya utafiti kuhusu nyimbo na ngoma za Wakamba kwa kuziainisha katika makundi mawili aliyoyaita; *Mbathi sya kivalo na myali*. *Mbathi sya kivalo* ni nyimbo katika jamii ya Wakamba zilizoimbwa huku zikiandamana na ala na ngoma fulani na *myali* ni nyimbo katika jamii hii zinazoimbwa pasipo kucheza ala yoyote. Katika kazi yake, Kimilu alitenganisha nyimbo na ngoma za wanawake, wanaume, na vijana. Aidha, aliainisha majukumu mahususi ya nyimbo za *kivalo na myali*. Utafiti huu ulinufaika na majukumu ya nyimbo aliyoainisha Kimilu hata ingawa alichunguza utanzu wa nyimbo kwa jumla. Vilevile, kazi ya Kimilu (1962)

ilichunguza historia ya jamii ya Wakamba na mifumo yake ya kijamii. Sehemu hii ya kazi yake ilifaa utafiti huu katika kuelewa chanzo, mila na itikadi za jamii ya Wakamba.

Wachunguzi wengine waliopiga hatua katika utafiti wa nyimbo za jamii ya Wakamba ni Kieti na Coughlin (1990). Walishughulikia nyimbo katika makumbo mawili; *mbathi syakivalo* na *myali* wakiwa na lengo la kufafanua majukumu, muktadha na uchezaji, hadhira, ala na mapambo yanayotumiwa wakati wa uchezaji na maana yake. Aidha, walieleza athari za asasi ya dini ya kikristo na ukoloni katika nyimbo na ngoma za kiasili za Wakamba. Utafiti wa Kieti na Coughlin (waliotajwa) uliufaa huu kutokana na ufafanuzi walioshughulikia kuhusu historia ya jamii ya Wakamba na majukumu yanayotekelezwa na nyimbo na ngoma mbalimbali za Wakamba. Tofauti ya kazi yao na hii ni kwamba, walishughulikia tanzu za nyimbo tofauti na utanzu wa nyimbo za jando ulioshughulikiwa na utafiti huu. Aidha lengo lao lilikuwa kuanisha nyimbo za jamii ya Wakamba kwa makumbo tofauti na kuonyesha majukumu ya nyimbo hizo tofauti na lengo la utafiti huu ambao ulidhamiria kubainishaa kuwa, maudhui ya nyimbo za jando za Wakamba hubadilika kiwakati kulingana na mabadiliko ya kijamii.

Utafiti mwingine uliochangia huu ni wa Kilonzi (1992). Huyu alishughulikia uchezaji wa ngoma ya *kinzekatika* jamii ya Wakamba. Alichobainisha Kilonzi ni kwamba, ngoma ya *kinze* ina mtindo wake wa uchezaji, hadhira maalumu na maleba yanayoifafanua. Aidha, Kilonzi aliainisha majukumu yanayotekelezwa na ngoma ya kinze yakiwemo pamoja na kuburudisha, kuelimisha, kukashifu miongoni mwa majukumu mengine. Utafiti wake uliufaa huu kupitia majukumu ya nyimbo jadiya za jamii ya Wakamba aliyoainisha.

Vilevile, alishughulikia historia ya jamii ya Wakamba kipegele ambacho kilishughulikiwa na utafiti huu. Tofauti ya utafiti wa Kilonzi (1992) na huu ni kwamba, utanzu wa wimbo alioshughulikia ni tofauti na utanzu wa nyimbo za jando ulishughulikiwa na utafiti huu. Pia, kazi yake haikulenga kubainisha kuwa mabadiliko ya kijamii hubadilisha maudhui ya nyimbo zikiwemo za jando katika jamii ya Wakamba kama vile utafiti huu ulivyobainisha.

Akichunguza kuhusu matumizi ya taswira katikakuwasilisha ujumbe wa mwimbaji, Kieti (1999) anasema kuwa, nyimbo hutumia taswira kutoka mazingira zinamoundiwa. Anachokieleza Kieti kupitia utanzu wa ngoma ya Wakamba ijulikanayo kama *Myalini* kwamba, majina yaliyotumiwa katika baadhi ya nyimbo hizo yalikuwa na maana fiche. Kazi yake inatilia maanani umuhimu wa mazingira katika nyimbo ili maana yake iweze kueleweka. Haya yanashikiliwa na nadharia iliyoongoza utafiti huu ya Ethnografia ya mawasiliano inayosisitiza umuhimu wa mazingira katika mawasiliano. Umuhimu wa utafiti wa Kieti kwa huu ni kwamba, aliongozwa na nadharia ya Ethnografia ya mawasiliano sawa na iliyoongoza utafiti huu. Kazi ya Kieti (1999) ilichangia utafiti huu kupitia ufafanuzi wa mihimili ya nadharia ya ethnografia ya mawasiliano. Hata hivyo, kazi yake ni tofauti na hii kwani alishughulikia utanzu wa nyimbo kwa jumla. Hakujifunga katika nyimbo za jando za jamii ya Wakamba kama vile utafiti huu ulivyolenga.

Naye Wambua (2001) alitafiti kuhusu mtindo na matumizi ya lugha katika nyimbo za Kakai Kilonzo. Kupitia kazi yake, mtafiti huyu alibainisha kuwa uteuzi wa lugha katika

uwasilishaji wa ujumbe ni muhimu katika utunzi wa kazi ya fasihi. Aidha, Wambua alibainisha uhusiano kati ya uteuzi wa lugha na maudhui. Lengo moja la kazi hii lilikuwa ni kuchunguza namna ambavyo matumizi ya mbinu za sanaa hutumiwa na watunzi wa nyimbo za jando za Wakamba kuibua maudhui sawa na alivyofanya Wambua. Aidha, Kazi ya Wambua (aliyetajwa) ilichangia kazi hii kwa kuipa mwelekeo wa kuchanganua nyimbokimaudhui. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na huu kwani yeye alitafiti nyimbo za Kakai Kilonzo akilenga kubainisha matumizi ya lugha katika nyimbo hizo ili kuibua maudhui. Utafiti huu ulichunguza nyimbo za jando katika jamii ya Wakamba.

Utafiti mwingine uliokuwa na mchango kwa huu ni wa Kilauni (2007) aliyetafitia athari za usasa katika maudhui na utendakazi wa *itheke*; yaani, ngoma katika jamii ya Wakamba. Kilauni anarai kuwa, ujumbe wa ngoma ya *itheke* miongoni mwa jamii ya Wakamba hubadilika kulingana na wakati, tukio, mazingira na hadhira. Utafiti wake pia uligundua kuwa, usasa katika maudhui unajitokeza kupitia maswala ambayo hayalengi jamii ya Wakamba, bali, yanalenga jamii pana ya Kenya ama ya ulimwengu. Kulingana na Kilauni, usasa katika nyimbo ndio unaofanya nyimbo za *itheke* kutekeleza majukumu ya kijamii. Kilauni aliongozwa na nadharia ya Usasa kufikia lengo lake. Umuhimu wa utafiti wa Kilauni kwa huu ni kwamba, amefafanua chimbuko na historia ya jamii ya Wakamba iliyochunguzwa na utafiti huu. Vilevile, alibainisha maudhui ya nyimbo jadii ya zikiwemo nyimbo za jando zilizochunguzwa na utafiti huu. Tofauti na utafiti wa Kilauni, utafiti huu ulishughulikia utanzu wa nyimbo za jando za Wakamba ukiwa na lengo la kubainisha kuwa, mabadiliko ya kijamii huathiri maudhui ya nyimbo hizi kulingana na wakati.

Utafiti mwingine ulionufaisha huu ni wa Wathome (2009) unaohusu mitindo katika nyimbo za tohara za Wakamba wa Masaku ya kati. Wathome ameshughulikia sifa za kimitindo zinazodhihirika katika nyimbo za nyiso za Wakamba. Aliongozwa na nadharia ya Mtindo katika uchanganuzi wa nyimbo hizo. Wathome aligundua kuwa, mitindo iliyotumiwa katika nyiso za jamii ya Wakamba imebadilika. Kubadilika huku kunatokana na kuathiriwa kwa wanajamii kupitia dini ya kikristo. Aidha, kazi yake iligundua kuwa, nyimbo zilizokuwa zikiimbwa pamoja na miondoko yake zinaendelea kudidimia kutokana na kukengeuka kwa jamii ya Wakamba wa Masaku ya kati. Umuhimu wa utafiti wa Wathome ni kwamba, amefafanua historia ya jamii ya Wakamba iliyochunguzwa na utafiti huu. Aidha, katika matokeo ya utafiti wake, amebainisha kuwa mifumo ya kijamii kama elimu ya kisasa pamoja na dini ya kikristo imechangia kubadilika kwa mitindo ya nyiso za Wakamba. Utafiti huu ulinufaika na mifumo ya kijamii inayochangia kubadilika kwa mitindo ya nyiso aliyoinisha Wathome katika utafiti wake. Vilevile, Wathome aligusia maudhui yanayoibuliwa na nyiso za Wakamba, sehemu ambayo iliufaa utafiti huu. Tofauti ya kazi ya Wathome na hii ni kwamba, kazi yake ililenga kubainisha mabadiliko ya mitindo katika nyiso za Wakamba, ilhali utafiti huu ulilenga kuchunguza mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za jando kulingana na mabadiliko ya jamii.

Musyoka (2012) alichunguza nyimbo za mazishi miongoni mwa Wakamba. Katika kazi yake, Musyoka amechunguza mtindo wa nyimbo hizi na kueleza kwamba, nyimbo za mazishi katika jamii ya Wakamba hutumia kauli na maneno teule yanayowasilishwa kwa mahadhi maalumu, ili ziweze kutekeleza jukumu lake muhimu la kuliwaza

waathiriwa. Musyoka alilenga kubainisha kuwa, kauli za lugha zinazotumiwa katika nyimbo za mazishi za Wakamba husaidia kuibua taswira ya kimawazo kuhusu kifo. Kazi yake iliongozwa na nadharia ya mtindo na nadharia ya ethnografia ya mawasiliano. Hata ingawa Musyoka alichunguza utanzu tofauti wa nyimbo na uliotafitiwa na kazi hii, utafiti wake ulichangia huu kwa kufafanua baadhi ya mihimili ya nadharia ya ethnografia, ambayo ilizingatiwa katika kuchanganua maudhui ya nyimbo za jando za Wakamba. Vilevile, utafiti huu ulinufaika kupitia ufafanuzi aliofanya Musyoka (2012) kuhusu historia ya jamii ya Wakamba ambayo ilichunguzwa na utafiti huu.

Kutokana na udurusu wa tafiti na tahakiki mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti huu, ilibainika kuwa nyimbo za jando katika jamii ya Wakamba hazijazingatiwa kwa uketo hasa kuhusiana na mabadiliko ya maudhui kwa mujibu wa wakati. Azma ya utafiti huu ilikuwa kubainisha mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za jando za Wakamba kulingana na mabadiliko ya kijamii. Utafiti huu hivyo basi ni hifadhi ya utamaduni huu ambao una tishio la kudidimia.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Njia za Utafiti

Utafiti huu ulifanywa kwa njia tatu. Utafiti wa maktabani, utafiti katika mtandao na utafiti wa nyanjani. Utafiti wa maktabani ulitangulia utafiti wa nyanjani na utafiti katika mtandao.

3.1.1 Utafiti wa Maktabani

Utafiti huu ulifanyiwa maktabani ukiwa na kusudi la kupata maelezo ya kimsingi kuhusu masuala ya kinadharia na tafiti kuhusu nyimbo zikiwemo za jando. Maeneo haya yalimwezesha mtafiti kupata yaliyoandikwa kuhusu mada pamoja na data iliyohitajika kufanikisha utafiti. Mtafiti alitumia maktaba za kitaifa za Nairobi na Machakos. Aidha, alitumia maktaba za Vyuho Vikuu vya Mount Kenya, Nairobi, Moi, Egerton, na Kenyatta. Ili kupata maelezo ya kimsingi kuhusu jamii ya Wakamba kwa mfano utamaduni, mila na itikadi zao, historia yao, nyimbo zao jadii zikiwemo za jando miongoni mwa mengine, mtafiti alizingatia maandishi mbalimbali kwenye maktaba.

Vilevile, mtafiti alisoma tafiti mbalimbali kuhusiana na mada ya utafiti. Kwa njia hii, mtafiti aliweza kupata mwelekeo na msingi imara wa kinadharia ambao ulimwezesha kuchanganua kazi hii. Aidha, mbinu za kukusanya na kuchanganua data zilitiliwa maanani wakati wa kufanya utafiti maktabani. Mtafiti alifaidika na data iliyoandikwa kwenye vitabu, majarida, magazeti, ripoti za serikali, makala za semina, tasnifu za

Uzamili na Uzamifu, ramani na makala yoyote yale yanayohusiana na mada ya utafiti. Pia, utafiti ulifanywa katika makavazi ya Machakos na ya kitaifa jijini Nairobi ambapo, kulipatikana hati na nyaraka zinazohusu utamaduni wa Wakamba.

3.1.2 Utafiti katika Mtandao

Kwa sababu ya maendeleo na kuimarika kwa teknolojia ya habari na mawasiliano, utafiti huu ulifaidika kutokana na tovuti, wavuti na nyavuti mbalimbali. Mtafiti alitumia tovuti mbalimbali ili kupata data kuhusu usuli wa jamii ya Wakamba pamoja na fasihi simulizi yao. Aidha, data kuhusu nadharia zilizoongoza utafiti ilipatikana mtandaoni. Vilevile, kupitia tovuti, wavuti na nyavuti mbalimbali, mtafiti aliweza kuchunguza tasnifu za Uzamili na Uzamifu zinazohusiana na mada ya utafiti kutoka vyo vikiu mbalimbali. Aidha, baadhi ya masuala kuhusiana na chanzo na historia ya jamii ya Wakamba yalipatikana kupitia tovuti mbalimbali.

3.1.3 Utafiti wa Nyanjani

Utafiti wa nyanjani ulizingatiwa ili kupata data ya kimsingi kuhusu nyimbo za jando za Wakamba kupitia vipindi mbalimbali vya kihistoria. Ili kutekeleza shughuli hiyo, mtafiti alizuru kata za Nzyiitu, Kalimbui, Ngalange, Mwangea, Nzanzeni na Kaluilaakatika Kaunti ndogo ya Tseikuru, Kaunti ya Kitui. Vituo vya utafiti viliteuliwa kwa njia ya makusudi kwa sababu vina ithibati ya wasanii ambao hutunga nyimbo za jando. Utafiti wa nyanjani ulihusu kunakili majibu yaliyotakana na usaili wa ana kwa ana katika daftari,

kurekodi nyimbo kupitia utendaji wake halisi katika kinasa sauti, kupiga picha kwa kutumia kamera pamoja na kuchukua video ili kunasa vipengele muhimu vya utendaji.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyiwa kaunti ya Kitui, kaunti ndogo ya Tseikuru na kata za Nzyiitu, Kalimbui, Ngalange, Mwangea, Nzazeni na Kaluila. Eneo hili lilituliwa kama mojawapo ya vitovu vya utamaduni ambavyo havijaathiriwa na maendeleo ya miji na utamaduni wa kigeni kwa kiwango kikubwa. Hii ni kutokana na sababu kwamba, sehemu hii imo sehemu za mashambani na hivyo ni dhahiri kuwa haina athari kubwa ya mila za jamii nyingine ikilinganishwa na sehemu zingine kama Machakos ambayo inapakana na mji wa Nairobi.

3.3 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti huu walikuwa masogora wa nyimbo za jando, wazee ambao walikuwa viongozi wa sherehe za jando waliojulikana kama *nzavili*(*taz. Kiambatisho* cha 1), ngariba, wasaidizi wake pamoja na vikundi vya kijamii.

3.4 Sampuli lengwa na Mbinu za Uteuzi wa Sampuli

Utafiti huu ulitumia sampuli ya kimakusudi. Uteuzi sampuli kimakusudi uliegemezwa kwa kile kinachomuongoza mtafiti, yaani sababu fulani maalumu za kitafiti na kiuchunguzi alizonazo. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999), uteuzi sampuli

kimakusudihumruhusu mtafiti kuteua eneo na wahojiwa ambao wana habari muhimu kuhusu suala la utafiti. Katika utafiti huu, mtafiti aliteua wahojiwa ishirini na saba (27) ambao ni wenye ujuzi kuhusu mila ya tohara na nyimbo za jando katika jamii ya Wakamba. Wahojiwa hao ni wazee wa *kisuka* na *kivalo* (taz. Kiambatisho 1), masogora, ngariba nawasaidizi wake.

Jamii ya Wakamba ni pana na imejumuisha watu waishio kaunti za Kitui, Makueni, na Machakos. Hata ingawa jamii hii ni pana, utafiti huu ulitumia utafiti elekezi ili kuteuasehemu ya utafiti pamojana wasailiwa ambao walitumiwa katika utafiti. Utafiti elekezi humruhusu mtafiti kuteua eneo au wahojiwa ambao wana habari muhimu kuhusu suala la utafiti (Mugenda na Mugenda, 2003). Kaunti ya Kitui, Kaunti ndogo ya Tseikuru na kata za Nzyiitu, Kalimbui, Mwangea, Ngalange, Nzanzeni na Kaluilaa ndiko mpaka kufikia sasa kunapatikana masogora ambao wanashiriki jando hizi. Vilevile, ni eneo ambalo wakaaji wake wangali wanashikilia utamaduni wa kiasili na lina historia ya asili ya utamaduni huu.

Kata hizi zimewakilisha Tseikuru yote kwa vile tamaduni za watu wa kata teule za utafiti ni sawa na tamaduni zinazopatikana katika eneo zima la Tseikuru. Gwiji aliyejulikana alimwelekeza mtafiti kwa gwiji mwingine mpaka data iliyotakikana ikapatikana. Kupitia mbinu elekezi, magwiji ambao walionyesha ujuzi kuhusu mila ya jando katika jamii ya Wakamba na nyimbo za jando zinazofungamana na sherehe hii walihusishwa katika utafiti. Wahojiwa waliteuliwa kimakusudi kwa kutumia vigezo vifuatavyo:

- a) Ngariba ambaye alifanya kazi ya kutahiri kwa zaidi ya miaka kumi katika kaunti ndogo ya Tseikuru pamoja na wasaidizi wake wawili.
- b) Masogora ambao ni magwiji maarufu wa nyimbo za jando na weledi wa fasihi simulizi, mila na desturi za Wakamba, na ambao wameongoza na kutunga nyimbo hizi kwa muda usiopungua miaka kumi.
- c) Wazee wa *kivalo* na *kisuka* (taz. Kiambatisho 1.) ambao wana umri wa kati ya miaka 60-70. Wazee hawa huwepo katika sherehe za jando kutokana na welewa wao wa mila za jando katika jamii hii.

Kupitia usaidizi wa chifu na naibu wake, mtafiti kwa kutumia mbinu elekezi aliweza kuwatambua na kuwateua wahojiwa walioshiriki katika utafiti huu. Wahojiwa hao walikuwa wazee wawili kutoka kila kata, masongora wawilikutoka kila kata, ngariba mmoja na wasaidizi wake wawili jumla wasailiwa ishirini na saba (27). Mbinu elekezi ilisadifu katika kuwateua wasailiwa kupitia vigezo vilivyoonyeshwa hapo juu.

3.5 Vifaa Vya Utafiti

Mulokozi (2003) alisisitiza umuhimu wa kutumia vifaa mbalimbali katika utafiti. Katika ukusanyaji data, utafiti huu ulitumia vifaa mbalimbali mathalan kalamu, karatasi na rununu. Utafiti ulitumia kalamu na karatasi katika kuandika data mbalimbali zilizopatikana katika utafiti. Aidha, kalamu na karatasi ilitumika katika kuandika nyimbo za jando za Wakamba kwa lugha ya Kikamba na baadaye kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Simu ya rununu ilitumika ili kunasa nyimbo za jando za kipindi cha kabla ya

ukoloni zilizoimbwa na masogora na wazee teule wa *kivalo* na *kisuka*. Vilevile, rununu ilitumika kupiga picha tuli matukio wakati wa sherehe ya jando na pia kuchukua video wakati wa utendaji wa nyimbo za jando katika miktadha yake halisi.

3.6 Ukubalifu na Utegemeo wa Vifaa vya Utafiti

Utafiti huu ulitumia vifaa mbalimbali katika ukusanyaji wa data. Kabla ya utafiti wenyewe, mtafiti alifanyia vifaa vya utafiti majaribio ili kuhakiki uhalali na utegemeo. Umuhimu wa kuzingatia uhalali na utegemeo wa vifaa vya utafiti umesisitiwa na Mulokozi (2003) na Mugenda na Mugenda (2003). Vifaa hivi nikalamu, karatasi na simu ya rununu iliyotumikakunasa sauti, kuchukua picha tuli na video wakati wa utendaji. Kata zilizochaguliwa kujaribia vifaa vya utafiti ni Kaluila, Kalimbui na Ngalange kupitia utafiti elekezi. Vifaa vya utafiti vilifanyiwa majaribio mwezi Agosti 2012 na Desemba 2012. Kila kifaa kiliufaa utafiti kama ifuatavyo:

3.6.1 Kalamu na Karatasi

Utafiti huu ulitumia kalamu na karatasi katika kuandika data mbalimbali zilizohusiana na mada ya utafiti hususan, nyimbo za kipindi cha kabla ya ukoloni zilizoimbwa na wasailiwa lengwa. Aidha, mielekeo, maoni na falsafa za watafitiwa kuhusiana na mada ya utafiti zilinakiliwa kupitia kalamu na karatasi. Baadaye, data iliyokusanywa na kuandikwa ilichanganuliwa kwa kutumia lengo na madhumuni ya utafiti. Vifaa hivi viliufaa utafiti kwa sababu ni vyepesi na hubebwa kwa urahisi na pia havihitaji utaalamu kuvihifadhi.

3.6.2 Rununu

Rununu ni kifaa cha mawasiliano ambacho hutumika pia katika ukusanyaji data wakati wa utafiti (Kothari, 2004). Ina uwezo wa kunasa sauti, kupiga picha tuli za wahusika na mandhari ya utendaji na pia kuchukua video. Rununu ilitumika katika utafiti huu kurekodi nyimbo za jando za kipindi cha kabla ya ukoloni zilizoimbwa na wasailiwa. Aidha, ilitumiwa kuchukua picha tuli katika muktadha halisi wa utendaji (taz. kiambatisho 10-19). Vilevile, ilitumika kuchukua video ya matukio wakati wa sherehe ya jando (taz. kiambatisho 20). Pia, ilitumiwa kurekodi kauli na maoni waliyotoa watafitiwa kuhusiana na mada ya utafiti. Kifaa hiki kiliufaa utafiti kwa sababu mtafiti aliweza kusikiliza nyimbo zilizorekodiwa mara nyingi iwezekanavyo kabla ya uchanganuzi wa data. Vilevile, kifaa hiki kilimpunguzia mtafiti kazi ya kuandikaandika wakati wa uimbaji wa nyimbo za jando. Rununu pia ni nyepesi, hubebwa kwa urahisi na haihitaji utaalumu wa kuihifadhi ikilinganisha na vifaa vingine kama kamera na utepe wa video.

3.7 Mbinu za Ukusanyaji Data

Katika ukusanyaji data, utafiti huu ulitumia mbinu mahususi mathalan mwongozo wa hojaji, mahojiano na uchunguzi shiriki. Kulingana na Mugenda na Mugenda(2003) na Kothari (2004), matumizi ya mbinu mbalimbali za utafiti ni muhimu ili kupata matokeo yenye kutegemewa. Nyimbo katika kipindi cha kabla ya ukoloni zilipatikana kupitia mbinu ya mwongozo wa hojaji na mahojiano ya ana kwa ana na wasailiwa. Kwa kuwa wengi wa wahojiwa hawajui kusoma na kuandika, mbinu hii ya usaili wa ana kwa ana

ilisadifu. Wahojiwa waliombwa kuimba nyimbo za jando za kabla ya ukoloni ili kutathmini maswali, lengo na madhumuni ya utafiti kwa kutegemea mihimili ya nadharia zilizoongoza utafiti. Wahojiwa walioshirikishwa katika uimbaji wa nyimbo za jando za kipindi cha kwanza cha utafiti ni wazee waliokuwa na umri wa miaka 60-70, ngariba na masongora ambao walikuwa wamehudhuria sherehe za jando kwa zaidi ya miaka kumi (taz. 3.4). Mwongozo wa hojaji ulitumiwa kuwaongoza wahojiwa kueleza iwapo walishuhudia kipindi cha kabla ya ukoloni. Mbinu ya kutumia mwongozo wa hojaji ni muhimu katika utafiti kwa sababu inampatia mhojiwa uhuru wa kujibu maswali kulingana na maoni yake. Aidha, huwaruhusu wahojiwa kueleza misukumo na sababu za mienendo yao (Kothari, 2004). Pia, huweza kuibua maswala mengi katika muda mfupi. Vilevile, mbinu ya uchunguzi shiriki ilitumika katika utafiti huu wakati wa utendaji wa nyimbo za jando katika muktadha wake halisi.

Uchunzaji shiriki huweza kukumbwa na kwelikinza ya mchunzaji; hivyo, kuathiri uhalisi wa data (Kothari, 2004; Kobia, 2008). Ili kukabiliana na kwelikinza hii, mtafiti na wasaidizi wake walitangamana na watafitiwa katika uimbaji na utendaji wa nyimbo za jando ili kuondoa dhana ya kwamba wanatafitiwa. Hali hii ilimuweka mtafiti katika mazingira na miktadha halisi ambapo nyimbo za jando huimbwa na hadhira ya nyimbo hizo. Njia hii ya kujumuika na kushiriki katika utendaji wa shughuli ya kijamii imependekezwa na watafiti kama Foley (1995) na Mugenda na Mugenda (2003).

3.8 Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa ilirekodiwa na kuhifadhiwa katika kanda za kinasa sauti na katika utepe wa video. Vilevile, ilinakiliwa katika daftari. Data iliyorekodiwa kwenye kinasa sauti ilinukuliwa moja kwa moja kupitia njia ya usikilizaji. Nyimbo ziliandikwa kwa lugha ya Kikamba na baadaye kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Kwa kuwa utafiti huu ulikusanya nyimbo za jando nyingi (taz. Kiambatisho 2), ilimbidi mtafiti kuzichuja na kuteua nyimbo za jando thelathini (30) zilizolenga mada ya utafiti. Nyimbo zilizochaguliwa zilionesha mabadiliko ya maudhui kulingana na mapisi. Hatimaye, nyimbo za jando zilihakikiwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti, maswali, nadharia na mipaka ya utafiti. Matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya ufafanuzi wa kimaelezo.

3.9 Maadili ya Utafiti

Ukusanyaji data kupitia mbinu yoyote ya utafiti huhitaji kuzingatia maadili kwa upande wa watafitiwa, mtafiti na katika mchakato wa utafiti (Mulokozi, 2003; Kothari, 2004; Kobia, 2008). Utafiti huu ulizingatia maadili kama ifuatavyo:

3.9.1 Maadili ya Utafiti yanayohusu Mtafiti

Mtafiti aliandika barua ya kujitambulisha na kuomba kibali cha kukusanya data kutoka kwa Halmashauri ya kitaifa ya Sayansi na Teknolojia ubunaji na kupata barua iliyomruhusu kukusanya data katika sehemu teule ya utafiti (taz. Kiambatisho 21). Kabla ya utafiti, mtafiti aliwasiliana na kujitambulisha kwa chifu bwana Titus Mutui na naibu

wake Annah Kilonzo kutoka sehemu ya utafiti ambao walimpa ruhusa ya kukusanya data. Vilevile, kupitia utafiti elekezi, mtafiti aliwatembelea walengwa wake hususan masogora wa nyimbo za jando, wazee teule katika kata za Nzyiitu, Kalimbui, Mwangea, Nzanzeni, Ngalange na Kaluila na kuwaeleza sababu ya kutaka kukutana nao. Aliwaeleza kwamba, alitafuta kibali cha kukusanya nyimbo za jando za Wakamba akiwa na nia ya kuzihifadhi nyimbo hizo katika maandishi. Pia aliwaeleza kwamba, nyimbo za jando za Wakamba zinaendelea kudidimia na kusahaulika hivyo basi, kuzitafitia kutachangia katika kuhifadhi utamaduni wa Wakamba kwa manufaa ya vizazi vijavyo. Zaidi ya maelezo hayo, mtafiti alizingatia maadili ya utafiti kwa kutowalazimisha wasailiwa kuimba nyimbo wala kuwakatiza wakati wa uimbaji au wakati wa kujibu maswali wakati wa mahojiano. Vilevile, mtafiti alijenga ukuruba na watafitiwa kwa kutangamana nao wakati wa uimbaji na utendaji wa nyimbo za jando.

3.9.2 Maadili ya Utafiti yanayohusu Watafitiwa

Mtafiti alijitambulisha kwa watafitiwa kwa kuwaonyesha kitambulisho chake cha kitaifa, na pia kwa kuwaonyesha barua kutoka Halmashauri ya Sayansi na ubunaji iliyompa kibali cha kufanya utafiti katika kaunti ya Kitui, kata ndogo ya Tseikuru. Vilevile, aliwaeleza sababu za kukusanya na kuhifadhi nyimbo za jando za Wakamba. Aliwaeleza kwamba, nyimbo jadiya za Wakamba zikiwemo za jando zinaendelea kudidimia na kusahaulika katika jamii na hivyo, pana umuhimu wa kuzitafiti, kuzikusanya na kuzihifadhi ili ziweze kutumiwa na vizazi vijavyo. Mtafiti aliwaomba masogora na wazee

teule waimbe nyimbo za jando zilizoimbwa kabla ya ukoloni huku akizinasua kupitia kwa rununu. Mtafiti hakuwalazimisha watafitiwa kushiriki katika uimbaji wa nyimbo.

3.9.3 Maadili ya Utafiti yanayohusu Mchakato wa Utafiti

Utafiti huu ulizingatia maadili ya utafiti kupitia kunukuu za kazi za kitaaluma zinazohusiana na mada ya utafiti. Vilevile, utafiti huu uliweka wazi matokeo ya utafiti na kupendekeza sehemu ambazo zinaweza kufanyiwa utafiti wa baadaye kuhusiana na mada ya utafiti. Aidha, mtafiti aliweza kujenga ukuruba na wanajamii wa sehemu ya utafiti kwa kujumuika nao wakati wa sherehe ya jando pasipo kuwaonyesha kwamba anawatafiti. Lugha ya Kikamba ilitumika nyanjani wakati wa ukusanyaji data.

SURA YA NNE

UCHANGANUZI WA MAUDHUI YA NYIMBO ZA JANDO ZA WAKAMBA KATIKA KIPINDI CHA KABLA NA BAADA YA UKOLONI

4.0 Utangulizi

Lengo kuu la sura hiini kuchanganua maudhui katika nyimbo za jando za jamii ya Wakamba katika kipindi cha kabla ya ukoloni, hadi kipindi cha baada ya ukoloni ili kubainisha kuwa, maudhui haya yamekuwa yakibadilika kulingana na mabadiliko ya kijamii. Vilevile, sura hii imebainisha mbinu za kisanaa zinazotumika na watunzi wa nyimbo za jando katika jamii ya Wakamba ili kubadilisha maudhui kulingana na wakati.

4.1 Maudhui ya Nyimbo za Jando za Wakamba katika Kipindi cha Kabla ya Ukoloni.

Katika sehemu hii, mtafiti amechanganua nyimbo kumi na tano zilizoimbwa katika kipindi cha kabla ya ukoloni kwa kuzingatia maudhui yake. Nyimbo katika kipindi hiki zinasheheni maudhui yaliyoibuka kutokana na hali ya jamii na wakati wake. Uchanganuzi huu umefanywa kwa mujibu wa nadharia ya Uhalisia, Uamali na Ethnografia ya mawasiliano. Vipengele vya nadharia hizi vilivyoongoza uchanganuzi wa nyimbo za jando za Wakamba ni pamoja na uhalisia wa maisha, matumizi ya lugha kulingana na muktadha, utamaduni na mazingira mbalimbali katika jamii. Ili kuainisha lugha na matumizi yake, kipengele cha muktadha kimetumiwa ili kuchunguza vile mawasiliano yanayotumia lugha yanavyoendeshwa, na vile mawasiliano haya

yanavyoibua mchakato mzima wa mawasiliano kupitia kwa maudhui. Ifuatayo ni mifano ya maudhui katika nyimbo za jando za Wakamba katika kipindi cha kabla ya ukoloni.

4.1.1 Umuhimu wa Tohara

Jamii ya Wakamba ilitilia mkazo tohara kwani ilikuwa kama kivuko kwa wavulana kutoka maisha ya utotoni hadi utu uzima. Kupitia tohara, wavulana walipata mafunzo ambayo hayangepitishwa katika muktadha mwingine hususan mafunzo kuhusu unyumba, majukumu ya kiuana, siri na historia ya jamii miongoni mwa mafunzo mengine. Aidha, baada ya tohara watahiriwa walichukuliwa kama wanajamii kamili na waliruhusiwa kurithi mali. Umuhimu wa tohara katika jamii ya Wakamba unatiliwa uzito na wimbo wa *Nitilwe mindo* (Nikatwe kitu, Na.9) kupitia mishororo ifuatayo:

<i>Ninitilwe mindo</i>	Nikatwe kitu
<i>Ninitilwe oyu</i>	Nikatwe sasa
<i>Mundu utemutile mindo</i>	Mtu ambaye hajakatwa kitu
<i>Ti mundu</i>	Si mtu
<i>Nithi ngasunge mbui sya na u</i>	Niende nikatunze mbuzi wa baba
<i>Muvea ute mundu mwaike ti muvea</i>	Aila ambayo haina mtu ametahiriwa si aila

Wimbo huu unasheheni maudhui ya umuhimu uliopewa tohara katika jamii ya Wakamba. Shughuli hii ilichukuliwa kama ngazi muhimu katika ukuaji wa mwanajamii kutoka utotoni na kuingia utu uzima na ilitumiwa kama tambiko la upisho kwa watahiriwa. Wimbo huu unaonyesha majukumu ambayo yaliandamana na tohara. Mtahiriwa anasema *nitilwe mindo, nitilwe oyu* (nikatwe kitu, nikatwe sasa) katika mshororo wa 1 na wa 2 kuonyesha hamu yake kubwa ya kutahiriwa. Katika mshororo wa 5 anasema *nithi ngasunge mbui sya nau* (niende nikatunze mbuzi wa baba) kumaanisha kurithi mali

ya babake. Mshororo wa 6 unasema *Muvea ute mundu mwaike ti muvea* (Aila ambayo haina mtu aliyetahiriwa si aila). Mshororo huu unaonyesha umuhimu ambao ulipewa tohara kama kivuko muhimu katika maisha ya kila mwanajamii.

Kupitia wimbo huu, ni muhimu kuelewa maana ya neno ‘mtu’ na ‘si mtu’. Kwa mujibu wa jamii ya Wakamba, mtu ni yule aliyefanyiwa tohara zote. Ni mwanajamii ambaye ametahiriwa na kupewa majukumu anayostahili kulingana na mila na desturi za jamii. ‘Si mtu’ ni yule ambaye hajapashwa tohara. Mtu kama huyu hata awe ni mzee bado alichukuliwa kama ‘mtoto’(kivisi) na hakuruhusiwa kutangamana na wazee wengine katika hafla yoyote ya kijamii. Alidharauliwa na jamii haingemruhusu hata kuo. Kutokana na itikadi hii, vijana waliohitimu umri wa kutiwa jandoni walijitangaza kupitia kwa wazazi wao kwamba, wanataka kutahiriwa ili wavuke kutoka ngazi ya utotoni hadi utu uzima.

Aidha, matumizi ya msembo ‘kutunza mbuzi wa baba’ yametumiwa kulinganisha kutunza mbuzi na kurithi mali. Katika jamii ya Wakamba, mwanamume hangepata urithi wowote kabla ya kupitia jando ndogo, kubwa na ya kucheza. Sherehe hii ilikuwa kama ishara ya kuhitimu kutoka hadhi moja hadi nyingine. Vilevile, neno *mindu*(kitu) ikiwa na maana ya mboo litaeleweka na jamii na hadhira katika muktadha wa jando. Msanii anatomia mbinu ya tasfida yenye adabu na heshima badala ya kutaja sehemu hii nyeti kwa uwazi. Ni hadhira pekee katika jamii mahususi ya Wakamba ambayo inaweza kung’amua maana ya neno hili katika muktadha wa jando. Vipengele vya muktadha,

hadhira lengwa na utamaduni ni vya kimsingi mno katika kuelewa maana ya maneno kama yalivyotumiwa katika kazi ya sanaa (Hymes, 1974).

Kuelewa utamaduni wa Wakamba ni muhimu ili kuelewa maana ya maneno yanayotumiwa katika muktadha na mazingira ya jando. Katika jamii ya Wakamba, mwanamume pekee ndiye kiongozi wa familia na ndiye mmiliki wa mali. Urithi wa mashamba na mifugo ulipitishwa kwa vijana wa kiume kutoka kwa baba yao. Hili lilifanyika baada ya mvulana kutiwa jandoni ambapo iliaminika kuwa, amekomaa na ana uwezo wa kutunza mali ya babake. Huu ulikuwa uhalisi wa maisha katika jamii ya Wakamba. Uhalisi wa kurithisha wavulana lakini si wasichana. Mwelekeo huu unadhihirisha uhalisi wa maisha ya Wakamba wakati wa kabla ya ukoloni, na unaweza kuchanganuliwa katika misingi ya nadharia ya Uhalisia iliyoongoza utafiti huu. Kwa mujibu wa nadharia hii, maswala ya kijamii kama nyimbo huonyesha uhalisi wa maisha katika kipindi husika.

Wimbo mwingine ambao ulitungwa kuonyesha umuhimu wa tohara ni wimbo wa *Mwasa na ngomo* (Anayechonga na kishoka, Na. 10) kupitia mishororo ifuatayo;

<i>Mwasa na ngomo ii</i>	Unayechonga
<i>Wiasa ki?</i>	Unachonga nini?
<i>Utuku twambiliilye kwitya</i>	Usiku tulianza komba
<i>Ta tukwinzia</i>	Kama tunaichimbia

Wimbo huu unamulika hamu ya watahiriwa ya kupitia tambiko hili muhimu la kijamii. Hamu yao inasawiriwa kupitia swali la balagha wanalouliza ngariba kupitia mshororo wa 1 na wa 2 *Mwasana ngomo wiasa ki?* (unayechonga unachonga nini?). Swali hili la

balagha linaloulizwa ngariba lina lengo la kumuhimiza afanye kazi yake hima. Kupitia mshororo wa 3 na wa 4 usemao *utuku twambiliilye kwityata tukwinzia* (usiku tuanze kuomba kama tunachimbia), watahiriwa wanaonyesha hamu ya kutahiriwa ili wapate kibali cha kutongoza wanawake.

Neno 'kuchimbia' linaibua maana kuwa, haikuwa rahisi kumshawishi mwanamke kushiriki ngono; kwa hivyo, mtahiriwa alihitajika kujitahidi 'kuomba', ikiwa na maana ya kusihhi. Maneno 'kuchimbia' na 'kuomba' yataeleweka kulingana na tukio, hadhira, utamaduni na muktadha wa wimbo huu. Vilevile, maneno *kwasa*(kuchonga) na *kung'ela* (kukata mara moja) yana maana tofauti na yataeleweka tu na hadhira kupitia kuelewa utamaduni wa jamii ya Wakamba na muktadha wa jando. Jamii ya Wakamba ina utamaduni wa uchongaji. Kabla ya majilio ya wakoloni, Wakamba walifanya biashara na jirani zao hususan Wameru, Waembu, Wagikuyu, na Waarabu. Miongoni mwa bidhaa walizobadilishana nafaka nazo ni vinyago vya kuchongwa. Istilahi 'kukata' na 'kuchonga' zimetumika kulingana na utamaduni wa uchongaji katika jamii hii. Kukata huwa ni mara moja hasa kwa kifaa chenye makali ilhali, kuchonga huchukua muda. Katika muktadha wa tohara, kukata mara moja hakuna uchungu mwingi kama kuchonga polepole.

Matumizi haya ya maneno kulingana na utamaduni na muktadha yanaungwa mkono na Saville- Trioke (1982) anaposhadidia kuwa, ili kuelewa aina ya ujumbe unaokusudiwa, ni lazima tuelewe utamaduni unaofuatwa na wanajamii. Uwezo wa kutumia maneno kulingana na muktadha ili kufanikisha mawasiliano unaafikiana na nadharia ya

Ethnografia ya mawasiliano iliyoelekeza utafiti huu. Kwa mujibu wa nadharia hii, matumizi ya maneno kulingana na muktadha huchukuliwa kama kigezo cha ndani cha ubora wa kazi ya kifasihi. Uwiano wa muktadha na matumizi ya maneno yanayoibuliwa na nyimbo za jando za jamii ya Wakamba ndio unaumba maudhui yenye utendakazi muhimu kwa jamii hii.

4.1.2 Kupongeza Ujasiri

Ujasiri na ukakamavu ni sifa iliyosisitizwa katika nyimbo za jando za jamii ya Wakamba. Watahiriwa walitarajiwa kuonyesha ujasiri wakati wa 'kukatwa'. Hawakutarajiwa kuonyesha dalili zozote za kuogopa kisu cha ngariba. Sifa ya ujasiri ilipelekea mtahiriwa kusifiwa baada ya tohara na kufananishwa na babake. Mtahiriwa aliyeonyesha dalili za woga alikejeliwa na kufananishwa na mamake. Ili kuchelea kashfa na kejeli, watahiriwa walionyesha ujasiri wakati wa tohara kwa kuimba wimbo wa *Muti mumu* (Mti uliokauka, Na. 4) kama vile sehemu ifuatayo ya wimbo huu inavyoshadidia:

Mwaikwa: Kwa sisya wone

Mwaiki: Muti uu ni mumu

Mwaiki: Umite nza na nthini no mwiu

Mwaiki: Ninguutila

Mwaikwa: Tila

Mtahiriwa: Angalia uone

Ngariba: Mti huu umekauka

Ngariba: Umekauka nje lakini ndani haujakauka

Ngariba: Nitaukata

Mtahiriwa: Kata

Ngariba anamtisha mtahiriwa kwa kumwambia kwamba 'mti' umekauka katika mshororo wa 2, naye mtahiriwa anamtia shime aukate. Mtahiriwa anaonyesha ujasiri na ukakamavu kwa kumwambia ngariba 'kata' katika mshororo wa 5 licha ya kwamba, mti umekauka na haitakuwa rahisi kuukata. Ukavu wa 'mti' katika muktadha wa wimbo huu unaashiria ugumu ambao utakuwepo wakati wa kukata govi la mtahiriwa. Katika wimbo

huu, lugha ya kitamathali imetumika kulingana na mazingira ili kuibua maudhui ya ukakamavu. Mbinu ya sitiari imetumika katika kufananisha govi la mtahiriwa na mti mkavu. Katika mazingira ya Ukambani hasa sehemu ya utafiti, ukosefu wa mvua mara kwa mara husababisha ukavu wa mimea. Kutokana na ukavu huu, baadhi ya miti huwa imekauka. Watahiriwa na wanajamii wanaoishi katika mazingira haya wana welewa kuwa, kukata mti uliokauka huchukua mda kuliko mti ambao hujakauka. Kwa kuambiwa na ngariba kuwa mti ni mkavu lakini ataukata, watahiriwa wanatarajishwa kuwakitendo hicho hakitakuwa rahisi na lazima wastahimili uchungu wakati huo wote. Watahiriwa kupitia wimbo huu wanafahamishwa kwamba, ni lazima waonyeshe ujasiri na uvumilivu wakati wa kutahiriwa.

Lugha iliyotumiwa katika wimbo huu pia ni ya kimapumbo. Inaeleweka na hadhira lengwa na wanajamii husika pekee. Kwa mfano, wanaotarajiwa kutahiriwa wanamwambia ngariba *kwa sisyawone* (angalia uone) katika mshororo wa 1, naye ngariba anaelewa anachoambiwa aangalie, yaani mboo. Ngariba pia anatumia mafumbo anapojibu *muti uu ni mumu, umite nza na nthini no mwiu* (mti umekauka nje, lakini ndani haujakauka) mshororo wa 2. Maana yake ni sehemu hiyo ya siri imekauka nje, lakini ndani ina mbegu za uzazi; yaani, ina manii. Wavulana katika jamii ya Wakamba kabla ya majilio ya wakoloni walikuwa wakitahiriwa wakiwa na umri mkubwa. Kwa mujibu wa King'ei (1982), wavulana walikuwa wakitahiriwa wakiwa na zaidi ya miaka kumi na mitano. Hii ni kwa sababu walitarajiwa kutwikwa majukumu ya utu uzima baada ya tohara. Kutokana na uhalisi huu, ngariba analinganisha mboo za watahiriwa na mti uliokomaa na kukauka. Tamathali ya sitiari imetumika katika wimbo huu ili kuibua

maudhui ya ujasiri. Katika ubeti wa mwisho, mishororo ifuatayo inatumiwa na ngariba kuwahimiza watahiriwa wasiogopekutahiriwa. Anasema:

<i>Ekai ukia</i>	Wacheni kuogopa
<i>Ta matila ma kiimani,</i>	Kama wajinga wa milimani
<i>Matesi mbilano</i>	Wasiojua kazi

Ngariba anawafananisha wanaoogopa na wajinga wa milimani ambao hawajui ‘kazi’ yaani, ngono. Wajinga wa milimani kwa mujibu wa wimbo huu ni Wakikuyu kwa sababu wanaishi sehemu zenye milima kinyume na Wakamba wanaoishi sehemu tambarare. Katikamuktadha wa utamaduni waWakamba, watu wa milimani yaani Wakikuyu wanachukuliwa kuwa wavivu,na ambao hawajiwezi kimapenzi (Wathome, 2009). Watahiriwa kwa kuchelea kufananishwa na ‘wajinga kutoka milimani’ wanajikaza na kutoonyesha dalili zozote za woga.

Mbinu ya tashbihi imetumiwa na ngariba katika kuwafananisha watakaonyesha dalili za woga na ‘wajinga wa milimani’. Mbinu ya tashbihi inatumiwa ili kuchochea ujasiri kwa watahiriwa. Huu ulikuwa uhalisi wa maisha wakati wa tohara kabla ya majilio ya wakoloni. Tabia ya ujasiri ilitiliwa mkazo na jamii ya Wakamba kwani, watahiriwa walitarajiwa kuwa ‘nthele’ (taz. kiambatisho, 1) baada ya tohara ambao walitegemewa na jamii kuilinda kutokana na uvamizi wowote kutoka kwa maadui zao.

Akiandika kuhusu umuhimu wa kuzingatia muktadha katika Ethnografia ya mawasiliano, Hymes(1974) anasema ni muhimu kuzingatia muktadha ili kuelewa maana ya maneno yanayotumiwa kimapenzi katika usemi.Maoni ya Hymes yanalandana na maoni ya Mohamed (1995) anaposema kuwa, lugha ya kitamathali inayotumiwa katika jamii

huchota maudhui kutoka kwa mazingira ambapo wazungumzaji wa lugha husika huishi. Tamathali ya sitiari inayobainika katika wimbo huu inatokana na mazingira ya jamii ya Wakamba ya ukavu.

Wimbo mwingine ambao unaashiria maudhui ya ujasiri ni wimbo wa *Tila mukoko* (Kata mukoko, Na. 12) kupitia mishororo ifuatayo:

<i>Tila mukoko ii</i>	Kata mukoko ii
<i>Niw'o twinuke</i>	Ndio twende nyumbani
<i>Ng'ela mwa kung'ela</i>	Kata kwa haraka tafadhali
<i>Ng'ela twinuke</i>	Kata twende nyumbani

Ngariba alikuwa akihimizwa afanye kazi yake harakaharaka ili watahiriwa wafumukane waende makwao. Wimbo huu uliimbwa na mutribu huku mtahiriwa akiwa ameangalia mbele bila kusonga wala kupepesa macho. Katika lugha ya Kikamba, *mukokoni* aina ya mti mgumu ambao huwa si rahisi kuukata na ni mweusi kwa rangi. Katika muktadha na mazingira ya jando, *mukokounaashiria* sehemu ya siri ya mtahiriwa inayokatwa wakati wa tohara. Kwa kumwambia ngariba *Ng'ela mwa kung'ela* (Kata kwa haraka) katika mishororo wa 3 ina maana kuwa, mtahiriwa ana ujasiri wa kuhimili uchungu wa kisu cha ngariba. Hata ingawa mboo yake inafananishwa na mti wa *mukoko*, ambao huchukua mda kukatwa kutokana na ugumu wake, anahimiza ngariba aukate haraka. Taswira ya ngariba aking'ang'ana kukata govi ya mtahiriwa ambayo imekauka inaibua maudhui ya ujasiri wa mtahiriwa.

Wimbo mwingine ulioimbwa kuonyesha umuhimu wa ujasiri kwa watahiriwa ni wimbo wa *Eka utelema*, (Wacha kutetemeka Na. 6) kupitia mishororo ifuatayo:

<i>Witelemwa ni kyau na mwenyu no ukwene</i>	Unaogopa nini na mamako anakuona
<i>Witelemwa ni kyau na mwivawa no ukwene</i>	Unaogopa nini na mjombako anakuona
<i>Witelemwa ni kyau na nau no ukwene</i>	Unaogopa nini na babako anakuona
<i>Witelemwa ni kyau na andu no makwene</i>	Unaogopa nini na umati unakuona

Wimbo huu utaeleweka kupitia kuelewa uhalisia wa maisha katika jamii ya Wakamba ya jadi. Utamaduni wa Wakamba ulihimiza ushirikiano katika jamii. Mtahiriwa alipaswa kuonyesha ujasiri mbele ya kila mwanajamii atakayehudhuria sherehe hiyo. Katika mshororo wa 1 mtahiriwa anaulizwa, ‘unaogopa nini na mamako anakuona’, mshororo wa 2, anaulizwa ‘unaogopa nini na mjombako anakuona’, mshororo wa 3, anaulizwa ‘unaogopa nini na babako anakuona’, mshororo wa 4 anaulizwa ‘unaogopa nini na umati unakuona.’ kwa hivyo, mtahiriwa anahimizwa asionyeshe dalili za woga kwani kila mwanajamii anamtazama. Wimbo huu pia unaashiria umuhimu ambao jamii hii iliipa sherehe ya jando. Unasawiri uhalisi wa maisha katika jamii ya Wakamba ambao waliishi kwa ushirika.

Nadharia ya Ethnografia ya mawasiliano iliyoongoza utafiti huu inashikilia umuhimu wa tukio na hadhira ili kukamilisha mawasiliano. Watahiriwa waliimbiwa wimbo huu ili wajue kwamba, kila mwanajamii anawatazama kushuhudia ujasiri wao. Wengi wao walionyesha ukakamavu wasije wakakejeliwa na umati uliohudhuria. Mbinu ya balagha imetumika katika wimbo huu ili kubainisha maudhui ya ujasiri. Mtahiriwa anaulizwa ‘unaogopa nini’ katika mwanzo wa kila mshororo. Swali hili halihitaji jibu bali ni la kutilia mkazo na kusesitiza ujumbe kwamba, kila mwanajamii anamuangalia mtahiriwa hivyo, asionyeshe dalili zozote za woga asipate fedheha. Watahiriwa walijua kwamba,

kila mzazi angetaka kumuoza binti yake kwa mvulana aliyeonyesha ujasiri wakati wa tohara.

Katika kuchanganua wimbo huu, muktadha, utamaduni na mazingira ni muhimu katika kudhihirisha uhalisi wa maisha katika jamii. Kwa kuzingatia namna wanajamii wanavyowasiliana, huweza kuashiria taratibu za jamii zinazofungamana na itikadi na mila zinazoitawala. Sherehe za jando za Wakamba hazikuwa za mwanajamii bali wanajamii wote. Fasihi simulizi ni chombo ambacho kilitumiwa kuwaunganisha watu katika jamii ya Wakamba.

4.1.3. Kukejeli Tabia Zilizoenda Kinyume na Matarajio ya Jamii

Katika sherehe ya jando, mwanajamii aliyejulikana kuwa na tabia hasi alitajwa na kosa lake likakejeliwa hadharani kupitia nyimbo. Kwa sababu hii, kila mwanajamii alijaribu kukwepa kutenda jambo lolote lililoenda kinyume na maadili ya jamii asije akapakwa tope wakati wa sherehe za jando. Baadhi ya tabia zilizokejeliwa ni pamoja na;

4.1.3.1 Woga wa Kisu

Walioogopa kutahiriwa walikejeliwa na kubezwa kwa sababu ya woga wao. Kejeli hii pia ilikusudiwa wazazi wa mtahiriwa aliyeonyesha woga. Vilevile, wakati wa sherehe ya tohara, kejeli haikukusudiwa watahiriwa na wazazi wao pekee mbali kwa wanajamii walioonyesha tabia zisizokubalika katika jamii mathalan uchoyo, ukahaba, uchawi miongoni mwa tabia nyingine. Nyimbo nambari 6, 10 na 11 ni mifano ya nyimbo za

kejeli. Katika wimbosoo *uvuvwe* (Baragumu ipulizwe, Na.10) mishororo ifuatayo inaonyesha kejeli dhidi ya woga wakati wa kutahiriwa:

Wiuu mbu utethwe nuu?
Mwite mwenyu akutetee

Unapiga nduru usaidiwe na nani?
Muite mamako akutetee

Maudhui ya kejeli yanaibuliwa kupitia swali la balagha linaloulizwa mtahiriwa kupitia mshororo wa1. Mtahiriwa anaulizwa anapiga nduru asaidiwe na nani?Katika jamii ya Wakamba, tabia ya kupiga nduru inahusishwa na wanawake. Wanaume hawapaswi kuonyesha sifa ya woga kama kupiga nduru.Mtahiriwa ambaye alilia wakati wa tohara alikejeliwa hadharani kwa kusawiri tabia ya woga ambayo ni ya kike. Aidha, hisia za huruma kwa mujibu wa wimbo huu ni ishara ya udhaifu wa wanawake. Mwanaume hapaswi kuonyesha huruma hadharani kwa mfano kumuonea huruma mvulana wake akitahiriwa.Neno ‘mwenyu’ (taz. Kiambatisho 1) kama lilivyotumika katika muktadha wa wimbo huu linamaanisha ‘mama yako’. Katika jamii ya Wakamba, mtu akitumia neno ‘mwenyu’ huwa anaonyesha dharau na lugha isiyo ya heshima kwa mwanamke. Kwa kuchelea kukejeliwa, watahiriwa walijikaza kwa kukodoa macho bila kupepesa ili kujitangaza kwamba, wao ni wanaume kamili.

Ujumbe unaoenda sambamba na kukejeli woga wakati wa jando pia umeshadidiwa na mishororo ifuatayo katika wimbo *Munyambu nuukiva* (Simba anaguruma, Na. 6).

Wimbo huu uliimbwa mkesha wa jando:

Munyambu nuukiva wi ukavi Simba anaguruma akiwa ukavi.
Ni nau uwitie Ni baba aliyemwita
Sisya ndukathilie Chunga usitetemeke

Wimbo huu ulikuwa wa kutahadharisha watahiriwa dhidi ya kuogopa kisu cha ngariba. Mshororo wa 3 usemao ‘chungu usitetemeke’ una toni ya kejeji. Kutetemeka huashiria woga mkubwa. Tabia ya ukakamavu ilikuwa ya kimsingi mno wakati wa sherehe ya tohara. Kila mzazi hasa baba alimtarajia mtoto wake aonyeshe ujasiri wakati wa kukatwa ili asiye akakejeliwa kwa kuitwa mwanamke. Tabia ya woga ilifananishwa na ya kike. Kila mtahiriwa alijikaza asionyeshe dalili zozote za woga asikejeliwe na wanajamii.

4.1.3.2 Kukashifu Uchoyo

Tabia ya uchoyo pia ilikejeliwa hadharani wakati wa sherehe za tohara. Wasanii wa nyimbo za jando walitunga nyimbo kukejeli wanajamii waliojulikana kuwa wachoyo miongoni mwa tabia nyingine hasi. Katika wimbo (Na.34) *Naendie vandu* (Nilienda mahali), msanii anamshambulia mwanamke ambaye alipika chakula na kumnyima mwanajamii mwenzake kupitia sehemu ifuatayo;

<i>Naendie vandu kiveti kinavulya,</i>	Nilienda mahali mwanamke akachukua
<i>Mui, kyaua ngima nyingi</i>	Akasonga ugali mkubwa
<i>Kyambia ndikasama</i>	Akaniambia sitaionja

Katika wimbo huu, msanii anawashambulia wanawake ambao ni wachoyo na ambao hawawezi kuwalisha wanajamii wenzao. Mila na desturi za Wakamba humtarajia kila mwanajamii kuwa mkarimu. Msanii anatumia mbinu ya taswira kuchora picha ya kimo cha ugali alichopika mwanamke. Hata ingawa kimo cha ugali ni kikubwa kama asemavyo katika mshororo wa 2, *nyima nyingi* (ugali kubwa), anamyima mwenzake. Anachohimiza msanii wa wimbo huu ni kwamba, kila mwanajamii anapaswa kumsaidia

mwenzake kwa mahitaji ya kila siku kama kumpatia chakula kama ilivyokuwa katika jamii ya jadi ya Wakamba.

4.1.3.3 Mazoea ya Mwanamke ya Kutorokea kwao Baada ya Ugomvi na Mumewe

Mazoea ya mwanamke ya kutorokea kwao alikozaliwa baada ya ugomvi baina yake na mumeweilitungiwa nyimbo zilizoonyesha mtazamo wa kijamii kuhusiana na tabia hiyo. Mwanamke katika jamii jadi ya Wakamba hakutarajiwa kuwa na mazoea ya kwenda kwao kila mara hata akikosana na mumewe. Alitarajiwa kutumia mavyaa iwapo ndoa yake ingekumbwa na mtafaruku wowote ili kujaribu kumpatanisha na mumewe (Somba, 2000; Watuma, 2001). Kupitia sehemu ifuatayo ya wimbo Na. 35 *Naangiwe muunda niSyomasengela* (Nilikanyangiwa shamba na Syomasengela),mwanamke kwa jina *Syomasengela* anakejeliwa kutokana na tabia yake ya kuenda kwao kila mara.

Naangiwe muunda ni Syomasengela

Aendaa ku?

Aendaa kwoo

Kitau kyaumania muthumo nokanywa

Nilikanyangiwa shamba na Syomasengela

Alikuwa akienda wapi?

Alikuwa akienda kwao.

Kidonda kimetoka mguuni hadi kinywani.

Lengo la msanii kutunga wimbo huu ni kusimanga wanawake ambao wana tabia ya *Syomasengela* ya kukimbia kwao kila mara wapatapo shida katika ndoa zao. Msanii kupitia mshororo wa 1 na wa 3 anasema alikanyangiwa shamba na *Syomasengela* akienda kwao. Aidha, katika mshororo wa 4 anasema *Syomasengela* ana kidonda kikubwa kutoka mguuni hadi kinywani kuashiria kwamba, alikuwa amechapwa na mumewe. Msanii anatumia taswira ya mwanamke huyo anayepitia katika shamba akitorokea kwao kuibua maudhui ya kejeli kwa wanawake ambao kwa mujibu wa wimbo huu, hawatumii

mantiki. Wimbo huu unalenga pia kupitisha ujumbe kwa wanajamii kwamba, hawapaswi kupitia kwa mashamba ya wenyewe. Kukanyanga mashamba husababisha ukavu. Mwanamke katika wimbo huu anasawiriwa kama kiumbe kisichotumia mantiki kwa sababu kila binadamu aliyekomaa anapaswa kujua kwamba, mashamba hayapaswi kukanyangwa.

4.1.4Kupongeza Wazazi wa Mtahiriwa

Baadhi ya nyimbo za jando za Wakamba kabla ya majilio ya wakoloni zilikuwa na maudhui ya kuwasifia baadhi ya wanajamii kutokana na sifa zao nzuri. Kila mwanajamii aliyeonyesha tabia chanya kama ukarimu, bidii kazini, heshima miongoni mwa tabia nyingine alisifiwa. Mfano mzuri wa nyimbo za sifa ni wimbo Na. *3Nau niwandila* (Baba amenitahiri,) kupitia sehemu ifuatayo:

<i>Aliili! Nau niwandila</i>	Aliili! baba amenitahiri
<i>Niwambumya utunduuni</i>	Amenitoa ujingani
<i>Aliili ! Nau niwandila</i>	Aliili! baba amenitenga

Wimbo huu unaashiria furaha ya mtahiriwa. Anamsifia babake kwa kumpeleka kwa tohara anaposema *nau niwandila* (baba amenitahiri) mshororo wa 1. Mtahiriwa anamsifia babake kwa kumpeleka jandoni ambapo sasa amekuwa mtu mzima kulingana na utamaduni wa tohara katika jamii ya Wakamba. Vilevile, anamsifia babake kwa kumtoa ujingani na kumtenga. Kumtenga katika mshororo wa 3 kuna maana kuwa, mtahiriwa ametengwa na kundi la wavulana ambao hawajatahiriwa maarufu kama *ivisi*(taz. Kiambatisho 1)katika jamii ya Wakamba. Kuondolewa ujingani katika muktadha huu ina maana ya kuvuka ngazi ya utotoni hadi utu uzima ambapo, watahiriwa wanaelimishwa

kuhusu majukumu yao ya utu uzima, mambo ya unyumba, siri za jamii, masuala kuhusu historia ya jamii miongoni mwa mengine. Kila mzazi aliyemlea mwana, mpaka kufikia kiwango cha kutiwa jandoni alisifiwa kwa kushikilia jukumu lake hilo.

4.1.5 Kusifia Ngariba

Wimbo *Munyambu nuukiva* (Simba anaguruma, N. 10) ni mfano wa nyimbo zilizoimbwa katika sherehe ya jando ya Wakamba ili kusifia Ngariba. Jukumu la kuchagua ngariba atakayetahiri vijana lilitwikwa baba wa mtahiriwa au mjomba wake. Ngariba alichaguliwa kwa kuzingatia hulka zake, tajriba, mafanikio yake, ustadi wake wa kutahiri vijana vizuri, na ambaye alitumia dawa nzuri ya kuonya kidonda haraka. Sehemu ifuatayo inaonyesha sifa zilizomiminiwa ngariba ili atahiri vizuri;

Munyambu nuukiva wi ukavi
Ni nau uwitie
Sisya ndukathilie

Simba anaguruma akiwa ukavi.
Ni baba aliyemwita
Chunga usitetemeke

Wimbo huu ulikuwa na lengo la kumsifia ngariba ili watahiriwa wawe na imani naye na pia yeye ahisi amethaminiwa na jamii. Mshororo wa 1 ni jazanda ambayo inamlimbikizia ngariba sifa kwa kumfananisha na simba (Simba anaguruma). Simba ni mnyama mkali ambaye anaogopwa na binadamu kwa ukali wake (angurumapo simba mcheza nani?). Katika muktadha wa wimbo huu msanii anamlinganisha ngariba na simba ili aweze kutekeleza wajibu wake ipasavyo kwa kufahamu kwamba, wanajamii wanamwamini na wanamdhamini kupitia kazi yake. Watahiriwa wanaambiwa kwamba, ngariba huyo mkali asiogopwe kwa sababu aliyemualika ni baba hivyo, hawezi kuwadhuru kulingana namshororo wa 2 (ni baba aliyemwita). Kwa mujibu wa Wathome (2009), kuna ngariba

wengine ambao baada ya kutahiri, kidonda cha mtahiriwa kilichukua muda mrefu kupona hivyo basi, wakasemekana wana ‘mkono mzito’ (*kwokwo kuito*). Kutokana na imani hii, ngariba aliyechaguliwa alifahamu kwamba, wanajamii wanamwamini kwa umahiri wa kutahiri. Kutokana na imani hii, watahiriwa wanahimizwa wasitetemeke (mshororo wa 3) kutokana na sababu kwamba, ngariba atakayewatahiri ni mweledi katika kazi yake na ataifanya kwa ufasaha. Lengo la kumfananisha ngariba na simba lilikuwa la kumlimbikizia sifa ili atahiri vijana kwa ufasaha.

4.1.6 Kushauri Watahiriwa kuhusu Ngono za Kwanza

Sherehe ya jando ilikuwa njia kuu ambapo elimu ya jadi iliweza kupitishwa kwa watahiriwa na wanajamii wote. Nyimbo za jando zilikuwa na ushauri wa hali ya juu ambao haungeweza kutolewa katika muktadha mwingine. Sherehe ya jando ilikuwa sehemu muhimu ya mapisi katika maisha ya wavulana. Nyimbo zilizoimbwa katika sherehe hii zilijumuisha mafunzo ya kitamaduni yaliyosheheni matarajio ya mtahiriwa baada ya jando. Mshororo ufuatao wa wimbo *Niwa nithi* (naambiwa niende, Na.5) unaonyesha maudhui ya ushauri kwa watahiriwa kuhusu ngono ya kwanza ikizingatiwa kuwa, ni wavulana waliotahiriwa pekee ndio waliokuwa na kibali cha kuchumbiana na kuo katika jamii ya Wakamba.

Kitumbulu kya mbee kina muthanga Kuma ya kwanza ina changarawe

Msanii wa wimbo huu anawaonya watahiriwa kwamba, sehemu za siri za wanawake watako chumbiana nao kwa mara ya kwanza zina changarawe. Hili ni fumbo ambalo lina maana kwamba, kitendo cha ngono hakitakuwa rahisi mara ya kwanza. Ie tajiriba

watakayopata kutokana na ngono za kwanza itakuwa kinyume na matarajio yao. Wimbo huu uliimbwa kabla ya tohara ili kumfungulia mtahiriwa ukurasa mpya kuhusu mapenzi. Una ushauri ambao haungeweza kutolewa kwa kikao kingine chochote kwa wakati huo isipokuwa katika sherehe ya jando. Katika utamaduni wa Wakamba, ni wakati wa jando tu ambapo ushauri kuhusu maswala ya ngono ungeweza kupitishwa kwa vijana.

Ili kuelewa baadhi ya nyimbo kama asemavyo Saville- Troike (1982), lazima tuelewe aina ya ujumbe unaokusudiwa hasa kwa kuzingatia utamaduni unaofuatwa na wanajamii husika. Kutokana na wavulana kuchukuliwa kuwa hawana tajriba yoyote kuhusu ngono kabla ya tohara, wimbo huu uliimbwa ili kuwatayarisha kuhusu mahusiano yao na wanawake.

Matumizi ya manenokulingana na muktadhayanatiliwa uzito na nadharia ya Ethnografia ya mawasiliano iliyoongoza utafiti huu. Hymes (1974) anasema ili kuelewa maana ya misemo na utaratibu wa kuongea, ni lazima swala la muktadha lizingatiwe. Katika wimbo huu, ni muhimu kuelewa maana ya neno 'changarawe' katika muktadha wa jando. 'Changarawe' hii si ile ya kawaida bali ni ule ugumu watakaokabiliana nao wakati wa kufanya mapenzi. Mbinu ya sitiari imetumiwa kulinganisha na kufananisha ngono ya kwanza na sehemu ya siri ya mwanamke ambayo ina changarawe. Wimbo huu unaonyesha uhalisi katika maisha ya jadi ya Wakamba ambapo kulingana na mila na tamaduni zao, wavulana walitarajiwa kujiepusha na ngono mpaka baada ya kutiwa jandoni.

4.1.7 Matarajio ya Jamii kwa Watahiriwa

Baadhi ya nyimbo za jando za jamii ya Wakamba kabla ya majilio ya wakoloni zilisheni kwa kiasi kikubwa matarajio ya jamii kwa mtahiriwa na wanajamii wengine. Watunzi walitunga nyimbo zilizosheni maudhui kuhusu matarajio ya kijamii ili kila mwanajamii ayatilie maanani kujiepusha na lawama. Huu ndio msingi wa kuimba wimbo *Mwanake ndaneena na kiveti kyeene* (Mvulana hatongozi mwanamke wa wenyewe, Na.15) kama vile mshororo ufuatao wa wimbo huu unavyoshadidia:

Mwanake ndavoyaa kiveti kyeene Mvulana hatongozi mke wa mwenyewe

Wimbo huu unapitisha onyo kwa watahiriwa na wavulana wengine kwamba, jamii inawakataza kutongoza mwanamke aliyeolewa. Jamii ya jadi ya Wakamba haikutarajia mvulana kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanamke aliyeolewa. Tabia hii ilikashifiwa na waliopatikana wakiwa na uhusiano huo waliadhibiwa vikali katika kikao maalum kilichojulikana kama *mbai*(taz. Kiambatisho, 1).

Zaidi ya hayo, watahiriwa walitarajiwa kuwa *nthele*(taz. Kiambatisho, 1) baada ya tohara. Jukumu moja muhimu ambalo walipaswa kutekeleza ni kuilinda jamii kutokana na uvamizi wowote kutoka kwa majirani zao. Wimbo *Ekuyu mesilile Mutha* (Wagikuyu walipitia Mutha, Na. 14) kupitia mshororo huu unashadidia hilo:

Ekuyu mesilile Mutha, Wagikuyu walipitia Mutha

Msanii anapitisha historia ya uhasama baina ya jamii ya Wakamba na majirani zao kupitia wimbo huu. Neno ‘Mutha’ linawakilisha sehemu ya Ukambani ambapo Wakamba kutoka Tseikuru hupakana na Watigania. ‘Wagikuyu’ katika muktadha wa

wimbo huu ni majirani wa Wakamba. Watahiriwa hivyo basi wanamulikiwa sehemu ambayo maadui zao walikuwa wakipitia kulingana na historia ya jamii yao ili waweze kujitayarisha kuilinda jamii.

Vilevile, baadhi ya nyimbo za kipindi cha kabla ya ukoloni zilitungwa zikiwa na lengo la kuonya watahiriwa dhidi ya uvivu. Jamii ya Wakamba katika kipindi cha kabla ya ukoloni ilimtarajia mtahiriwa kuwa na bidii kazini ili kuonyesha uwezo wa kuikimu familia yake akioa. Tabia ya uvivu ilikashifiwa hadharani wakati wa sherehe ya jando. Ilifananishwa na sifa ya kike. Mwanamume katika jamii ya Wakamba alitarajwa kuikimu familia yake kupitia majukumu aliyotengewa na jamii. Mfano wa wimbo uliosheheni kashfa ya kijamii kuhusu uvivu ni kama wimbo Na. 37 *Wotitingilya na mwenyu* (Bure tu kama mamako) kupitia sehemu ifuatayo:

<i>Wotitingilya na mwenyu</i>	Bure tu kama mamako
<i>No titi kivila</i>	Kazi yake ni kukaa tu na kustarehe

Wimbo huu una lengo la kuonya watahiriwa na vijana wengine dhidi ya uvivu. Mtahiriwa anaonywa dhidi ya kukaa tu bila kufanya lolote kama mwanamke katika mshororo wa 2. Kwa mujibu wa wimbo huu, mwanamke ndiye humilikisifa ya uvivu (mshororo wa 1). Wimbo huu ulitungwa ili kuwaonya wajiambae na sifa za kike kama uvivu.

4.1.8 Nafasiya Mwanamke katika Jamii

Picha ya mwanamke kama kiumbe duni, asiye na akili razini na asiyetumia mantiki iliendelezwa katika nyimbo za jando za jadi katika jamii ya Wakambakwa nia ya kumdunisha. Baadhi ya nyimbo za jando katika kipindi cha kabla ya ukoloni zinamchora

mwanamke kama kiumbe duni na ambaye anatumiwa kama kifaa cha kumfurahisha mwanamume. Hoja hii imeshadidiwa na wimbo, *Naamukawua naka* (Nilikuwa nikiamshwa na wanawake, Na.8) katika sehemuifuatayo;

<i>Namukawua naka ngomete ii</i>	Nilikuwa nikiamshwa na wanawake nikilala
<i>Ngiwa nenda nithi ngwate nondo</i>	Ninaambiwa nikitaka niende nikawashike matiti
<i>Na ngikwata ngitavwua ni tata we!</i>	Nikiyashika baba ananikemea, wacha! <i>Isu ni mali</i>
<i>yakwa ngathoosya kila ngwenda</i>	Hiyo ni mali yangu nitaiuza nitakacho.

Maudhui yanayohusu kudunishwa kwa mwanamke katika jamii ya Wakamba yanaibuliwa kupitia mshororo wa 2 unaosema, *ngiwa nenda nithi ngwate nondo* (Ninaambiwanikitaka nishike matiti).Taswira kama hii inamchora mwanamke kama kiumbe dhaifu kimapenzi, anayemshawishi mwanaume ambaye si mume wake kumshika matiti.Licha ya kuchukuliwa kama chombo cha kumfariji mwanamume kama vile mshororo wa 2 unavyobainisha, mwanamke pia amesawiriwa kama bidhaa ambayo inaweza kuuzwa bei yoyote aitakayo mwenyewe.Taswira inayoibuliwa na mshororo wa 4 usemao *isu ni mali yakwa ngathoosya kila ngwenda*(hiyo ni mali yangu nitaiuzanitakacho) ni ya kiumbe ambaye ni kama sanamu. Hana uhuru wa kujiamulia lolote lile. Mshororo wa 4 unaashiria mahari ambayo baba wa msichana anapata akimwoza bintiye. Mbinu ya istiari imetumiwa katika mshororo wa 4, kumfananisha mwanamke na bidhaa.

Suala la mahari katika jamii ya Wakamba lina historia ndefu. Mahari ni mojawapo ya asasi za kijamii ambazo zimehifadhiwa na kuendelezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hii ni mila ambayo inaendelea kufuatwa katika jamii nyingi za Kiafrika. Katika jamii ya Wakamba, mahari ni utamaduni ambao jamii za jadi zilitumia kumsawiri

mwanamke kamabidhaa. Kutokana na kubidhaahishwa kwa mwanamke, kila mwanaume aliyezaa mabinti aliwaona kama mali atakayoipata akiwaoza (Nzioki 1982).

Mwanamke akiposwa na kuolewa katika jamii ya Wakamba inasemekana amenunuliwa (Nzioki, 1982). Analipiwa ng'ombe watatu, mbuzi kumi na wawili, buyu kubwa la asali, pesa taslimu kama elfu hamsini zinazojulikana kamambesa sya mukwaambazo zinakabidhiwa mama wa msichana kwa uchungu wa kuzaa, miongoni mwa bidhaa nyingine (Kimilu, 1962; Mbiti, 1969; King'ei, 1982). Huku ni kumdhalilisha mwanamke. Kutokana na kununuliwa huku, mwanamke alipaswa kumnyenyekea mumewe kwa vyovyote vile na awe na heshima kwa wanaume wote kwa jumla (Somba, 2000).

Akizungumzia suala la mahari, Uvetie akinukuliwa na Gibbe (1978) anaeleza kuwa, itikadi ya ubabedume ilipoanza kumkandamiza mwanamke, iliamua kumkaba zaidi huyo mwanamke kwa kumlipia mahari. Taswira inayoibushwa na kitendo cha kumkaba mwanamke inaashiria binadamu anayenyimwa uhuru wa kutenda lolote. Uvetie anasema mahari yalimtia mwanamke pingu, yakamfanya mtumwa. Utumwa huu wa mwanamke katika jamii ya Wakamba unamnyima uhuru wa kujiamulia. Maamuzi kumhusu yanafanywa na babake. Kwake bintiye ni mali ambayo anaitunza vyema ili aweze kuiuza atakavyo.

Hymes (1974) anasisitiza kuwa, ili kung'amua maana ya maneno, ni muhimu kuzingatia suala la muktadha. Katika muktadha wa wimbo huu, neno matiti katika mshororo wa 2 lina maana ya kutenda kitendo cha ngono. Maana yake inaeleweka kulingana na

muktadha wa wimbo. Aidha, kumithilisha mwanamke na mali katika mshororo wa 4 kutaeleweka kulingana na kuelewa utamaduni wa suala la mahari katika jamii husika. Saville- Troike (1982) anashikilia hili kwa kusema kuwa, lazima tuelewe aina ya ujumbe unaokusudiwa hasa kwa kuzingatia utamaduni unaofuatwa na wanajamii husika. Maudhui ya nafasi duni aliyotengewa mwanamke na jamii ya Wakamba yanachukua nafasi muhimu katika wimbo huu. Huu ulikuwa uhalisia wa maisha kabla ya majilio ya wakoloni.

Wimbo mwingine ambao unamsawiri mwanamke kama kiumbe asiyetumia mantiki ni wimbo (Na. 15) *Mwanake ndaneena na kivetu kyeene* (Mvulana hatongozi mke wa mwenyewe). Katika wimbo huu, mwanamke anasawiriwa kama asiyejali, na anayefanya mapenzi na wavulana ambao hawajatahiriwa. Sehemu ifuatayo ni mfano mzuri;

<i>Mwanake ndavoyaa kivetu kyeene</i>	Mvulana haombi mke wa mwenyewe
<i>Anengawe kwa kutalilya</i>	Anapewa kwa kubahatisha
<i>Kiu ndyaakiwua</i>	Sijasikia hilo

Mshororo wa 1 unawaonya watahiriwa dhidi ya kumtongoza mwanamke aliyeolewa. Mshororo wa 2 usemao ‘anapewa kwa kubahatisha’ unathibitisha kuwa, mwanamke aliyeolewa alishiriki ngono na vijana wadogo ambao hawajatahiriwa. Mshororo wa 3 usemao, *kiu ndyaakiwua* (Sijasikia hilo) una maana kuwa, mila na tamaduni za Wakamba hazimruhusu mvulana na mwanamke aliyeolewa kujihusisha katika kitendo cha ngono. Wimbo huu unamchora mwanamke kama kiumbe dhaifu kimapenzi. Una lengo la kumkashifu mwanamke ambaye ana tabia ya kushawishiwa na wavulana ambao hawajatahiriwa kushiriki ngono nao. Wimbo huu unaonyesha mwelekeo wa jamii ya

Wakamba kuhusu wanawake ambao walichukuliwa kama viumbe duni wasio na akili. Wanasawiriwa kama makahaba ambao wanaweza kutenda lolote la aibu kama kushiriki ngono na wavulana wadogo wasio wa rika lao.

Vilevile, kuna baadhi ya nyimbo za jando za jamii ya Wakamba ya jadi ambazo zilitungwa kupitisha ujumbe kwa watahiriwa na wanajamii wengine kwamba, mwanamke anapaswa kupigwa. Kwa mujibu wa Watuma (2001), mwanamke katika jamii ya Wakamba alipaswa kuadhibiwa kupitia kuchapwa na mumewe ama, wakati mwingine na mwanaume mwingine rika la mumewe akimkosea mumewe heshima. Kutokana na mila hii, wanawake walichapwa kiasi cha kupata majeraha. Wimbo Na. 35 *Naangiwe muunda ni Syomasengela* (Nilikanyangiwa shamba na Syomasengela)

kupitia sehemu ifuatayo ni mfano mzuri:

<i>Naangiwe muunda ni Syomasengela</i>	Nilikanyangiwa shamba na Syomasengela
<i>Aendaa ku? Aendaa kwao</i>	Alikuwa akienda wapi? Alikuwa akienda kwao
<i>Kitau kyaumaniamuthumo</i>	Kidonda kimeanzia mguuni
<i>Nokyo ki kanywa</i>	Mpaka mdomoni

Wimbo huu unaibua taswira ya mwanamke ambaye amejeruhiwa vibaya kutokana na ugomvi wa kinyumbani. Mshororo wa 3 unasema Kidonda kimeanzia mguuni hadi kinywani. Kichapo alichopata Syomasengela kinampelekea kutorokea kwa wazazi wake kulingana na mshororo wa 2. Kupitia wimbo huu, msanii anamchora mwanamke kama kiumbe duni na dhaifu ambaye anapaswa kuadhibiwa na mumewe. Wimbo huu unaonyesha uhalisia wa maisha ya ndoa katika kipindi cha kabla ya ukoloni ambapo kwa mujibu wa Nzioki (1982), mwanamke aligeuzwa mali ya mwanaume kupitia mahari

aliyolipiwa na mume huyo. Mwanaume alikuwa na uhuru wa kumtendea mkewe atakalo kutokana na sababu kwamba, alikuwa amemnunua.

Taasubi ya kiume katika jamii nyingi za Kiafrika ilizusha tafsiri na sifa ambazo zilimtazama mwanamke kwa namna iliyopotoka (Masinde, 2003). Tafsiri hizi ziliathiriwa na mazingira mbalimbali yaliyogumbikwa na uhalisia wa maisha katika jamii husika. Huu ni mkabala wa kuumeni ambao ulitawala jamii nyingi jambo ambalo lilichangia kudunishwa na kupuuzwa kwa mwanamke.

4.1.9 Majukumu ya Kiuana

Wakati wa tohara ndogo, watahiriwa waliimbiwa nyimbo zilizoashiria kwamba, sasa lililongojewa kwa siku nyingi linatendeka. Kupitia nyimbo hizo, watahiriwa walitarajiwa kupata ujumbe kwamba, wamevuka daraja kutoka utotoni hadi utu uzima ambapo, wangehitajika kuchukua majukumu ya kiuana kama kuoa na kujikimu kimaisha. Wimbo *Mwai kwa niwalika ndiani* (Mtahiriwa ameingia kidimbwini, Na. 13), unaonyesha kwamba, mtahiriwa amevuka daraja kutoka utotoni hadi utu uzima na anatarajiwa kujikimu kimaisha, pasipo kuwategemea wazazi wake. Sehemu ifuatayo ya wimbo huu inaashiria hilo;

<i>Mwai kwaii</i>	Mtahiriwa ii
<i>Yu niwalika ndiani</i>	Sasa ameingia kidimbwini
<i>Ndiani ya kulungilwa</i>	Kidimbwi cha kujitafutia.

Wimbo huu uliimbwa wakati mtahiriwa alikuwa tayari ‘anakatwa’. Una lengo la kumfahamisha kwamba, umewadia wakati wake wa kuingia katika kina kirefu cha

maisha. Mshororo wa 2 unasema ‘sasa umeingia kidimbwini’. Mbinu ya jazanda imetumiwa na msanii katika wimbo huu kufananisha maisha na kidimbwi cha maji. Wimbo huu ulikusudiwa kumpa mtahiriwa mawaidha ya maisha ya utu uzima yanayomsubiri. Mshororo wa 3 usemao ‘kidimbwi cha kujitafutia’ una maanisha kuwa, mtahiriwa baada ya sherehe hii atatwikwa majukumu ya utu uzima kama kuoa na kuanza maisha mapya ya kuikimu familia yake bila kutegemea wazazi wake. *Nenokulungilwa* katika mshororo wa 3 limetumiwa kitamathali. Katika lugha ya Kikamba, linamaanisha kutengwa kwa vifaranga na mama yao ili apate nafasi ya kutaga mayai tena.

Nadharia ya Uamali kwa mujibu wa Levinson(1983) inashikilia kwamba, maana ya maneno hueleweka kulingana na muktadha yalimotumika. Ili kuelewa maana ya neno *kulungilwa* kama lilivyotumika katika wimbo huu, ni lazima pia kuelewa muktadha lilipotumika. Katika muktadha wa jando, neno hili linaibua maana ya watahiriwa kutengwa na wazazi kutokana na machukulio kwamba, sasa wamekuwa watu wazima ambao wanaweza kujitegemea. Kupewa zawadi kwa vijana ili waweze kuanza maisha yao upya bila kuwategemea wazazi ndio kunafananishwa na kutengwa kwa vifaranga. Zawadi alizopewa mtahiriwa ziliashiria kwamba, sasa ana mali ya kumwezesha kuanza maisha yake upya. Zawadi hizi zilikuwa ng’ombe, mbuzi, kondoo, kuku, shanga, nyute miongoni mwa zawadi nyingine (Nzioki 1982). Wimbo huu ulipitisha ushauri kwa mtahiriwa kwamba, baada ya tohara, angekuwa na uhuru wa kupata jiko na kujikimu kimaisha. Wazazi wake hawana ulazima wa kumlisha tena.

4.1.10 Migogoro ya Kijamii

Katika jamii za Kiafrika, uhasama kati ya makabila na koo mbalimbali ulikuwepo mara kwa mara. Uhasama huo ulisababisha vita miongoni mwa jamii na koo jirani (Were na Wilson, 1968; Finnegan, 1970; Nketia, 1982). Jamii ya Wakamba sawa na jamii zingine ilipitia uadui na uhasama na makabila jirani kama Wagikuyu na Wamasai miongoni mwa makabila mengine kutokana na sababu za kutangamana wakifanya biashara ama wakilisha mifugo wao. Nyimbo jadiya zikiwemo za jando zilitungwa ili kusawiri migogoro ya kijamii. Migogoro ya kijamii ilijitokeza kupitia nyimbo za jando kwa mfano, kupitia sehemu ifuatayo ya wimbo *Ekuyu mesilile Mutha* (Wagikuyu walipitia Mutha, Na. 14) :

<i>Ekuyu mesilile Mutha</i>	Wagikuyu walipitia Mutha
<i>Kiveti cha Kavyu nikyavenwa muume</i>	Mke wa Kavyu amenyang'anywa mume
<i>Koma na mwenyu uthele</i>	Lala na mamako uangamie

Wimbo huu unasheni maudhui ya kuelimisha watahiriwa kuhusu migogoro ya kijamii. Waliotajwa katika wimbo huu ni Wagikuyu ambao wanasimamia majirani wote wa jamii ya Wakamba. Watahiriwa walipaswa kujua na kufahamu historia ya jamii yao hususan kuhusiana na uhasama uliokuwepo kati ya jamii yao na majirani. Uadui huu ulisababisha vita vya mara kwa mara. Wakati wa kiangazi, baadhi ya wanajamii hasa wanaume walilazimika kuhamia sehemu walizokaa Wagikuyuhasa wa Kirinyaga, sehemu za Igembe ama sehemu nyingine ambapo wangepata chakula. Baadhi ya wanaume walikuwa wakihamia huko na kuwaoa wanawake kutoka sehemu hizona kutelekeza familia zao kama vile mshororo wa 2 unavyoeleza *kiveti kya Kavyu nikyavenwa muume* (mke wa Kavyu amenyanganywa mume). Wanawake wengi waliachiwa

majukumu ya kuwakimu watoto. Wengi wa wanaume waliohama Ukambani kuelekea sehemu za Kirinyaga waliwekewa libwata na wanawake waliowachukua kiasi kwamba, walikuwa wakitekeleza majukumu ambayo katika jamii ya Wakamba yanatengewa wanawake kama kupika, kukama ng'ombe, kuchota maji, kupalilia mimea shambani miongoni mwa majukumu mengine. Wimbo huu uliimbwa kuwasuta wanaume kama hao ambao waliamua kutoroka familia zao kwa sababu ya shida.

Kadhalika, wimbo huu unawatahadharisha wavulana waliotahiriwa kuhusu uwezekano wa kupoteleakwa Watigania, Wakikuyu, ama makabila mengine na kuwaacha wanawake zao. Kwa hivyo, walishauriwa wajihadhari na wanawake wengine ambao wangewalaghai na kuwafanya kutelekeza jamii zao. Kutokana na historia hii ya baadhi ya wanaume kutoroka nyumbani na kwenda kuishi katika jamii nyingine, uhasama uliingia baina ya jamii ya Wakamba na baadhi ya jamii hizo kiasi kwamba, wavulana kutoka jamii ya Wakamba walikuwa wakionywa kutoa wake kutoka jamii ambazo wanawake zao huwawekea wanaume libwata.

4.1.11 Ushirikiano wa Kijamii

Baadhi ya nyimbo zilizoheni maudhui ya umuhimu wa ushirikiano wa kijamii kwa mfano wimbo *Miunda ni mali* (mashamba ni mali, Na.17) kupitia mishororo ifuatayo:

<i>Miunda ni mali ya onthe</i>	Mashamba ni mali ya wote
<i>Vivya uimbivisya</i>	Choma ukinichomea

Katika utamaduni wa jadi wa Wakamba, mashamba yalikuwa mali ya wanajamii. Hayakuwa ya mtu binafsi. Wanaume walishiriki pamoja katika kutayarisha mashamba

wakati wa ukavu hususan, kufyeka na kuchoma miti iliyokatwa ili shamba liwe tayari kulimwa wakati wa mvua. Kwa mujibu wa wimbo huu, ushirikiano wa kijamii wakati wa shughuli muhimu kama hii unatiliwa uzito na mshororo wa 2, ‘choma ukinichomea’ ukiwa na maana kuwa, ukitayarisha kwako, hata kwangu tayarisha.

Kwa kiwango kingine, maudhui ya ushirikiano yalijitokeza katika nyimbo za jando ili kubainisha nafasi ya kila mwanajamii. Ni wakati wa sherehe hii ambapo watahiriwa walijulishwa aila yao yaani, wakwe, wajomba, shangazi miongoni mwa wengine. Maudhui haya yanabainishwa kupitia wimbo Na. 7 (Mwasya yilili) katika mishororo ifuatayo:

Witelemwa ni kyau na mwenyu no ukwene Unaogopa nini na mamako anakuona
Witelemwa ni kyau na mwivawa no ukwene Unaogopa nini na mjombako anakuona
Witelemwa ni kyau na nau no ukwene Unaogopa nini na babako anakuona
Witelemwa ni kyau na andu onthe no makwene Unaogopa nini na watu wote wanakuona

Katika muktadha wa wimbo huu, ilikuwa muhimu kwa kila mwanajamii kuhudhuria hafla hii ili kuonyesha mshikamano wa kijamii kama vile mshororo wa 4 unavyobainisha (Unaogopa nini na watu wote wanakuona).

Kwa mujibu wa nadharia ya Uamali (Levinson, 1983), maneno hueleweka tu kulingana na utamaduni na muktadha wa kijamii. Kuelewa utamaduni wa Wakamba kabla ya majilio ya wakoloni ambao ulishikilia kuwa, mashamba ni mali ya kila mwanajamii kutarahisisha kuelewa maudhui yanayopitishwa kupitia wimbo huu (Na, 17). Msanii wa wimbo huu anatumia mbinu ya taswira kuchora picha ya ushirika wa wanaume katika kutayarisha mashamba ili kuisitiza umuhimu wa kufanya kazi kwa ushirika katika jamii.

4.1.12 Kuelezea Historia ya Jamii ya Wakamba

Baadhi ya majukumu yaliyotekelezwa na nyimbo za jando katika jamii ya Wakamba ni kuhifadhi historia ya jamii hii. Wavulana walifunzwa matukio makuu ya kijamii kwa mafanovita vikuu vya dunia ambapo, wengi wa wanaume Wakamba walishiriki na kupoteza maisha yao. Sehemu ifuatayo ya wimbo *Mundu ndakusaa Ngai atanenda* (Binadamu hafi Mungu asipopenda, Na.18) inatoa taswira ya matukio ya vita hivyo kwa watahiriwa:

Meli yaathwa nivo ngivoya

Meli ikashambuliwa nikiomba

No syongo sya andu noonie kiwuni

Ni vichwa vya watu tu niliona majini

Nyimbo jadiiya za Wakamba zikiwemo za jando zilikuwa na rekodi ya historia ya jamii hii. Nyimbo hizo zilienda sambamba na matukio ya kihistoria. Usuli wa wimbo huu ulitokana na vita vikuu vya dunia. Wanaume katika jamii ya Wakamba walichukuliwa kwenda kushiriki katika vita vya kwanza vya dunia (1914) na vya pili vya dunia (1939) kule Burma. Wimbo huu ulitungwa na ukawa unaimbwa katika sherehe za jando kuwakumbusha vijana na wanajamii wengine tukio hili muhimu la kihistoria. Hii ni kwa sababu Wakamba hutumia fasihi simulizi kama ghala muhimu ya kuhifadhi mila na tamaduni zao.

Wimbo wa pili ambao ulitungwa ili kupitisha historia ya jamii ya Wakamba ni wimbo *Syokimau* (Na. 28) kupitia sehemu ifuatayo:

Syokimau ndathanie

Syokimau alitabiri

Andu eu, makuitwe ni syimbalutya

Watu weupe ndani ya vipepeo

Angi me nzokani,

Wengine ndani ya nyoka

Makuite myaki mivukoni

Wakiwa na moto kwa mifuko

Maineena ta nyunyi

Wakiongea kama ndege

Wimbo huu unasawiri historia ya Wakamba na fasihi simulizi yao. Syokimau ni jagina wa Wakamba ambaye anasomwa katika historia na fasihi simulizi yao. Ni mwanamke ambaye alikuwa na kipawa cha kutabiri matukio ya usoni na yanatendeka kulingana na utabiri wake. Kulingana na historia ya jamii hii, Syokimau alitabiri majilio ya wakoloni barani Afrika. Kupitia sehemu ya wimbo huu (Na. 28) kama ilivyonukuliwa hapo juu, Syokimau alitabiri na kusema anaona watu weupe wakija wakiwa ndani ya nyoka mkubwa na wengine ndani ya vipepeo. Vilevile, alitabiri kuwa watu hao wanaongea kwa kasi kama ndege lugha ngeni na wamebeba moto mifukoni. Utabiri huu kulingana na Wakamba ulitimia. Vipepeo ni ndege na nyoka mkubwa ni gari la moshi. Wakavumbua moto unaowekwa kwa mifuko (viberiti), na ambao walitumia lugha ya Kiingereza. Msanii wa wimbo huu alikuwa na lengo la kumsifia jagina wa Wakamba Syokimau na wakati huo huo kupitisha historia ya jamii hii kwa vizazi vya leo.

Kwa jumla, nyimbo katika kipindi cha kabla ya ukoloni zilibainisha masuala ya kimsingi kama kuonya, kukejeli, kupongeza ujasiri, kushauri, na kuelimisha watahiriwa kuhusiana na majukumu yao ya utu uzima. Aidha, zilikuwa na maudhui ya kuwaelimisha watahiriwa umuhimu wa ujasiri ambao ulitiliwa maanani na wanajamii hii wakati wa sherehe za jando. Kwa wazazi wa mtahiriwa, nyimbo hizi ziliwapongeza kwa kuzaa na kumtunza mtoto wao hadi akafikia kiwango cha kutahiriwa. Wavulana nao walishauriwa dhidi ya mambo mengi hususankuhusu ngono ya kwanza, walionywa dhidi ya kuwachukua wanawake walioolewa na kuwafanya wake zao miongoni mwa mafunzo mengine. Maudhui katika nyimbo za kipindi hiki yalikuwa ni kuwapa ushauri na pia

kuwatia moyo watahiriwa. Nyimbo za jando za kabli ya ukoloni ziliwatayarisha watahiriwa kuhusu sherehe yenyewe na vilevile kuhusu maisha ya baadaye.

4.2 Maudhui ya Nyimbo za Jando za Wakamba katika kipindi cha baada ya Ukoloni.

Fasihi nzuri ni ile yenye kuelimisha, kuhimiza, kuboresha au kuimarisha ujenzi wa jamii imara yenye uadilifu na usawa (Njogu, 2007). Kulingana na Njogu (aliyetajwa), maudhui ya fasihi yoyote huzalika kutokana na hali ya jamii ilivyo na kwa wakati wake. Wimbo una uwezo wa kutumiwa na jamii kama chombo cha kukosoa au kuongoza watu katika jamii husika. Dhamira kuu ya mwanafasihi katika utanzu wowote ule wa fasihi atakaoushughulikia huwa hasa ni kuyatumia maandishi au simulizi kwa ajili ya kuwalea, kukuza hadhira yake kwenye misingi inayokubalika, na kuijenga jamii mpya iliyokitwa kwenye maadili na falsafa njema ya maisha (Wamitila, 2003).

Vilevile, Ndungo (1985) anasema fasihi ni kielelezo cha hali halisi ya maisha. Kulingana naye, msanii kama mwanajamii huandika au kusimulia kutokana na tajriba anayoipata kutoka katika jamii anamoishi. Utafiti huu unaunga mkono maoni hayo ya Ndungo anaposhikilia kuwa, kazi nyingi za fasihi huweza kueleweka kupitia maudhui yake yanayohusu jamii na wakati fulani. Akishikilia kauli hiyo, Ngugi (1993) anasema fasihi haitoki katika ombwe tupu. Inapata mwelekeo, umbo na umuhimu wake kutoka kwa maswala ibuka katika jamii mahususi. Kwa mujibu wa Ngugi (aliyetajwa), maswala yanayoipa fasihi mwelekeo ni pamoja na uchumi, siasa, elimu, dini na mabadiliko yoyote

yatokeayo katika nyanja zozote za maisha ya jamii. Asema mabadiliko hayo huathiri kazi ya fasihi maudhui yakiwemo. Kulingana naye,tamaduni zinazobadilika ili kusawiri mabadiliko yanayotokea ndizo mwafaka zaidi.

Matukio makuu ya mwongo fulani yaweza kutambulika kutokana na fasihi ya mwongo huo, kupitia kipengele cha maudhui. Maoni haya yanatiliwa uzito na Njogu na Chimera (1999) wanaoshikilia msimamo kuwa, fasihi ni hai na hubadilika kadri jamii inavyozidi kubadilika. Kubadilika kwa maudhui ya nyimbo kulingana na wataalamu kama King'ei na Kisovi (2005) ni kwa sababu wimbo, ni utanzu wa fasihi simulizi ulio hai, ambao hukua, na kubadilika kutokana na mpito wa wakati na mabadiliko ya mfumo wa jamii.

Mabadiliko katika jamii yamewachochea watunzi kutunga nyimbo zinazolandana na wakati. Msukumo huu wa mabadiliko unaungwa mkono na Njogu na Chimera (1999) wanaposema kuwa, kuna uhusiano mkubwa baina ya sanaa na matukio ya kijamii; kwa hivyo, msanii hawezi kujitenga na matukio ya jamii yake kwani ana maslahi katika jamii hiyo. Hivi ni kumaanisha kwamba, maudhui ya msanii hutokana na mambo ambayo yanamsukuma kwa kipindi alichonacho. Maudhui yafuatayo yanaonyesha mabadiliko ya nyimbo za jando kulingana na mabadiliko ya jamii:

4.2.1 Umuhimu wa Elimu Mpya ya Kisasa

Baada ya majilio ya wakoloni, jamii ya Wakamba sawa na jamii nyingi za Kiafrika ilipapia elimu ya Kimagharibi ambayo ilihusu usomaji wa darasani. Suala la elimu ya Kimagharibi ni nyeti katika jamii ya kisasa kwa sababu inahusishwa na nguvu na uwezo

wa kiuchumi (Kauai, 2008). Kutokana na imani hii, baadhi ya nyimbo za jando zinasawiri maudhui ya umuhimu wa elimu mpya ya kisasa katika kubadilisha maisha ya wanajamii kiuchumi. Lengo la msanii kutunga nyimbo hizi ni kuhimiza vijana watilie maanani umuhimu wa masomo, ili wabadilishe maisha yao. Aidha, zinatoa changamoto kwa wanajamii ili wawaelimishe wanao. Mfano ni wimbo wa Syokimau, (Na.28) kupitia mishororo ifuatayo:

<i>Syokimau ndathanie</i>	Syokimau alitabiri
<i>Kukooka kisomo kya Mungelesa</i>	Kutakuja masomo ya Mwingereza
<i>Kwatai kisomo</i>	Shikeni masomo
<i>Muikweye muthanga</i>	Msije kutupa mchanga

Wimbo huu uliimbwa ili kuwahimiza watahiriwa na vijana wengine watilie maanani elimu ya Kizungu kama vile mshororo wa 3 unavyosema *kwatai kisomo* (shikeni masomo). Kulingana na wimbo huu, ni kupitia masomo ambapo vijana watajipusha na kazi za sulubu ambazo hazina mapato mazuri kama kutupa mchanga (mshororo wa 4). Kutupa mchanga katika wimbo huu kuna maana ya kuchimba mitaro shambani maarufu kama *levu* katika lugha ya Kikamba.

Matumizi ya nahau *kwikya muthanga*, yanajitokeza ili kuibua taswira ya ugumu wa kazi hiyo. Aidha, imetumiwa na msanii ili kuakisi utamaduni, historia na mazingira wanamoishi Wakamba. Lugha ya kitamathali iliyotumika katika wimbo huu (Na. 28) imechota maudhui yake kutoka kwa mazingira ambapo wazungumzaji wa lugha husika huishi. Wakamba kama vile tulivyong'amua katika sura ya pili ni wakulima. Wanapanda mahindi, maharagwe na mtama miongoni mwa mazao mengine. Wao huchimba *milevu* (mitaro) shambani ili kuzuia mchanga kubebwa na maji ya mvua. Uchimbaji wa mitaro

hii si rahisi. Ni kazi ya sulubu inayohitaji mda na nguvu nyingi na huchimbwa na wanaume kwa malipo fulani. Ndiposa msanii anawahimiza vijana wasome wasije kuchimba mitaro ambayo huchimbwa na walala hoi, ambao hawana njia nyingine ya kujitafutia riziki. Kuuelewa utamaduni wa jamii husika kunafanikisha mawasiliano yanayoibuliwa na wimbo wa Syokimau kwa walengwa wake.

4.2.2 Tahadhari Dhidi ya Ukimwi

Maradhi ya Ukimwi yalitambulika Afrika Mashariki miaka ya 1980 (Ngoyani, 2006; Kinara, 2012). Uvumbuzi wa maradhi haya uliwafanya wanajamii kupitia katika hatua mbalimbali za kuyumbayumba kabla ya kupata uelewa kuhusu maradhi haya. Ngoyani (2006), na Kinara (2012) wanasema maradhi ya Ukimwi mwanzoni wa mwaka wa 1980 yalijulikana kwa majina mengi ambayo yalitokea kule Marekani ambako ndiko unakisiwa kuanzia. Baadhi ya majina haya ni kama *Gay cancer*, *wrath of God syndrome* miongoni mwa majina mengine. Humu nchini Kenya, maradhi haya yalijulikana kama Ukimwi ikiwa na maana ya Upungufu wa Kinga Mwilini ambapo mwili hupoteza kinga ya magonjwa na kusababaisha kushambuliwa na magonjwa nyemelezi (Hiv/Aids Stigma. <http://www.avert.org/hiv-aids-stigma.htm>).

Vilevile, Mutembe(2009) na Kinara, (2012) wanasema maradhi haya yalitambuliwa nchini Kenya miongoni mwa wanajamii maskini ambao waliishi vijijini na waliojishughulisha na uvuvi na biashara. Utambuzi huu uliwapa wanajamii nafasi ya kuubatiza majina tofauti hususan; maradhi ya wafanyabiashara, maradhi ya makahaba na

maradhi ya madereva wa masafa marefu ambao walikuwa wakifanya biashara ya usafirishaji wa bidhaa kati ya nchi ya Kenya, Uganda na Tanzania.

Tangu ugonjwa wa ukimwi ulipogunduliwa nchini Kenya miaka ya 1980, jamii imeendelea kuhamasishwa kuhusu namna ya kujikinga na kukabiliana na maradhi haya.

Katika jamii ya Wakamba, nyimbo za kisasa za jando hutungwa ili kuwatahadharisha wanajamii kuhusiana na maradhi haya hususan wimbo *Waminwa ni Katulilangi*

(Ukimalizwa na Katulilangi, Na.19) kupitia sehemu ifuatayo:

<i>Waminwa ni nzou, ndikautula muti</i>	Ukimalizwa na ndovu , sitakulaumu
<i>Waminwa ni nzoka, ndikautula muti</i>	Ukimalizwa na nyoka, sitakulaumu
<i>Waminwa ni muthesu,ndikautula muti</i>	Ukimalizwa na donda ndugu, sitakulaumu
<i>Waminwa ni kitundumo, ndikautula muti</i>	Ukimalizwa na radi, sitakulaumu
<i>Indi waminwa ni muthelo, ngautula muti</i>	Lakini ukimalizwa na Ukimwi, nitakulaumu
<i>Waminwa ni Katulilangi, ngautula muti</i>	Ukimalizwa na <i>Katulilangi</i> , nitakulaumu.

Katika muktadha wa wimbo huu, msanii ametumia mbinu ya uradidi. Neno ukimalizwa (waminwa) limerudiwarudiwa katika kila mshororo. Urudiaji huu unalenga ujumbe wa msanii kwa watahiriwa na wanajamii kwamba, kifo kinaweza kutokea kupitia njia nyingihususan,binadamu anaweza kufariki kupitia kuuliwa na ndovu, kuumwa na nyoka, kuuliwa na donda dugu, kupigwa na nguvu za radi lakini, kumalizwa na ukimwi kupitia kuambukizwa na wanawake kama *Katulilangi* kunalaumiwa (mshororo wa 5 na 6). Kwa mujibu wa wimbo huu, *Katulilangi* ni mwanamke wa kifasihi ambaye hana msimamo. Amepewa jina la kimajazi *kutulilanga* likiwa na maana ya kurukaruka. Anashiriki ngono na wanaume wengi. Hivyo, wanaume wanatahadharishwa dhidi ya kujihusisha na wanawake kama hawa.

Ukimwi ni suala nyeti lililogubikwa katika siri (<http://www.avert.org/hiv-aids-stigma.html>). Kugubikwa kwa ukimwi kama siri katika jamii mbalimbali humu nchini Kenya kuliupelekea ugonjwa huu kuwa tatizo lililojikita katika utamaduni wa jamii husika. Mitazamo ya kijamii kuhusu ugonjwa huu iliwatatiza wanajamii na kuwapelekea kuibua majina tofauti ili kuashiria maradhi haya kutokana na vile yalivyomaliza na kuwadhalilisha wanajamii. Sitiari kadhaa zilitumiwa na bado zinatumiwa kuurejelea hususan, ‘kudungwa na mwiba’, ‘mnyama hatari’, ‘funza’ miongoni mwa sitiari nyingine (Kinara, 2012). Kwa kutumia sitiari hizi, ujumbe kuhusu athari ya ugonjwa huu unawafikia hadhira kwa njia yenye nguvu kuliko kutumia lugha ya kawaida. Hii ni kwa sababu sitiari zina uwezo wa kuibusha taswira zenye nguvu ambazo zina mnato mkubwa wa kuweza kubadili maoni, msimamo, mielekeo, falsafa na ufasiri wa jambo fulani.

Katika jamii ya Wakamba, maradhi haya yamepewa jina la kimajazi *muthelo* kama vile mshororo wa 5 katika wimbo wa *Katulilangi* unavyoshadidia. *Muthelo* ni istilahi inayotumiwa na jamii ya Wakamba kuashiria siku za mwisho hapa duniani. Katika Biblia, kitabu cha Matayo mlango wa 24 kifungu cha 7 kinafunza kuhusiana na ishara za siku za mwisho hapa duniani ikiwemo ishara ya kuchipuka kwa magonjwa yasiyo na tiba. Ukimwi kwa wanajamii ya Wakamba ni moja ya magonjwa yasiyo na tiba yaliyotabiriwa katika biblia. Hivyo, Wakamba wameupachika jina hilo la *muthelo* kuashiria kwamba, binadamu anaishi katika siku zake za mwisho.

Kwa mujibu wa nadharia ya Uamali (Levinson,1983), lugha inayotumika katika kazi ya sanaa ili kuleta mawasiliano yanayokusudiwa ni muhimu . Katika wimbo huu, ni muhimu

kuelewa lugha husika ili kung'amua matumizi ya maneno ya kimajazi kuashiria ukimwi. Kwa mfano *nenomuthelo* (mshororo wa 5) linalomaanisha kumaliza watu wengi. Vilevile, wimbo huu umetumia tamathali ya takriri ili kusisitiza hoja husika. Msisitizo wa neno *waminwa* (ukimalizwa) na *ngautula muti* (nitakulaumu) katika kila mshororo unaibua uzito wa kuwatahadharisha vijana dhidi ya ugonjwa wa ukimwi, ambao unaambukizwa kupitia ngono za kiholela.

Wimbo wa *Sengeze ni nzuku* (Mchezo ni mbaya, Na.18) ni wimbo mwingine ambao unaimbwa katika jando za kisasa ili kuwatahadharisha watahiriwa na wanajamii wenginekuhusiana na ugonjwa wa Ukimwi. Mishororo hii inashadidia hoja hii:

<i>Sengeze ni nzuku</i>	Mchezo ni mbaya
<i>Munyamu ni Ukimwi</i>	Jinamizi ni Ukimwi
<i>Witwa ngusye mbola</i>	Unaitwa mvuta polepole
<i>Syana sya aka kunai ngua</i>	Wasichana shikilieni nguo
<i>Aume namo mavinde kithoko</i>	Wanaume nao wasuke kamba

Wimbo huu unatilia mkazo maendeleo na mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za jando za jamii ya Wakamba inayobadilika. Wimbo huu unatumia mbinu ya tasfida kwa sababu ya hadhira changamano katika sherehe za jando. Kutokana na mabadiliko ya maisha kiwakati, lugha ya utusani iliyosheheni nyimbo za jando katika kipindi cha kabla ya ukoloni haitumiwi tena. Msanii anatumia neno '*sengeze*' kuelezea kitendo cha ngono. Huenda kitendo hicho kingetajwa kwa jina lake halisi bila kuficha katika nyimbo za kipindi cha kwanza cha utafiti. Lugha fiche hii inaakisi kubadilika katika jamii.

Kadhalika, ugonjwa wa ukimwi umepewa jina la kimajazi '*mvutapolepole*'(mshororo wa 3)kuashiria ugonjwa unaomgofua mtu na kumuua polepole. Aidha, msanii

ametumia lugha ya kimapumbo katika maneno ‘kushikilia nguo’(mshororo wa 4) kwa wasichana akiwa na maana kuwa, wanapaswa kujiambaa kabisa na tendo la ngono mpata waolewe. ‘Kusuka kamba’(mshororo wa 5) kwa wavulana ina maana kuwa, hawapaswi kuwa na wapenzi wengi. Wanapaswa kuwa na mmoja. Msanii anawatahadhalisha vijana wajiepushe na ngono za kiholela kwani huweza kupelekea mhusika kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi.

Matumizi ya mbinu ya tasfida yanaashiria mabadiliko ya jamii ambapo lugha chafu haitumiwi tena katika nyimbo za kisasa. Mabadiliko haya yamesababishwa na kuchukua dini ya kikristo. Kutumia lugha ya utusani ni mojawapo ya tabia hasi ambazo dini ya kikristo inakashifu. Aidha, msanii anatumia lugha ya mafumbo hususan, mshororo wa 4 na 5 ili kusisitiza umuhimu wa kutoshiriki ngono kiholela. Matumizi ya taswira pia yametumiwa na msanii kuibua picha ya mgonjwa wa ukimwi ambaye amedhoofika kiafya polepole katika mshororo wa 3 unaoupa ugonjwa huu jina la kimajazi *ngusye mbola*(mvuta polepole.)

Ili kuelewa maana ya wimbo huu, msikilizaji anapaswa kuelewa muktadha wake. Hymes (1974) akieleza utendakazi wa nadharia ya ethnografia ya mawasiliano anashikilia kuwa, sharti uelewe muktadha wa maneno na tukio fulani ili maana yake ieleweke. Ni kupitia muktadha wa jando ambapo wimbo huo utaeleweka kwani umetumia mbinu za lugha kama majazi mfano, mshororo wa *3ngusye mbola* (mvuta polepole), na pia tasfida mfano *sengeze* mshororo wa 1 kuashiria ngono. Kutilia maanani utamaduni wa jamii husika ni muhimu ili kuelewa ujumbe unaokusudiwa katika nyimbo hizi. Wakamba walikuwa na

mila na desturi ya kupachika wanyama ama magonjwa hatari majina ya kimajazi ili yasisikie yakitajwa na kuwashika wanaoutaja. Ilikuwa mwiko kuwataja wanyama hatari kwa majina usiku kwa mfano nyoka alitwa *ulii*(uzi) usiku ili asijue kwamba ni yeye anatajwa. Ugonjwa wa ukoma ulijulikana kama *musungu*(weupe) usisikie na kuwavamia wanajamii. Ukimwi nao kutokana na utamaduni huu unaitwa *ngusye mbola*(mvuta polepole).

4.2.3 Ubaguzi wa Mwanamke

Suala la ubaguzi wa mwanamke linalojitokeza katika nyimbo za jando za Wakamba ni kiwakilishi cha mtazamo wa jamii hii kumhusu mwanamke. Taswira hasi ya mwanamke inayochorwa kupitia nyimbo za jando inajaribu kueleza mtazamo na itikadi ya jamii ya Wakamba kuhusu jinsia ya kike. Baadhi ya nyimbo za jando za kisasa katika jamii ya Wakamba zinamsawiri mwanamke wa kisasa kama kahaba, mlevi, mchawi na mgomvi. Mfano wa wimbo ambao unamsawiri mwanamke kama kahaba ni wimbo (Na.19)

Katulilangi kupitia sehemu ifuatayo;

Indi waminwa ni muthelo, ngautula muti Lakini ukimalizwa na Ukimwi, nitakulaumu
Waminwa ni Katulilangi, ngautula muti Ukimalizwa na *Katulilangi* , nitakulaumu.

Katulilangi kwa mujibu wa wimbo huu ni mwanamke wa kisasa, ambaye ana tabia ya kushiriki ngono na wanaume wengi. Kutokana na tabia yake ya ukware, analaumiwa kwamba yeye ndiye huambukiza wanaume ukimwi. Lengo la wimbo huu ni kuwaonya wanaume dhidi ya wanawake ambao hawana msimamo wa kuwa na mpenzi mmoja. Mshororo wa 2 usemao ‘ukimalizwa na *Katulilangi* nitakulaumu’, unashadidia hoja

hiyo.Kupitia wimbo huu,wanawake wanasawiriwa kama viruka njia ambao wana tabia ya kuwa na wapenzi wengi, tabia ambayo inawapelekea kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi. Kwa mujibu wa wimbo huu, mwanamke ni mwiba wa kutahadhari kwa sababu yeye ndiye huambukiza wanaume ukimwi licha ya kwamba, wanaume anaoshiriki ngono nao pia wanaweza kumuambukiza.

Ujumbe unaoenda sambamba na huu umekita katika wimbo Na.26 *nzonge na ileve*. Wimbo huupia unamsawiri mwanamke kama kahaba anayeshiriki ngono na wanaume kwa ajili ya pesa. Sehemu ifuatyo inashadidia hili;

<i>Ndukue ngili ya manyanga</i>	Beba elfu ya wasichana
<i>Ndukue ing'olo ya mutumba</i>	Beba shilingi tano za wanawake wazee

Wimbo huu unamsawiri mwanamke kama kahaba ambaye anashawishiwa kushiriki ngono kulingana na kiwango cha pesa alichonacho mwanaume. Uchumi wa pesa na hali ya kutaka kujikimu ni vitu ambavyo vimekuwa na athari kubwa katika jamii. Mshororo wa 1 na wa 2 kama ilivyonukuliwa inatilia mkazo hoja kwamba, pesa zimeharibu utaratibu wa maisha ya jamii. Baadhi ya wanawake wamepoteza mwelekeo kwani wamekuwa wachuuzi wa miili yao. Elfu moja katika mshororo wa 1 inasimamia pesa nyingi, ilhali shilingi tano katika mshororo wa 2 zinasimamia kiwango kidogo cha pesa. Pesa zimevuruga maadili ya kijamii jambo ambalo huwakera watunzi wa nyimbo za jando za Wakamba. Kupitia kero hii, wanatunga nyimbo kushutumu tabia za aina hii. Msanii wa wimbo huu anapitisha ujumbe kwa watahiriwa na wanaume wengine kwamba, wanawake wa kisasa wanashiriki ngono ili wafaidike kifedha. Lengo la wimbo huu ni

kuwatahadharisha wanaume katika jamii ya Wakamba dhidi ya baadhi ya wanamke wa kisasa ambao hawana mapenzi kwa mwanaume. Mapenzi yao yamo kwa pesa.

Mifumo ya kiuchumi ya kikoloni iliwafanya Waafrika kushindwa kukimu na kukidhi mahitaji yao na ya familia zao (Masinde,2003). Hii ndiyo sababu baadhi ya wasichana wanashawishiwa kuuza miili yao ili wapate pesa. Pia, ndicho chanzo cha taasubi za kiume ambapo wanaume wanawachukulia wanawake kama vifaa vya kuwastarehesha, mradi wametoa pesa. Jambo hili linamulika uhalisia wa maisha katika jamii ya kisasa na linaonyesha kuwa maadili hayatiliwi maanani tena. Ubinafsi na kule kujali pesa ni sifa ambazo zimevunjilia mbali utu na maisha ya ujima.

Nao wimbo Na. 29 (Mjomba wetu amefura) unamsawiri mwanamke kama mgomvi na anayesababisha matatizo katika ndoa. Sehemu ifuatayo ya wimbo ‘mjomba wetu amefura’ inaonyesha ugomvi wa mwanamke;

<i>Inaume witu nimwimbu</i>	Mjomba wetu amefura
<i>Muka Kasivu nake nimwimbu</i>	Kasivu naye amefura
<i>Kasivu ni ke ke ke ndakilasya</i>	Kasivu ni ‘ke ke ke’ hanyamazi
<i>Kisomo kya Mungelesa nikiyatuvuthisye</i>	Elimu ya Mwingereza imetudhalilisha
<i>Kiveti nikiyonwe ngovi</i>	Mwanamke achapwe makofi

Wimbo huu unamsawiri mwanamke kama mgomvi na aliye na tabia ya kumchapa mumewe. Mshororo wa 1 unasema ‘mjomba wetu amefura’ kuonyesha kwamba, kufura kwake kulisababishwa na vita baina yake na mkewe Kasivu. Kupitia mshororo wa 3, msanii anatomia mbinu ya takriri ‘ke ke ke’ ili kupitisha ujumbe kuwa, Kasivu anaongea sana na tabia hii ndiyo inayozua ugomvi baina yake na mumewe. Kupitia tabia hiyo, anachapwa mpaka anafura kama vile mshororo wa 2 unavyosema ‘mkewe kasivu naye

amefura'. Kwa mujibu wa wimbo huu, mwanamke anasawiriwa kama mgomvi kutokana na sababu kwamba ni msomi (Mshororo wa 7). Msanii analenga kupitisha ujumbe kwamba, masomo ya kimagharibi yanamfurisha kichwa mwanamke asiwe na heshima kwa mumewe na kutokana na sababu hiyo, hata ndoa husambaratika. Katika muktadha wa wimbo huu, mwanamke anabaguliwa kwa sababu ugomvi huwa kati ya watu wawili si mtu mmoja. Vilevile, suala la ubaguzi wa mwanamke linajitokeza kupitia mshororo wa 8 ambapo msanii anapendekeza kwamba, mwanamke anapaswa kuchapwa.

Wimbo huu utaeleweka vyema kupitia kuelewa utamaduni wa jadi wa Wakamba. Katika jamii ya jadi ya Wakamba, mwanamke alipaswa kumwonyesha heshima mumewe kiasi kwamba, hata wakati wa mumewe amemkosea heshima, alipaswa kutumia mavyaa wake kuongea na mumewe ili kusuluhisha matatizo baina yao (Watuma, 2001). Mtunzi wa wimbo huu alikuwa na lengo la kukashifu hasira za mwanamke. Kulingana naye, hasira ni hasara. Hasira hupelekea watu kutenda mambo yasiyo na mwelekeo. Msanii anaelekea kuwatahadharisha wanawake kuwa, ni heri kunyamaza kuliko kutoa tamko kwa hasira kama anavyofanya Kasivu kwa sababu husababisha ugomvi katika ndoa.

Kwa upande mwingine, wimbo (Na. 27) 'Mtoto wa binamu' unambagua mwanamke kwa kumsawiri kama mchawi na mlevi kupitia sehemu ya wimbo huu ifuatayo;

<i>Nikilya noosa musaala mwisu wa mwei</i>	Nikichukua mshahara mwisho wa mwezi
<i>Aimbonethya tuthi tukakunde twiili</i>	Ananiambia twende tukanywe mbili
<i>Navindukie neethia Mbulwa e muthei</i>	Niliamka nikampata Mbulwa akiwa uchi
<i>Aithyululuka ngua syakwa ailuma ta simba</i>	Akizunguka nguo zangu akinguruma ja simba

Kupitia wimbo huu, msanii anamchora mwanamke kama mlevi. Mshororo wa 2 unasema ‘ananiambia twende tukanywe mbili’. Aidha, unamchora mwanamke kama mchawi. Mshororo wa 3 na wa 4 unasema ‘ niliamka nikampata Mbulwa akiwa uchi, akizunguka nguo zangu akinguruma kama simba’. Kwa mujibu wa wimbo huu, hii ni tabia ya kichawi.

Msanii anaonyesha mtazamo walionao wanajamii ya Wakamba kuhusu mwanamke katika jamii ya kisasa. Hapaswi kushiriki vileo lakini mwanamume anaruhusiwa. Huu ni ubaguzi wa mwanamke kupitia kunyimwa uhuru wa kutenda atakalo katika ulimwengu huru. Kupitia wimbo huu, watahiriwa wanafunzwa wachukue mda kuwajua na kuwafahamu wanawake kabla ya ndoa kama ilivyokuwa katika jamii jadi ya Wakamba. Wanafahamishwa umuhimu wa kuoia mwanamke mwenye tabia zinazokubalika katika jamii yao kama, mwanamke ambaye anatoka katika familia nzuri na isiyo ya wachawi. Aidha, mwanamke katika jamii hii hapaswi kuwa mlevi na anapaswa kuwapenda wakwe zake. *Mbulwa* amesawiriwa kinyume na sifa hizi hivyo basi, wavulana wanaonywa wajiambae na wasichana kama yeye.

4.2.4 Ushirikiano wa Kijamii

Maudhui ya ushirikiano wa kijamii yanapatikana katika kipindi cha kabla na baada ya ukoloni. Hii ni kwa sababu jamii ya Wakamba inaafiki ukweli wa methali ‘umoja ni nguvu utengano ni udhaifu’(Mbiti, 1969). Jamii ya Wakamba iliishi kwa ushirika na umoja kabla ya majilio ya wakoloni. Mbiti (aliyetajwa) anatilia uzito utamaduni wa

Wakamba wa kushirikiana anapoeleza kwamba, katika jamii hii, kila mtu aliishi kwa ajili ya mwingine. Ushirika huu uliwapa wanajamii mshikamano ambao uliwawezesha kukabiliana na baadhi ya matatizo kama jamii moja. Kupitia desturi hii, nyimbo za jando za kisasa hutungwa ili kuwahimiza wanajamii waendeleze ushirikiano wa kijamii. Mfano wa nyimbo ambazo zinahimiza msikamano huu ni kama wimbo wa *Muvuviwa ndili* (Mpuliza baragumu, Na. 21) kupitia mishororo ifuatayo:

<i>Muvuvi wa ndiliii</i>	Mpuliza baragumu ii
<i>Niwavuva ndili tweeyumilya</i>	Umepuliza baragumu tukajitokeza
<i>Twivoya ngwatanio Ukamba</i>	Twaomba ushirika Ukambani
<i>Twivoya Akamba makwatane mbau</i>	Twaomba Wakamba washirikiane

Wimbo huu unasheheni maudhui ya ushirikiano wa wanajamii. Mtahiriwa anaambiwa katika mshororo wa 2 *niwavuva ndili tweeyumilya* (umepuliza baragumu tukajitokeza). Kupuliza baragumu ni kujitangaza kwamba yuko tayari kutahiriwa. Kila mwanajamii alitarajiwa kuhudhuria sherehe hii kwa sababu ilikuwa ya jamii nzima. Jamii ya jadi ya Wakamba ilihimiza umoja ambapo, kila mwanajamii alitegemea mwingine katika utendakazi. Shughuli kama kilimo hususan upanzi wa mimea, kupalilia, kuwinda ndege, kuvuna miongoni mwa shughuli nyingine zilifanywa kwa ushirikiano.

Sherehe za kijamii mathalan kukaribisha mtoto, tohara, harusi, na mazishi zilikuwa za kila mwanajamii. Historia hii inauwekea msingi wimbo huu wa jando ambao unaimbwa katika jamii ya Wakamba ya kisasa. Lengo la wimbo huu ni kuisitiza kwamba, wanajamii wanatarajiwa kuishi pamoja kwa ushirika kama vile jamii ya jadi ya Wakamba ilivyoishi. Maneno ‘Kushikana mbavu’ katika mshororo wa 4 yametumiwa

kitamathali. Kushikana mbavu kwa mujibu wa wimbo huu ni kushirikiana. Ni ishara ya kuishi pamoja kwa kutegemeana.

Katika muktadha wa jando, Watahiriwa wanaimbiwa wimbo huu ili kuwahimiza kuwa na ushirikiano wanapoanza maisha yao mapya. Kutokana na mabadiliko ya kijamii yanayosababishwa na elimu ya kisasa, dini ya kikristo na mbinu mpya za uzalishaji mali, maisha ya wanajamii yamebadilika ambapo wengi wamehamia mijini kutafuta riziki. Maudhui haya ya ushirikiano yanaonyesha uhalisi wa maisha katika jamii ya Wakamba. Kulingana nao, jifya moja haliinjiki chungu, hivyo basi, fasihi simulizi yao zikiwemo nyimbo za jando zinawarai wanajamii washirikiane pamoja katika kila hafla ya kijamii.

Wimbo wa *Muti ukuema makuli* (Mti unaowashinda nyani, Na.22) pia unathibitisha kuwa, kwa jamii ya Wakamba, ushirikiano ni suala la kimsingi. Mishororo ifuatayo inaeleza hoja hiyo:

<i>Ethiwa ndukwenda kutwika muoi</i>	Ikiwa hutaki kuwa mrogi
<i>Mituki wiyunge naitu</i>	Fanya haraka ujiunge nasi.

Wimbo huu uliimbwa wakati wa kilele cha sherehe ya jando. Una maudhui ya kuwasuta wanajamii wasiojiunga na wengine katika sherehe muhimu za kijamii kama hii. Kujitenga kwa baadhi ya wanajamii na sherehe za kijamii kama ya jando kunatokana na wanajamii ambao wamekengeushwa na utamaduni wa kimagharibi. Kulingana nao, tamaduni za Wakamba zimepitwa na wakati na hazina nafasi katika ulimwengu unaobadilika. Kundi hili la wapinzani ndilo hukashifiwa katika wimbo huu.

Wanatahadharishwa kuwa iwapo hawataki kuonekana kama mahasimu wa jamii ‘wachawi’, wajiunge na wanajamii wengine katika mshororo wa 2. Jamii ya Wakamba ina imani ya ushirikina. Wanaamini kwamba, kuna wanajamii ambao ni wachawi na kutokana na sifa hiyo, hawapendi kushirikiana na wengine wasije wakatajiwa uchawi wao. Katika muktadha wa jando, mwanajamii aliyejulikana kuwa na tabia inayoenda kinyume na matakwa ya jamii hususan mchawi alitajwa, na kosa lake likatajwa na aila yake ikakashifiwa hadharani.

Maudhui ya ushirikiano vilevile yalijitokeza bayana katika wimbo wa *Kusyaaniwa kwimuyo* (Furaha ya kuwa na aila, Na.23). Mishororo ifuatayo inashadidia umuhimu wa ushirikiano kwa watahiriwa na wanajamii:

<i>Vai kindu ki muyo ta kusyaaniwa</i>	Hakuna kitu kitamu kama kuwa na aila
<i>Onaetha wingya</i>	Hata kama wewe ni maskini
<i>Ndukekala wi weka</i>	Hautakuwa mkiwa
<i>Ekai kuthinya Ngai, ndakolwe nithyi</i>	Tusimsumbue Mungu asitusahau

Wimbo huu una maudhui changamano. Kwanza, vijana watahiriwa pamoja na wanajamii wanahimizwa washirikiane kama ndugu. Kuwa na ushirikiano kunaleta amani katika jamii. Wanajamii wakiishi kwa ushirika husaidia maskini kama vile mshororo wa 2 unavyobainisha (Hata kama wewe ni maskini). Mshororo wa 3 una maana kuwa, ushirikiano unaondoa ukiwa kutokana na sababu kwamba, kila mwanajamii hutangamana na wengine kwa hivyo hawezi kuwa mpweke. Vilevile, msanii anawahimiza washirikiane kwani ushirika humfurahisha Mungu kama vile mshororo wa 4 unavyoshadidia ‘tusimsumbue Mungu asije akatusahau’. Wakamba waliamini Mungu

hupendezwa na watu kuishi kwa amani na ushirikiano ndiposa wakampa jina *Mwai wa nguthu*(Mungu wa wengi).

4.2.5 Ushoga na Ndoa za Jinsia Moja

Baadhi ya nyimbo katika kipindi cha baada ya ukoloni zinawaelimisha watahiriwa kuhusu umuhimu wa maadili, ambayo jamii inawatarajia kushikilia. Baadhi ya nyimbo zimetungwa ili kuwamulikia vijana wa kiume na wa kike kuhusu masuala ibuka mathalan tabia za ushoga na ndoa za jinsia moja. Itakumbukwa kwamba, katika jamii ya jadi ya Wakamba, mvulana alichaguliwa mke na baba ama mjomba. Vijana kote duniani sasa wana utamaduni wao ambao Brake (1980) anaueleza kama ‘ulimwengu huru’ wa vijana ulio na mitindo na njia za maisha ambazo, vijana hufuata ili kujitofautisha na utamaduni wa wazazi wao. Utamaduni wa vijana kwa kiasi kikubwa ni zao la maendeleo katika jamii za ulimwengu.

Maadamu kadri jamii inavyosonga mbele kimaendeleo, ndivyo ambavyo utamaduni wa vijana unakuzwa, unaimarishwa na kusambazwa miongoni mwa vijana kote duniani. Vijana wamebuni utamaduni wao kama njia moja ya kuasi dhidi ya utamaduni uliotawaliwa na wazee. Wanataka kujihusisha na tabia kama matumizi ya dawa za kulevya, ushoga, uasi wa maadili ya kijamii, mitindo mipya ya mavazi, muziki miongoni mwa tabia nyingine ambazo wanajua huwatenga wazee.

Kulingana na Kaplan (1989), hili ni jaribio la vijana kupania kuonyesha nguvu na uwezo wao wa kijamii. Ujumbe wanaopitisha ni kuwa hawako tayari kushiriki utamaduni

unaowadhibiti na kuwanyima nafasi yao katika jamii. Ili kuwaonya vijana kuhusiana na tabia ya ushoga, nyimbo za jando zimetungwa kukashifu tendo hili. Wimbo wa *Kiwanza kila kinai Kamuvalu* (Uwanja uliokuwa *Kamuvalu*, Na.24) ni mfano mzuri. Mishororo ya wimbo huu inayosisitiza hoja hii ni kama ifuatayo:

Kiwanza kila kinai Kamuvalu
Mwikuyuniwakindana na Mukamba
Ko nzau ikindanaa na ingi?

Uwanja uliokuwa Kamuvalu
Mkikuyu amefanya ngono na Mkamba
Kwani dume hushiriki ngono na mwingine

Wimbo huu huimbwa katika jando za kisasa ukiwa na lengo la kuwahamasisha watahiriwa kuhusu athari za mabadiliko ya maisha. Ulitungwa ili kuwatahadharisha vijana kujiambaa na ubasha. Msanii wa wimbo huu anaonyesha kuajabia kitendo hiki kama vile mshororo wa 3 unavyouliza, ‘kwani dume hufanya ngono na mwingine’? Msanii anatumia maswali ya balagha ili kuisisitiza na kuchochea hisia na ari kuhusu suala la ubasha. Katika utamaduni asili wa Kiafrika, tabia kama hii haikuwepo na kama ilikuwepo, ilifanyika kwa siri kali. Hii ni kwa sababu tabia yoyote ambayo ilienda kinyume na maadili ya kijamii ilikashifiwa.

Katika jamii ya Wakamba, mwanamume alitarajiwa kuoia mwanamke ili wazae watoto wa kuendeleza ukoo wake na jamii nzima kwa jumla. Wimbo huukiwanza *kila kinai Kamuvalu* umetumia tamathali ya tashbihi kwa kuwalinganisha wanaume na fahalikatika mshororo wa 3 (kwani fahali hushiriki ngono na mwingine?). Fahali ana jukumu la kuzalisha mtamba lakini fahali na mwingine hawawezi kuzalisha. Kitendo cha fahali akijihusisha ngono na fahali mwingine ni cha ajabu mno. Msanii anauliza swali hili la balagha, kuonyesha hisia zake za mchomo na mshangao ili kuisisitiza kwamba, hakuna uwezekano wa fahali kutenda tendo la ngono na fahali mwingine.

Tabia ya ushoga ina historia ndefu. Kulingana na imani ya dini ya kikristo, mashoga walikuwepo katika miji ya Sodomu na Gommorah. Kitabu cha Mwanzo 19:5 kinaeleza kuhusu mabasha waliofika nyumbani kwa Lutu usiku wakitaka kuwalawiti wageni wake ambao walikuwa malaika wa Mungu. Ushoga ni desturi ya kigeni katika jamii ya Kiafrika. Katika Bara la Afrika, tabia ya ushoga inachukuliwa kama mwiko na ambayo inaenda kinyume na maadili ya Kiafrika (UN 2005). Tabia ya ushoga kwa mujibu wa Kaplan (1989) na Brake (1980) inahusishwa pakubwa na kundi la vijana ambao hushiriki misingi sawa kote duniani. Brake (1980) anaeleza kuwa, tabia ya ushoga baina ya vijana husimilishwa, hufikiwa na kusambazwa kupitia teknohama. Njia za teknohama kama huduma za mtandao, setilaiti, runinga na redio hutumika kuzalisha tamaduni mpya za vijana zinazojikita katika muziki, filamu, mavazi na mitindo ya maisha pamoja na bidhaa wanazotumia.

Nchini Kenya, tabia ya ushoga imeripotiwa baina ya vijana katika shule za mabweni. Vilevile, walio katika ndoa wameripotiwa kujihusisha katika ushoga nje ya ndoa zao (UN 2005). Nchini Kenya, shirika la “The Gay and Lesbian Coalition of Kenya” liliundwa mwaka wa 2001 ili kupinga na kukashifu vitendo vya ushoga (Kau, 2008). Shirika hili liliundwa kuwaelimisha wanajamii hasa vijana kuhusiana na athari za ushoga kama uambukizwaji wa magonjwa ya zinaa ukiwemo ugonjwa wa ukimwi. Aidha, utafiti kupitia shirika hili ulionyesha kuwa, mashoga hupata ugonjwa wa kiakili na wengi huwawendawazimu (UN 2005). Vijana wanatarajiwa kujitenga nacho kwani baada ya jando, jamii inawakubalia kuo na kupata watoto watakaoundeleza jamii. Kuo na kuzaa watoto ni jambo la kimsingi katika jamii ya Wakamba, ndiposa kila mwanamke na

mwanaume waliohitimu umri wa kuo wa waliruhusiwa kufanya hivyo ili waweze kuendeleza ukoo wao.

Kwa mujibu wimbo huu (Na .24), kuporomoka kwa maadili ya vizazi vya kisasa kuna uhusiano mkubwa na kutupiliwa mbali kwa baadhi ya mila na tamaduni zilizotilia mkazo suala la maadili. Kulingana na wimbo huu, tabia ya mwanamume kutenda tendo la usenge na mwingine haikuwepo katika jamii ya jadi ya Mkamba aliyejulikana kama *Mukamba wa w'o* ama *Mukamba kivindyo*(Mkamba halisi).

Kwa mujibu wa nadharia ya Uamali, lugha yoyote ile huweza kueleweka tu katika miktadha ya kijamii. Hali kadhalika matumizi yake katika mawasiliano huzingatiwa kwa namna ambavyo huathiri kitendo au vitendo fulani. Nadharia hii ilisadifu katika kuchambua nyimbo za jando za Wakamba kwa sababu, mengi yaliyoshughulikiwa na nyimbo hizi ni mafumbo na huweza kufasiriwa vilivyo iwapo jamii lugha pamoja na mazingira yake yatazingatiwa. Neno 'fahali' katika muktadha wa wimbo huu limetumiwa kumaanisha mwanaume. Maana yake itaeleweka kupitia muktadha na tukio la jando. Vilevile, neno Mkikuyu limetumiwa kumaanisha majirani wote wa Wakamba ambao walikuwa na uhasama nao kupitia vita vya kuviziana.

4.2.6 Umuhimu wa Upangaji Uzazi

Jamii ya Wakamba ya kisasa inawahimiza vijana kuhusu upangaji uzazi ili kupata watoto wanaoweza kuwakimu. Nyimbo zinazohusiana na upangaji uzazi zinatokana na mabadiliko ya kijamii yaliyoletwa na elimu mpya ya kigeni ambayo ni ghali mno

pamoja na njia mpya za uzalishaji mali. Kutokana na ugumu wa maisha, vijana wa leo wanahimizwa kupitia nyimbo zikiwemo za jando wapange uzazi ili wapate watoto wanaoweza kuwakimu vizuri. Miongoni mwa nyimbo zinazosheheni maudhui ya umuhimu wa kupanga uzazi ni wimbo *Makato mwiitu wa Masimba* (Makato msichana wa Masimba, Na. 36) kupitia sehemu ifuatayo:

Makato mwiitu wa Masimba
Vundisya muika kuumba
Onakwa ngesila Tawa
Ngitonywa ndawa ya kuumba

Makato msichana wa Masimba
Fundisha vijana kupanga uzazi
Hata mimi nilipitia Tawa
Nikadungwa dawa ya kupanga uzazi

Wimbo huu uliimbwa ukiwa na lengo la kupitisha ujumbe kwa watahiriwa na vijana wengine kwamba, dunia ya leo imebadilika na wanahitajika kupata watoto ambao wanaweza kuwakimu kimaisha. Msanii kupitia mshororo wa 2 anasema kwamba, vijana wafunzwe kupanga uzazi. Anasema kupitia mshororo wa 3 na wa 4 kwamba, hata yeye alipitia Tawa (taz. Kiambatisho 1) akadungwa dawa ya kupanga uzazi. Suala la upangaji uzazi ni ibuka. Halikuwepo katika nyimbo za kabla ya ukoloni kutokana na sababu kwamba, gharama ya maisha haikuwa ghali kama ya leo. Watoto hawakuwa wakipelekwa shuleni na kulipiwa karo kama katika jamii ya sasa. Vilevile, njia za uzalishaji mali ambazo zinawalazimu baadhi ya wanajamii kuhamia mijini kutafuta riziki hazikuwepo. Wakamba walikuwa wakitegemea mashamba, ususi wa vikapu, uchongaji na usasi miongoni mwa njia nyingine ili kukimu familia zao. Mabadiliko ya maisha yaliyoletwa na wakoloni yamechangia kubadilika kwa nyimbo za jando katika jamii ya kisasa ya Wakamba ili kusawiri uhalisia wa maisha katika jamii hii inayobadilika.

4.2.7 Kulalamikia Mabadiliko katika Majukumu ya Kiuana

Baada ya majilio ya wakoloni, utamaduni wa Mwafrika uliathirika. Mabadiliko ya utamaduni yalianza baada ya elimu, dini na utamaduni wa kimagharibi kupenya katika maeneo ya Ukambani katika miaka ya 1890 na 1900 (Kimilu, 1962; Musyoka, 2012). Wamishionari walianza kuhubiri dhidi ya mila, desturi na utamaduni wa Mwafrika kwa jumla. Mila kuhusu majukumu ya kiuana ikaanza kupata athari hii kutokana na athari za uchumi wa pesa uliobadilisha njia za uzalishaji mali. Wanajamii wasomi waliohama kijijini na kuenda kuishi katika miji mikuu kutokana na sababu za kikazi ndio walioathirika zaidi na utamaduni wa kigeni.

Kutokana na athari za utamaduni wa kimagharibi, baadhi ya Wakamba walikengeushwa na kutengwa na jamii yao ya jadi ambayo ilikuwa na mipaka kuhusu majukumu ya wanaume na wanawake. Kutokana natabia ya mwanamume kuanza kutekeleza majukumu ya kike, wasanii nao wamelivalia suala hili njuga na kutunga nyimbo zinazoonyesha madhara yaliyoletwa na ukoloni. Aidha, wanatunga kukashifu wanaoenda kinyume na utamaduni wao wa jadi kuhusu majukumu ya kiuana. Wimbowa *Ninoonie kindu kyanzenya* (Niliyoyaona yalinishangaza, Na.25) ni mfano mzuri wa kashifa hii kupitia sehemu ya wimbo huu ifuatayo:

Ninoonie kindu kyanzenya
Mungelesa aetie kiumo nduani
Aume nimavulaniilwe
Masyokie ikoni
Masyokie usini
Indo ikaithwa nuu?

Niliyoyaona yalinishangaza
Mwingereza ameleta laana kijijini
Wanaume wamechanganyikiwa
Wamerudi jikoni
Wamerudi mtoni
Mifugo watachungwa na nani?

Wimbo huu uliimbwa kwa toni ya kejeli. Ni wimbo ambao unakashifu na kusimanga utamaduni wa Mwingereza ambao hauna mipaka kati ya majukumu ya kiuana, na ambao baadhi ya wanaume hasa wasomi wamekengeushwa nao. Katika mshororo wa 2, msanii anasema ‘Mwingereza ameleta laana kijijini.’ Laana kwa mujibu wa wimbo huu ni kutelekeza utamaduni wa Wakamba na kupapia utamaduni wa kigeni. Kulingana na wimbo huu, wanaume wameanza kutelekeza majukumu ya kike kama vile mshororo wa 3 na wa 4 unavyoshikilia, ‘wanaenda jikoni na mtoni’. Kulingana na msanii, kuenda jikoni na mtoni kuna maana ya kupika na kuchota maji, majukumu ambayo yalitengewa mwanamke katika jamii ya jadi ya Wakamba. Lengo la wimbo huu ni kukashifu utamaduni wa kimagharibi, ambao umetoa mipaka kati ya mwanamke na mwanamume kupitia majukumu wanayotarajiwa kutelekeza na jamii. Unasimanga wanaume ambao wamebadilishana majukumu yao na mwanamke.

Katika jamii za Kiafrika, kuna uhusiano mkubwa wa uana na majukumu ambayo binadamu hutengewa na jamii. Umuhimu wa kila jinsia kutelekeza majukumu yao unampelekea msanii kuuliza swali la balagha ‘mifugo watachungwa na nani?’ (Mshororo wa 6), iwapo wavulana wamegeukia majukumu ya kike. Kulingana na wimbo huu, kupapia utamaduni wa wazungu kunawadhalilisha wanaume wa Kiafrika kwa kuwakengeusha kiasi cha kutelekeza majukumu ambayo yametengewa wanawake. Msanii wa wimbo huu anaona tabia ya mwanaume kutelekeza majukumu ya kike kama jambo la ajabu. Ndiposa anasema *ninoonie kindu kyanzenya* ‘niliyoyaona yalinishangaza’ katika mshororo wa 1.

Kimilu (1962) anaeleza kuwa; katika jamii ya jadi ya Wakamba, *Mukamba wa w'o*(Mkambahalisi) ni yule aliyefuata mila na utamaduni wa jamii yake. Mwanamume halisi katika jamii hii alitengewa majukumu mahususi hususan, kuchunga mifugo, kuilinda jamii, kuikimu familia yake miongoni mwa mengine. Wanawake nao walitengewa majukumu kama kuzaa, kuwalea watoto, kuwapikia, kuchota maji, kutafuta kuni, kulima kupalilia, kuvuna mazao miongoni mwa majukumu mengine. Wimbo huu unawarai watahiriwa washike mila na tamaduni zao ili waondoe laana kijijini.

Ili kuuelewa ujumbe unaokusudiwa katika wimbo huu, hatuna budi kumrejelea Saville-Troike (1982) anaposema ni vizuri kuelewa aina ya ujumbe unaokusudiwa hasa kwa kuzingatia utamaduni unaofuatwa na wanajamii husika. Kuelewa utamaduni wa Wakamba kuhusiana na suala nzima la uana ni muhimu ili hadhira lengwa waweze kuwasiliana vilivyo na msanii. Wimbo huu unasawiri uhalisi wa mambo katika jamii ya kisasa ya Wakamba ambapo, kutokana na athari zilizoletwa na njia mpya za uzalishaji mali, na elimu ya kimagharibi inayohubiri usawa wa kiuana, majukumu ya kiuana hayana mipaka tena. Wanaume hutekeleza majukumu ya wanawake na wanawake nao hutekeleza majukumu ya wanaume.

Wimbo mwingine ambaounakashifu utamaduni wa Mwingereza katika jamii ya Wakamba ni wimbo wa *Inaume witu nimwimbu* (Mjomba wetu amefura, Na.29), kupitia mishororo ifuatayo:

<i>Inaume witu aimbite ndakumanyika</i>	Mjomba wetu amefura hajulikani
<i>Muka Kasivu nake nimwimbu</i>	Mkewe Kasivu naye amefura
<i>Akomete ndeyukilya</i>	Amelala hajiwezi
<i>Kisomo kya Mungelesa nikyativuthisye</i>	Elimu ya Mwingereza inatudunisha
<i>Kiveti nikonwe ngovi, aliilimwa!</i>	Mwanamke azambwe makofi,

Wimbo huu ulitungwa kumdhahiki Mzungu kwa kuubomoa utamaduni wa jamii ya Wakamba. Kwa mujibu wa wimbo huu, mjomba na mkewe wote wamefura (mshororo wa 2 na 3). Kufura kwao kumetokana na kupigana. Wimbo huu uliimbwa ukiwa na lengo la kubainisha kuwa, mwanamke hapaswi kupigana na mwanaume. Kupigana na mwanaume ni athari ya kukengeuka kwa wanawake kutokana na elimu ya kimagharibi, inayohubiri usawa wa kiuana (Kobia, 2008). Mshororo wa 4 unasema *Kisomo kya mungelesa nikyativuthisye* (elimu ya Mwingereza imetudunisha) kumaanisha kuwa, Mzungu analaumiwa kwa kuleta elimu iliyowakengeusha wanawake wajione kwamba, wako sawa na wanaume kupitia masomo. Kwa mujibu wa wimbo huu, mwanamke anapaswa kuchapwa, hapaswi kupigana na mwanaume kulingana na mshororo wa 5 usemao *kiveti nikonwengovi* (mwanamke azabwe makofi).

Ni bayana kuwa ili kupata maana inayokusudiwa na wimbo huu (Na. 29), ni sharti utamaduni wa Wakamba uzingatiwe. Nafasi ya mwanamke katika jamii ya Wakamba ni muhimu katika kuufahamu wimbo huu. Zaidi ya hayo, machukulio ya mke sharti

yazingatiwe pia katika muktadha wa jamii ya Wakamba. Ni baada ya kufahamu hayo ndipo wimbo huo huweza kuchukuliwa kama chombo cha mawasiliano.

4.2.8 Athariza Uchumiwa Pesa

Mabadiliko kimaudhui ya nyimbo za jando za jamii ya Wakamba pia yalithibitishwa na nyimbo ambazo ziliwaonya watahiriwa kuhusu athari ya uchumi wa pesa katika maisha ya kisasa. Ukolonikwakiwango kikubwa ulikengeusha jamii za Kiafrika kwa kuleta uchumi wa pesa na kazi za kuajiriwa. Kuzuka kwa miji kulipelekea vijana kuhamia mijini kutafuta kazi jambo ambalo liliathiri mielekeo na mitazamo yao ya kimaisha (Ngoyani, 2006). Kutokana na mabadiliko haya, mahusiano ya kimapenzi yakaegemezwa kwa upande wa pesa. Maudhui ya umuhimu wa pesa katika mapenzi yamesisitizwa katika wimbo *Nzonge naileve* (Nicheze ileve, Na.26) kupitia sehemu hii:

Ndukue ngili ya manyanga
Ndukue ing'olo ya mutumba

Ukiwa na elfu ni ya wasichana
Ukiwa na shilingi tano ni za mama mzee.

Wimbo huu unaimbwa katika jando za kisasa. Unasheheni maudhui ya mapenzi ya siku hizi ambayo yanaelekea kuwa ya kununuliwa kwa pesa. Kupitia mshororo wa 1 na wa 2, msanii anasema kuwa ukitaka 'manyanga' (msichana) ni lazima uwe na pesa nyingi, *ngili* (elfu moja) lakini ukiwa huna pesa, una *ing'olo*, (shilingi tano) utapata mwanamke mzee (*mutumba*). Suala hili la kubidhaaisha mapenzi linabainisha mabadiliko kimaudhui ya nyimbo za jando kulingana na mabadiliko ya kijamii. Awali, katika jamii ya Wakamba kabla ya majilio ya wakoloni, vijana walikuwa wakitafutiwa wake (King'ei, 1982). Mwanamume hakuoa kutokana na mapenzi. Aliozwa mwanamke kutokana na

sababu nyinyi ikiwemo ile ya msichana aliyezaliwa katika familia isiyo ya wachawi na aliye na maadili yanayotamanika (Nzioki, 1982).

Siku hizi kutokana na mabadiliko ya maisha na kukengeuka kwa wanajamii kutokana na utamaduni wa kimagharibi, vijana huasi utamaduni wao na hutenda vitendo kwa hiari. Hujitafutia wake na kwa kiwango kikubwa bila kuwahusisha wazazi. Kulingana na wimbo huu, aliye na pesa humpata msichana mrembo (manyanga) na asiye nazohuangukia mwanamke ambaye ametumika (mtumba). Akirejelea mabadiliko ya vijana, Kau (2008) anasema kuwa, katika kipindi cha ujana, tunatarajia kuona mabadiliko ya mitazamo mbalimbali ya kimaisha. Kulingana na Kau (aliyetajwa), vijana hukengeushwa na kuathiriwa na tamaduni mbalimbali wanazokumbana nazo kupitia mitandao mbalimbali. Kuathiriwa huku huzua maarifa, ubunifu na upenyefu wa fikra miongoni mwa vijana. Mabadiliko yanayosababishwa na upenyefu huu wa fikra miongoni mwa vijana huwapelekea baadhi ya wanajamii kuwaona vijana kama waasi wa maadili ya jamii. Nyingi ya nyimbo za jando hutungwaili kuwamulikia vijana athari wanazokumbana nazo katika maisha kutokana na uhuru wao, wa kujichagulia wachumba tofauti na ilivyokuwa katika jamii ya jadi ya Wakamba.

Ni bayana kuwa ili kupata maana sadifu inayokusudiwa na wimbo huu, ni sharti utamaduni wa Wakamba uzingatiwe. Utamaduni wa kuchagulia wavulana wake ni muhimu katika kufahamu wimbo huu. Vilevile, matumizi ya lugha ya vijana katika maneno *Ing'olo* (shilingi tano) na *mutumba* (kuashiria uzee) yanaibua umuhimu wa hadhira lengwa ya vijana katika kupitisha mawasiliano yanayokusudiwa. Kwa ujumla,

wimbo huu unanuia kuadilisha vijana. Watahiriwa wanatayarishwa kwa maisha yaliyojaa vishawishi na changamoto tele kama ulazima wa kuwa na pesa ili kujipatia mpenzi. Kutokana na maendeleo na mabadiliko ya kijamii, suala la mapenzi yasiyo ya dhati linatiliwa mkazo katika nyimbo za jando za kisasa.

4.2.9 Matatizo katika Ndoa za Kisasa

Suala la ndoa ni kipengele kinachotambuliwa duniani kote kama suala nyeti lenye kuathiri maendeleo ya kijamii (Mbiti, 1991). Suala la matatizo katika ndoa za kisasa limewavutia wasomi katika nyanja mbalimbali kama vile dini, historia, saikolojia, isimujamii, filofia na fasihi (Simiyu, 2007). Wasanii wa nyimbo za jando za Wakamba wamelivalia suala la ndoa junga kwa mfano kupitia wimbo *Mbulwa* (Mbulwa, Na.27). Wimbo huu unawatahadharisha wavulana dhidi ya kuchagua wanawake wasiowajua mienendo yao vizuri kupitia sehemu ifuatayo:

*Mwana wa mwendya niki wambikisye iko
motoni Uimbonania na Mbulwa mwiitu wi
aliye na Mavenzi movungu
Nikilya noosa musaala mwisowa mwai
mwezi Aimbonethya tuthi tukakunde twiili
ndyinukaa niona ta wanendeie*

Binamu kwa nini ulinitupa
Ukanionyesha Mbulwa msichana
Mapenzi ya uongo
Nikichukua pesa mwishoni mwa
Ananiambia twende tukanywe mbili
Kwetu siendi nafikiria ameniendea

Katika wimbo huu, msanii anasema mwanamke aliyejulishwa kwake aitwaye *Mbulwa* ana mapenzi ya uongo kama vile mshororo wa 2 na 3 unavyodhibitisha; ‘Ukanionyesha *Mbulwa* msichana mwenye mapenzi ya uongo’ (*Uimbonanyia na Mbulwa mwiitu wi mavenzi movungu*). Licha ya kuwa na mapenzi ya uongo, *Mbulwa* anasawiriwa kama mlevi katika mshororo wa 2. Anasema ‘kila mwisho wa mwezi anamwambia waende wakanywe mbili’. Hii ni tabia nyingine ambayo inamfanya mhusika kulalamikia tabia ya

mkewe Mbulwa. Vilevile, Mbulwa ni mchawi. Haya yanabainishwa kupitia sehemu ifuatayo ya wimbo huu:

Navindukie neethia mbulwa e muthei Niliamka nikamkuta akiwa uchi
Aithyululuka ngua syakwa ailuma ta simba Akizunguka nguo zangu akinguruma kama
simba

Kulingana na msanii wa wimbo huu, tabia ya Mbulwa ya kuvua nguo usiku na kumzunguka mumewe akinguruma kama simba ni ya kichawi. Uchawi ni miongoni mwa imani ambazo zimekita mizizi katika jamii ya Wakamba. Jamii hii iliamini kwamba, kuna wanajamii ambao ni wachawi na huwadhuru wengine kwa kuwaroga. Miongoni mwa athari za uchawi ni mtu kuzugwa akili mpaka anasahau majukumu yake ya kimsingi kama kuwakimu wazazi na jamaa zake. Anarogwa kiasi kwamba, havezi kuwasaidia kwa vyovyote vile. Katika wimbo huu, mhusika anasema haendi kwao na anafikiria *Mbulwa* ‘alimuendea’ katika mshororo wa 6. Neno ‘kumuendea’ limetumiwa kimafulmba katika wimbo huu. Lina maana ya kurogwa. Matumizi ya maneno kulingana na muktadha ili kuibua mawasiliano yanayotarajiwa kunaungwa mkono na Hymes (1974) anaposema kuwa, ili kuelewa maana ya misemo na utaratibu wa kuongea, ni lazima swala la muktadha lizingatiwe.

Wimbo huu uliimbwa ukiwa na lengo la kukashifu unafiki wa wanawake walio katika ndoa na ambao wana tabia za Mbulwa. Dhima moja kuu ambayo hutekelezwa nanyimbo za jando ni ile ya kuwakashifu wanaoenda kinyume na maadili ya kijamii. Katika jamii ya jadi ya Wakamba, msichana akivunja ungo alikuwa anapitishwa katika unyago ili kuashiria kwamba, amevuka kutoka awamu ya utotoni hadi utu uzima. Sherehe ya unyago ilikuwa muhimu katika jamii ya Wakamba kwa sababu, licha ya msichana

kupewa hadhi mpya yenye matarajio, matakwa na majukumu mapya baada ya kutahiriwa, alipitishwa kwenye mafunzo makali kuhusiana na mambo ya unyumba na namna ya kumtunza mume. Mafunzo haya yalitolewa na kungwi baada ya unyago. Msichana aliyetahiriwa aliheshimiwa na wavulana na alichukuliwa kuwa mwanamke mwenye staha katika jamii. Kutokana na mafunzo hayo, wasichana waliaminika kuwa wamepata maadili na watakuwa wake wazuri. Kwa upande mwingine, wavulana wakipitia tambiko la jando nao walipitishwa kwenye mafunzo kuhusu ndoa, majukumu ya kiuana pamoja na mambo kuhusu unyumba.

Mafunzo hayo yalitolewa na wasimamizi wao wanaojulikana kama *avwikii* wakiwa katika jando kubwa. Mvulanaakitaka kuoja kama vile tulivyobainisha hapo mbeleni, alimjulisha babake ama mjomba ambao walikuwa wametwikwa jukumu la kutafutia mwanao mke. Msichana mzuri iliaminiwa ni yule aliyetahiriwa na anatoka katika jamii yenye maadili isiyo ya wachawi. Kila mwanajamii alijulikana tabia na hulka yake na wanajamii wengine kutokana na wanajamii kushirikiana pamoja kwa kila hafla kiasi kwamba, waliokuwa na tabia hasi hususan wachawi na wezi walijulikana na kutengwa na wanajamii.

Wimbo huu huimbwa katika jando za kisasa ukiwa na lengo la kuwatahadharisha vijana dhidi ya akina *Mbulwa*. Katika muktadha wa wimbo huu, *Mbulwa* ni taswira ambayo inawakilisha wanawake wote wa kisasa ambao wameasi mila na tamaduni zao kutokana na kukengeushwa na tamaduni za kigeni. Unawamulikia wavulana kuhusu hatari ya kuoja wanawake wasiowafahamu vyema, kwani huenda wakawa wachawi na wenye tabia hasi

kamakushiriki vileo miongoni mwa nyingine. Mwanamke kulingana na utamaduni wa Wakamba anapaswa kushikilia majukumu yake ya kiuana hususan kuzaa, kulea watoto, na kumtunza mumewe miongoni mwa majukumu mengine. Hapaswi kuenda kwa vilabu kushiriki vileo kama wanaume.

Msanii ametumia mbinu ya istiari kulinganisha *Mbulwa* na moto. Katika mshororo wa 1, msanii anasema ‘binamu kwa nini ulinitupa motoni?’ Kuoia *Mbulwa* kwa mujibu wa wimbo huu ni sawa na kumtumbukiza mhusika katika moto. Maisha yake yamekuwa na shida nyingi kupitia ndoa hii. Aidha, msanii anatuchorea taswira ya *Mbulwa* akiwa uchi usiku, akizunguka nguo za mumewe huku akiguruma kama simba. Taswira hii imetumiwa katika wimbo huu ili kuibua uzito wa matatizo aliyonayo mhusika kwa kuishi na mchawi.

Nyimbo za jando za kisasa pia husawiri suala la ugomvi katika ndoa. Ugomvi katika ndoa za kisasa limekuwa nyeti katika ulimwengu wa leo. Wasanii wa nyimbo za jando za Wakamba nao wamelivalia junga ili kusheheni falsafa, imani na mtazamo wa jamii ya Wakamba kuhusiana nalo. Ili kupitisha ujumbe unaokusudiwa kuhusu ugomvi katika ndoa, wimbo wa *Inaume witu ni mwimbu* (Mjomba wetu amefura Na.29), kupitia mishororo ifuatayo ni mfano mzuri :

Inaume witu aimbite ndakumanyika
Muka Kasivu nake nimwimbu
Akomete ndeyukilya
Kasivu ni ke ke ke, ndakilasya
Utuku ni kumbulukumbulu

Mjomba wetu amefura hajulikani
Mkewe Kasivu naye amefura
Amelala hajiwezi
Kasivu ni ke ke ke, hanyamazi
Usiku ni ‘kumbulukumbulu’

Ugomvi ni mvurugano unaotokea baina ya watu kwa kutoelewana. Katika wimbo huu, Kasivu anasawiriwa kama mwanamke ambaye ni mpyoro. Ana tabia ya kumtukana mumewe kila mara. Mshororo wa 4 ‘Kasivu ni ke ke ke hanyamazi’ unathibitisha hilo. Tanakali ya usemi ‘ke ke ke’ imetumiwa na msanii kumithilisha kelele za Kasivu na sauti inayotolewa na cherahani wakati wa kushona nguo. Cherahani hutoa sauti hii ke ke ke kwa mfululizo bila kunyamaza. Kujibizana huku ni baadhi ya sababu ambazo zinasababisha mvurugano katika ndoa. Kutokana na tabia yake ya kumtusi mumewe, Kasivu alichapwa mpaka akafura na kuumizwa. Mshororo wa 3 unaosema ‘amelala hajiwezi’ unashadidia hilo. Vilevile, msanii wa wimbo huu anatumia tanakali ya sauti katika mshororo wa 5 *kumbulukumbulu* kuibua taswira ya uzito wa mvuruganouliopo baina ya Kasivu na mumewe.

Mwanamke katika jamii ya jadi ya Wakamba alipaswa kumyenyekea mumewe kwa vyovyote vile. Alikuwa amekatazwa kujibizana na wanaume na iwapo atakosewa na mumewe, imani za kijamii hazikumkubali kukabiliana na mumewe moja kwa moja. Alipaswa kutumia mavya au marika wa mumewe ambao, huwa na haki ya kumwadhibu kwa niaba ya mumewe. Vilevile, mwanamke katika jamii ya Wakamba hatarajiwi kuonyesha ujasiri ama uwezo wowote au nguvu za kukabiliana na mumewe. Anapaswa kuonyesha unyenyekevu, uvumilivu, subira na utiifu kwa wanaume wote (King’ei, 1982; Nzioki, 1982). Katika uhakiki wake wa *Utenzi wa Mwanakupona*, Momanyi (1998) anaunga mkono kauli hii anaposisitiza kuwa, mwanamke wa Kiafrika alishauriwa na jamii awe na nidhamu katika lugha yake. Alihitajika kunyamaza mbele ya mwanamume hata kama ametukanwa. Licha ya kusawiri mvurugano katika ndoa za kisasa, wimbo huu

huimbwa kukashifu wanawake kama Kasivu ambao wanawashambulia waume zao. Aidha, msanii anatahadharisha watahiriwa na wavulana wengine wawe makini katika kuchagua wake wasije wakachagua akina Kasivu.

4.2.10 Shutuma dhidi ya Tohara za Hospitalini

Kupashwa tohara kwa vijana katika mila na utamaduni wa Wakamba ilikuwa ndiyo nyenzo moja muhimu iliyotumiwa kurithisha au kupitisha maarifa mbalimbali miongoni mwa wanajamii. Haikuruhusiwa kushiriki ngono kati ya mvulana na msichana kabla ya sherehe hii. Isitoshe, mvulana ambaye hakuwa ametahiri hakutakiwa kurithi mali ya babake. Kufuatia umuhimu uliopewa tambiko hili la jando, mvulana anayetoroka na kutahiriwa hospitalini hukejeliwa. Husutwa kwa kuambiwa kuwa, daima hatakuwa mtu mzima. Atakufa bado akiwa mtoto. Familia yake pia hutwa lawamani kupitia nyimbo za jando kwa kumpeleka mtoto wao kutahiriwa hospitalini. Wimbo wa *Kusyulwa kikonde* (Kubambuliwa ngozi, Na.30) unasisitiza hoja hii kupitia mishororo ifuatayo:

<i>Ninoonie Usenyu</i>	Niliona maajabu
<i>Kivisi kya Mwalimu</i>	Mtoto wa mwalimu
<i>Kyaikiwe sivitali</i>	Alipelekwa hospitalini
<i>Kuu ti kwaikwa</i>	Huku si kutahiriwa
<i>No ta kusyulwa kikonde</i>	Ni kama kubambuliwa ngozi
<i>Ta muti wa muuku</i>	Kama mti wa <i>muuku</i>

Lengo kuu la wimbo huu lilikuwa kuwakejeli vijana waliotahiriwa hospitalini, na ambao hawapati mafunzo yanayopitishwa kwa watahiriwa jandoni. Uliyonesha mwelekeo wa wanajamii kuhusiana na jando za kisasa za hospitalini. Katika wimbo huu, tohara za hospitalini zinamithilishwa na kubambua mti maganda kama vile mishororo wa 4 na

5unavyodhibitisha *Kuu ti kwaikwa ,no takusyulwa kikonde* (huku si kutahiriwa, ni kama kubambuliwa ngozi). Mbinu ya tashibihi imetumiwa kumithilisha kutahiriwa hospitalini na kubambua ngozi ya mti kwa sababu, sehemu muhimu ya mafunzo ya jandoni haipo katika tohara za hospitalini.

Matumizi ya tashibihi yanaibua maudhui ya umuhimu wa jando za jadi zikilinganishwa na za kisasa za hospitalini. Kulingana na wimbo huu, kutahiriwa hospitalini ni kitendo cha kuajabisha kama vile mshororo wa 2 unavyobainisha, *ninoonie usenyo* (niliona maajabu). Wanajamii ambao ni wasomi ndiowanaowapeleka watoto wao hospitalini kutahiriwa kama vile mshororo wa 3 unavyosema *kivisi kya mwalimu* (mtoto wa mwalimu). Katika muktadha wa wimbo huu, neno ‘mwalimu’ linasimamia wasomi wote ambao wamekengeukakutokana na utamaduni wa jando za kiasili. Wimbo huu uliimbwa ili kukashifu wanaoenda kinyume na utamaduni wa Wakamba kuhusu jando za kiasili, na sherehe zinazondamana na jando hizo.

4.2.11 Nafasi ya Dini ya Kisasa katika Maisha ya Wanajamii

Maswalakuhusu dini ya kikristo katika nyimbo za jando za jamii ya Wakamba ni ibuka. Kwa kutaka kuonisha utamaduni wa jamii ya Wakamba na dini ya kikristo, nyimbo za dini zinaimbwa katika jando za kisasa na kuelekeza watahiriwa kuwa na imani katika dini hii. Baada ya majilio ya wakoloni, dini ya kikristo ilisambaa kwa kasi katika jamii ya Wakamba na mafundisho yake yakaanza kuhitilafiana na utamaduni wa jamii hii. Nyimbo za jando zikaanza kuonekana kama dhambi kwa sababu ya lugha

ambayo ilitumiwa (Wathome, 2009). Polepole, mkoloni akaanza kuwakengeusha Wakamba kwa kukataza nyimbo za kitamaduni, haswa nyimbo za jando na unyago. Kwa vile nyimbo hizi zilikuwa mhimili mkubwa kwa jamii hii kama kitambulisho chao, hazingeweza kupigika marufuku kabisa. Hivyo, Wakamba wakawa na mbinu nyingine za kuzigeuza ili ziziende kinyume na dini ya kikristo. Wakichelea kuonekana kama wanaenda kinyume na mafundisho ya kidini, watunzi wakazipa nyimbo hizi sura mpya. Zikaanza kusifia dini ya kikristo na kupitisha ujumbe kwa vijana na wanajamii wengine kuhusu umuhimu wa imani hii. Nyimbo za kidini katika muktadha wa jando ni ithibati kwamba, jamii ya Wakamba imebadilika na inaenda sambamba na mabadiliko ya kijamii hususan imani katika dini mpya ya Kikristo. Nyimbo za kidini katika muktadha wa jando hivyo basi ni kama kioo kinachoonyesha uhalisia wa maisha katika jamii ya Wakamba inayobadilika.

Ili kuthibitisha imani yao katika dini ya Kikristo, wimbo *Yesu ni ivia* (Yesu ni mwamba, Na.31) uliimbwa. Sehemu ifuatayo ya wimbo huu inasheheni imani ya wanajamii kuhusu imani yao kwa Mungu:

<i>Nuvoasya, Yesu nuvoasya</i>	Anaponya Yesu anaponya
<i>Nutusuviaa, Yesu nutusuviaa</i>	Anatujali, Yesu anatujali

Asili ya wimbo huu si Ukambani. Umeazimwa kutoka kwa dini ya kikristo (Wathome, 2009). Wimbo huu ulithibitisha kuwa, jamii ya Wakamba imeathiriwa na dini ya kikristo hata ingawa wanajamii bado wanashikilia baadhi ya tamaduni zao za kiasili. Wimbo wa *Yesu ni ivia* (Yesu ni mwamba) uliimbiwa watahiriwa baada ya tohara. Una maudhui ya kidini na unaashiria imani ya wanajamii kuhusu uwezo wa Mungu wa kumponya

mtahiriwa kidonda kilichosababishwa na kisu cha ngariba kama vile mshororo wa 1 unavyoashiria (anaponya, Yesu anaponya). Aidha, msanii wa wimbo huu anawahakikishia watahiriwa na wanajamii wengine kwamba, Yesu anawajali na anawalinda. Mshororo wa 2 unathibitisha hilo. Mbinu ya sitiari ilitumiwa na msanii kumlinganisha Yesu na daktari ili kuibua maudhui ya umuhimu wa dini ya kikristo kwa watahiriwa na wanajamii wengine. Wimbo huu ulitarajiwa kuwapa watahiriwa ujasiri na matumaini kwamba, Mungu, anawajali na atawaponya. Aidha, ulitarajiwa kuwajenga watahiriwa na wanajamii wengine kwa msingi mzuri wa kidini, wakimcha Mungu.

Wimbo wa *Usyao wa matuku aya* (kizazi cha siku hizi, Na. 32) uliimbwa mtafiti alipokuwa akihitimisha sherehe ya jando. Uliimbwa kama ombi kwa Mungu ili awabadilishe vijana mienendo yao; ambayokulingana na wimbo, imekuwa ya kuasi utaratibu wa kijamii. Imani ya wanajamii kuhusu uwezo wa Mungu katika kuadilisha vijana, inasawiriwa kupitia sehemu ya wimbo *Usyaowa matuku aya* (kizazi cha siku hizi, Na. 32) ifuatayo:

Mwaii ninguvoyea usyao wa matuku aya Mungu ninakiombea kizazi cha siku hizi
Nundu ninzyaityenye ngona nimuvinduku Kwa sababu nimeona kimebadilika.

Wimbo huu uliimbwa kwa toni ya kunyenyekea. Ulikuwa ombi kwa Mungu. Msanii anaombea kizazi kipyacha vijana *usyao wa matuku aya* (kizazi cha siku hizi) kulingana na mshororo wa 1 ambao, kwa mujibu wa wimbo huu, wamebadilika. Mshororo wa 2 unasema *nundu ni nzyaitye nye ngona nimuvinduku* (kwa sababu nimechunguza nikaona wamebadilika). Mienendo yao imekuwa kinyume na matakwa ya jamii. Wimbo huu unaonyesha imani waliyonayo wanajamii kuhusu uwezo wa Mungu katika kubadilisha

mienendo ya binadamu. Hatima ya vijana imekuwa ni kutenda yale yasiyosadifu na hivyo kupelekea baadhi yao kuondolewa katika kundi la jamii.

Kuanzia karne ya ishirini, suala la mabadiliko ya vijana limeangaliwa kama mabadiliko yanayotokana na mchanganyiko wa mawazo, na migogoro katika kuchanganya utamaduni na maendeleo. Tofauti za kimaadili zinajitokeza wakati taasisi za kijamii zinaposhindwa kumshikilia mwanajamii na kumwacha aingie katika dunia mpya yenye utamaduni tofauti (Kau, 2008). Kwa mujibu wa wimbo huu (Na.32), Mungu amesawiriwa kuwa na uwezo wa kuwabadilisha vijana kutokana na mienendo yao ya uasi. Mshororo wa 2 unasema ‘nimechunguza nikaona kimebadilika.’ Kutokana na mabadiliko ya kijamii, dini ya kikristo imechukua jukumu la kuwaelimisha vijana kuhusiana na mienendo inayokubalika na wanajamii.

Wimbo mwingine uliosheheni maudhui ya kidini ni wimbo wa *Ve musyi wonekaa* (Pana makoa yanayoonekana, Na.33). Wimbo huu unamulika imani ya Wakamba kuhusu maisha ya baada ya kifo kupitia mishororo ifuatayo:

<i>Ve musyi wonekaa</i>	Kuna makoa yanayoonekana
<i>Yiulu wa mwanda wa kikwu</i>	Ng’ambo ya pili ya mauti
<i>Na mathina maitonya kuweteka</i>	Huko hakuna taabu
<i>Kula sua yitathuaa na matu maivovaa</i>	Huko jua halitui na majani hayanyauki
<i>Musyi usu mwanake wa thaavu</i>	Mji huo unavutia wa dhahabu

Kwa mujibu wa wimbo huu, msanii analenga kupitisha ujumbe kwamba, hata ingawa binadamu anapitia maisha ya dhiki humu duniani, itatimia siku ambapo ataenda katika nchi nyingine ya ahadi, ambapo maisha yatakuwa mazuri kuliko wanayoishi sasa (mshororo wa 3, 4).

Wimbo huu uliimbwa kwa mahadhi ya kunyenyekea. Watahiriwa na wanajamii wanapata ujumbe kutoka kwa wimbo huu kwamba, walio na imani kwa Mungu, na wanaotenda kulingana na mapenzi yake, wataenda kuishi katika makao yaliyo mbinguni walioandaliwa na Mungu. Wimbo huu kupitia mshororo wa 1,2,4 na wa 5 unatoa taswira ya makao hayo. Taswira inayoibuliwa ya makao ya mbinguni ni ya mahali ambapo pana mwangaza wakati wowote kutokana na sababu kwamba, jua halitui. Mshororo wa 4 usemao 'kule jua halitui' ni thibitisho tosha. Vilevile, taswira ya makao hayo ya kijani kibichi inaibuliwa na mashororo wa 4 usemao, 'hata majani hayanyauki'. Wimbo huu ulikuwa na lengo la kuwapa wanajamii imani kwamba, hata ingawa wanapitia maisha magumu humu duniani, wataishi maisha mazuri mbinguni. Mshororo wa 3 usemao, *na mathina maitonya kuweteka* (huko hakuna taabu) unashadidia hilo.

Ili kuelewa mawasiliano kupitia wimbo huu, mazingira wanayoishi Wakamba sharti yazingatiwe. Wakamba kutoka sehemu ya utafiti wanaishi sehemu kavu. Wanajamii hukosa mahitaji ya kimsingi kama maji na chakula. Kutokana na maisha magumu wanaopitia, wana imani kwambaitakuja siku ambapo taabu zao zitafikia kikomo wakifika mbinguni.

Haya ni maudhui mapya katika nyimbo za jando za Wakamba za kisasa. Maudhui ya makao mapya ya mbinguni yalitokana na athari ya dini ya kikristo iliyoenezwa na wamishionari waliofika katika janibu za Ukambani kabla ya mwaka wa 1906 (Mbiti, 1969). Kulingana na Mbiti (aliyetajwa), kabla ya majilio ya wakoloni Wakamba waliamini kwamba, baada ya mtu kufa, roho yake iliachwa huru na iliishi mahali

ambapo mwanadamu wa kawaida hangefika. Kama mtu alikuwa mwovu, mathalan mchawi, roho yake haingetulia na ilikuwa inarandaranda ikiwatendea wanajamii maovu. Wale ambao walikuwa wema roho zao zilitulia na ndio walitumiwa na Wakamba kupitisha maombi yao kwa Mungu. Imani hii imebadilika kutokana na mabadiliko ya kijamii kupitia dini mpya ya Kikristo ambayo inashikilia kwamba, matendo ya mtu humu duniani ndiyo yatatumiwa na Mungu kuamua hatima yake baada ya kifo. Waliotenda mema hatima yao ni mbinguni makao ya Mungu, ilhali wenye dhambi makao yao ni motoni.

Imani kuhusu makao mapya baada ya kifo ni suala ibuka katika nyimbo za jando za Wakamba. Wasanii wa nyimbo za jando za kisasa wanatunga nyimbo zinazosawiri imani hii kama kielelezo cha hali halisi ya mambo katika maisha wa wanajamii. Nyimbo hizi zinatumiwa na Wakamba kama zana mojawapo ya kuleta matumaini ya maisha mazuri baada ya dhiki humu duniani.

4.3 Mabadiliko ya Maudhui ya Nyimbo za Jando za Wakamba kutoka Kipindi cha Kabla ya Ukoloni hadi Kipindi cha Baada ya Ukoloni

Baada ya kulinganisha na kulinganua maudhui ya nyimbo za jando za jamii ya Wakamba kupitia kipindi cha kabla na baada ya ukoloni, maudhui yalionekana kubadilika. Ifuatayo ni ithibati kwamba maudhui yamebadilika kulingana na mabadiliko ya kijamii.

Maudhui ya ujasiri wakati wa tohara yalipatikana katika nyimbo za jando za kipindi cha kabla ya ukoloni. Watahiriwa walitarajiwa kuonyesha ujasiri ili waweze kudhihirisha

kwamba, wako tayari kuulinda jamii na kutwikwa majukumu ya kiuana hususan, kuoana na kuikimu familia. Kabla ya majilio ya wakoloni, sherehe ya tohara katika jamii ya Wakamba ilikuwa kivuko muhimu kwa watahiriwa. Ni baada ya kupitia jando zote ambapo mtahiriwa alifunzwa siri za jamii yake, historia yao, namna ya kuulinda jamii pamoja na mila na tamaduni zinazofuatwa na jamii yake. Hivyo basi, suala la ujasiri lilikuwa la kimsingi wakati wa 'kukatwa' ili kudhihirisha kwamba, mtahiriwa alikuwa tayari kutwikwa majukumu aliyotarajiwa na jamii yake. Kwa mfano nyimbo (Na. 4, 6, 9, na 12) zinasisitiza umuhimu wa ujasiri wakati wa tohara.

Baada ya majilio ya wakoloni, maudhui ya ujasiri yakawa si ya kimsingi kutokana na sababu kwamba, jukumu la kuulinda jamii halikuwa tena jukumu la *nthele* (taz. Kiambatisho 1). Usalama ukaanza kutekelezwa na walinzi wa serikali. Viongozi katika jamii wakaanza kuchaguliwa na serikali. Badala la wazee wa *kisuka* na *kivalo* ambao walitwikwa jukumu la uongozi kabla ya ukoloni, kukawa na machifu na wadogo wao. Vilevile, kutokana na mabadiliko ya kijamii yaliyoletwa na mfumo mpya wa kielimu, na njia mpya za uzalishaji mali, wavulana wakaanza kutahiriwa wakiwa wadogo kuanzia umri wa miaka saba hadi kumi (Wathome, 2009). Hivyo basi, hawatarajiwi kuoana na kuanza jamii baada ya tohara. Wanatarajiwa kuendelea na masomo.

Hata hivyo, kwa vile fasihi simulizi ni mali ya jamii, nyimbo hizi ziliendelea kuimbwa kwa kusawiri mabadiliko ya jamii. Pindi tohara zilipoanza kutekelezwa hospitalini, basi nayo maudhui ya nyimbo hizi yakachukua mwelekeo mwingine. Badala ya kuwatia wavulana moyo wa ujasiri, zikawa zinawabeza waliotahiriwa hospitalini. Tohara za

hospitalini hazina uchungu kama tohara za jadi. Mtahiriwa hugandishwa govi kabla ya kutahiriwa. Kwa sababu mtahiriwa hahisi uchungu wakati wa kukatwa, hatarajiwi kuonyesha ujasiri. Wimbo (Na. 30) ni mfano mzuri wa nyimbo zinazowabeza watahiriwa waliopitia jando za hospitalini. Wimbo huu unamithilisha tohara za hospitalini na kubambuliwa ngozi ya mti. Haya ni mabadiliko ya maudhui yaliyoletwa na mabadiliko ya kijamii, yanayosisitiza tohara za hospitalini badala ya tohara za jadi.

Maudhui ya kuonya watahiriwa na wanajamii wengine dhidi ya tabia zisizokubalika katika jamii yalitawaliwa na itikadi na mila za jamii ya Wakamba. Jukumu la nyimbo za jando la kuonya watahiriwa na wanajamii wengine lilikuwa la kimsingi mno. Kwa mfano, watahiriwa walionywa dhidi ya kutongoza wanawake walioolewa kwa mfano wimbo (Na.2) *mwanake ndaneena na kivetu kyeene*. Vilevile, wanaume walitahadharishwa dhidi ya kutoroka na kutekeleza familia zao kwa mfano katika wimbo (Na. 14) *Ekuyu mesilile Mutha*.

Vilevile, mila na tamaduni za Wakamba hazikuruhusu wavulana ambao walikuwa hawajatahiriwa na kutiwa jandoni kushiriki ngono. Kutokana na mila hii, baadhi ya nyimbo zilizotungwa wakati wa sherehe ya tohara zilikuwa za kuwaonya watahiriwa kuhusu ngono za kwanza. Nyimbo za jando za kipindi cha kabla ya majilio ya wakoloni zilikuwa na ushauri ambao haungeweza kutolewa kwa kikao kingine chochote. Sherehe ya jando ilikuwa sehemu muhimu ya mapisi katika maisha ya vijana. Nyimbo zilizoimbwa kuhusu ngono zilijumuisha mafunzo ya kitamaduni ambayo hayangepitishwa katika muktadha mwingine.

Maudhui kuhusu suala la ngono limechukua mwelekeo mwingine katika kipindi cha pili cha utafiti. Badala ya nyimbo za jando kuwatahadharisha wavulana kuhusiana na ngono, kama vile wimbo (Na.5) unavyorai, vijana wanatahadharishwa kuhusiana na ngono za jinsia moja. (taz.wimbo Na. 24). Suala la vijana kujihusisha na tabia ya ushoga na ubasha limekuwa nyeti katika jamii ya sasa. Ili kuliangazia suala hili, nyimbo za jando zinatungwa ili kukashifu kitendo hicho ambacho ni kinyume cha mila na utamaduni wa Wakamba.

Maudhui kuhusu majukumu ya kiuana yalijitokeza katika nyimbo za jando za kabla ya ukoloni. Mfano ni wimbo (Na.13) *Mwaikwa niwalika ndiani*. Wimbo huu ulilenga kumpa mtahiriwa mawaidha ya maisha ya utu uzima na majukumu yanayomsubiri pasipo kuwategemea wazazi wake. Zawadi walizopewa baada ya jando zilitarajiwa kuanzisha maisha yao upya. Mifugo waliokabidhiwa na bidhaa nyingine kama nyute ni kiwakilishi cha kutengwa ili kuanzisha maisha ya utu uzima. Maudhui haya yamebadilika katika kipindi cha baada ya ukoloni. Nyimbo za jando za kisasa zinawamulikia vijana umuhimu wa elimu mpya ya kimagharibi, ili wabadilisha maisha yao ya baadaye. Wavulana wanatarajiwa kuendelea na masomo hata baada ya tohara kama vile wimbo Na. 28 unavyobainisha. Kwa mujibu wa wimbo huu, elimu hubadilisha maisha kwa sababu vijana wakisoma, wanapata kazi nzuri zenye mapato mazuri.

Aidha, maudhui kuhusu migogoro ya kijamii yalimulikwa katika nyimbo za jando za kabla ya majilio ya wakoloni. Katika jamii za Kiafrika, uhasama kati ya makabila na koo mbalimbali ulikuwepo mara kwa mara. Uhasama huu ulisababisha vita miongoni mwa

jamii mbalimbali. Jamii ya Wakamba sawa na jamii zingine ilipitia uadui na uhasama na makabila jirani kama Wakikuyu na Wamasai. Uhasama huu ulitokana na sababu za kutangamana wakifanya biashara ama wakilisha mifugo wao. Nyimbo zilizosawiri migogoro ya kijamii zilitungwa ili kuwaelimisha watahiriwa kuhusu migogoro hii na vilevile, kuwatayarisha kushiriki vita na kuikinga jamii iwapo vita vitatokea. Utafiti huu ulibainisha awali kwamba, kabla ya majilio ya wakoloni, jukumu moja muhimu la kuwatahiri na kuwatia wavulana jandoni lilikuwa kuwatayarisha ili kuikinga jamii kutokana na uvamizi wowote. Suala la migogoro ya kijamii halikumulikwa katika nyimbo za kipindi cha baada ya ukoloni kutokana na mabadiliko ya kijamii ambapo sasa, wanajamii hawatarajiwi kujihusisha na vita na makabila mengine kwani kufanya hivyo, ni kujichukulia sheria mikononi. Ni wajibu wa serikali kulinda wananchi wake. Aidha, watahiriwa katika jamii ya kisasa hawatarajiwi kuchukua jukumu la kuilinda jamii kama ilivyokuwa ada katika kipindi cha kabla ya ukoloni.

Vilevile, katika kipindi cha kwanza cha utafiti, baadhi ya nyimbo ziliimbwa ili kuwakumbusha wanajamii matukio muhimu ya kihistoria. Jukumu moja muhimu la nyimbo za jando za Wakamba ni kumulika na kuhifadhi matukio muhimu ya kijamii na kuyapitisha kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Wimbo Na. 18 na 28 ni mfano mzuri. Wimbo wenye maudhui ya vita vya pili vya dunia *Mundu ndakusaa Ngaiatanenda*(Na.18), uliimbwa kwa sababu ya kumbukumbu za Wakamba walioshiriki katika vita vya pili vya dunia Burma. Aidha, wimbo (Na. 28) *Syokimau* ni muhimu katika kupitisha historia ya jagina wa Wakamba kwa jina Syokimau. Nyimbo zinazobeba

historia kama hii ni muhimu kwani zinasaidia jamii kupokezana mila, historia, itikadi, utamaduni pamoja na mafunzo yenye maadili (Wamitila, 2003).

Maudhui kuhusu nafasi aliyotengewa mwanamke katika jamii ya Wakamba yalijitokeza katika kipindi cha kwanza cha utafiti. Mwanamke alisawiriwa kama mali ya kila mwanaume (shamba), asiyetumia mantiki katika kushiriki ngono na wavulana ambao hawajatahiriwa, kama bidhaa ya kuuzwa, kama kiumbe duni anayepaswa kuchapwa na mumewe miongoni mwa taswira nyingine hasi. Nyimbo Na.8 *Naamukawua naka*, Na.15 *Mwanakendaneena na kivetu kyeene* na Na. 17 *Miunda ni mali*, na 35 *Naangiwe muunda ni Syomasengela* ni mifanomizuri ya nyimbo zinazomsawiri mwanamke kwa njia hasi. Taswira zinazoimbuliwa na nyimbo hizi kuhusu mwanamke ni dumifu na ni kiwakilishi cha mahusiano ya kiuana katika jamii ya Wakamba ya jadi. Ziliakisi falsafa ya maisha ya ubabedume katika jamii hii. Kwa hivyo, nyimbo zilizochanganuliwa kuhusu taswira ya mwanamke kwa kiwango kikubwa ni makisio ya itikadi iliyotawala jamii hii kuhusiana na masuala ya kijinsia.

Taswira ya mwanamke katika jamii ya Wakamba imebadilika katika kipindi cha baada ya ukoloni. Kubadilika kwa taswira ya mwanamke katika jamii ya kisasa kumetokana na mabadiliko ya kijamii. Mabadiliko haya yanachangiwa na kuchipuka kwa magonjwa ya zinaa kama ukimwi yanayosababishwa na ngono za kiholela, elimu ya kigeni inayopigania usawa wa kijinsia, njia mpya za uzalishaji mali miongoni mwa matukio mengine ya kijamii. Mwanamke wa kisasa anasawiriwa kama mwimba wa kujidunga. Anaonekana kama kahaba ambaye anasambazia wanaume ugonjwa wa ukimwi. Kushiriki

ngono kiholela na mwanamke yeyote kunapigwa vita kupitia nyimbo za jando. Nyimbo za jando za kisasa zinawatahadharisha wanaume kuhusu kujihusisha na wanawake wengi wasije wakaambukizwa ugonjwa huu. Nyimbo Na.19 (Katulilangi) na 20(Sengeze ni mbaya) ni mifano ya nyimbo zinazotoa taswira ya mwanamke kama kahaba. Kutokana na mchipuko wa ugonjwa huu, wanawake sasa si mali ya kila mwanajamii kama vile wimbo (Na.17) ulivyoshadidia. Ni mwiba wa kutahadhari.

Uhalisia uliopo katika maisha ya leo ni kwamba, wanajamii wanapaswa kujitenga na ngono za kiholela ili kujiepusha na ukimwi. Ugonjwa wa ukimwi uligunduliwa hapa nchini Kenya miaka ya themanini. Kuanzia hapo mpaka leo, nyimbo nyingi katika jamii ya Wakamba zina ujumbe kuhusu ugonjwa huu kwa hadhira. Zinawaonya, kutahadharisha na kuwaelimisha kuhusu namna ya kujikinga kutokana na kuambukizwa ugonjwa huu usio na tiba.

Aidha, katika nyimbo za kabla ya ukoloni, mwanamke alisawiriwa kama kiumbe duni na dhaifu ambaye alichapwa na mumewe kama vile wimbo Na. 35 unavyobainisha. Taswira hii hasi ya mwanamke imebadilika katika nyimbo za jando za kipindi cha baada ya ukoloni ambapo mwanamke anamchapa mumewe panapotokea mtafaruku katika ndoa yao. Wimbo Na. 29 *inaume witu ni mwimbu* (mjomba wetu amefura) ni mfano mzuri. Mabadiliko haya ya maudhui kuhusu taswira ya mwanamke katika jamii ya Wakamba kabla na baada ya ukoloni ni ithibati kwamba, nyimbo za jando za Wakamba ni hai na zimebadilika maudhui kulingana na mabadiliko ya kijamii.

Mabadiliko ya maudhui pia yanaonyeshwa kupitia nyimbo ambazo zinatilia nguvu umuhimu wa elimu ya kimagharibi. Wimbo (Na. 28) *Syokimau* unamulika umuhimu wa elimu mpya ambayo hubadilisha maisha ya vijana na kuwaepusha na kazi za sulubu kama, kuwachimbia wengine mitaro maarufu kama *levu* katika jamii hii. Kazi ya kuchimba mitaro ina mapato finyu licha ya kuwa ni ngumu. Nyimbo za jando za kisasa zinatungwa ili kuwahimiza watahiriwa na vijana wengine kusoma ili wayabadilishe maisha yao kupitia elimu.

Vilevile, maudhui ya athari ya uchumi wa pesa katika mapenzi hayakuwepo katika nyimbo za jando za kabla ya ukoloni. Maudhui haya ni ibuka katika kipindi cha pili kusheheni mabadiliko ya nyimbo za jando kulingana na mabadiliko ya jamii. Mtindo wa kuzungumzia maswala ya mapenzi hadharani ni ibuka kwani haikuwa mila ya jamii ya Wakamba. Baada ya maingilio ya wakoloni, nyimbo za jando zilisheheni maudhui yaliyoathamini uchumi wa pesa katika mapenzi. Haya ni mabadiliko kutoka kipindi cha kabla ya ukoloni ambapo uchumi ulioathaminiwa ulikuwa ni ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda na mazao ya aina mbalimbali kutoka shambani. Baada ya maingilio ya wakoloni, uchumi wa pesa unatukuzwa na kuaminika kuchukua nafasi katika mahusiano ya kimapenzi. Hii ndio sababu nyimbo (Na. 26) *Nzonge na ileve* na (Na. 27) *Mavenzi mo vungu* zinasheheni maudhui haya. Lengo la msanii kutunga nyimbo zinazomulika mapenzi ya uongo ni kuwatahadhalisha vijana kuhusu mapenzi ya siku hizi.

Maudhui ya ushoga na ndoa za jinsia moja ni nyeti katika ulimwengu wa leo. Katika uhalisia wa maisha ya leo, suala hili halikwepeki. Dunia imebadilika na vijana

wamejipata katika njia panda kuhusiana na tamaduni mseto kupitia teknohama. Maisha yanayopendelewa na vijana ni yale ambayo huwapa uhuru wa kuishi maisha kwa tafakari zao wenyewe kwani; wakati hubadilika, na maisha vilevile. Wasanii wa nyimbo za jando za kisasa katika jamii ya Wakamba nao wamelivalia junga suala la ushoga na kutunga nyimbo ambazo zinakashifu na kukejeli tabia hii. Wimbo (Na. 24) *Kiwanza kila kinai Kamuvalu* ni mfano wa nyimbo zinazokashifu ushoga. Katika nyimbo za jando za kipindi cha kabla ya ukoloni, wasanii walitunga nyimbo zilizowaelekeza watahiriwa kuhusiana na ngono baina yao na wasichana waliotahiriwa. Mfano ni wimbo *ningukuna vilingi*(Nitapiga filimbi, Na. 1).

Maudhui kuhusu umuhimu wa ushirikiano katika jamii yamesawiriwa katika nyimbo za kipindi cha baada ya ukoloni mathalani nyimbo (Na. 21)*Muvuvi wa ndili*, (Na. 22)*Mutiukuema makuli*,na (Na. 23)*Kusyaaniwua kwi muyo*. Dini ya kikristo iliyoletwa na wamishionari katika janibu za Ukambani ilihubiri dhidi ya tamaduni kama za sherehe na nyimbo za jando, na kusababisha migawanyiko katika jamii (Kavyu, 1990). Aidha, njia za uzalishaji mali pamoja na elimu ya kisasa inawapelekea baadhi ya wanajamii kuhamia mijini na kuwatenga na wanajamii wenzao.Kutokana na sababu hizi na nyingine, nyimbo za jando za kisasa zinatungwa kuwarai wanajamii washirikiane kwa kila hafla ya kijamii ili kusawiri utamaduni asili wa Wakamba uliovurugwa na wakoloni.

Vilevile, suala la ndoa limemulikwa katika nyimbo za jando za kipindi cha pili cha utafiti. Ni swala ibuka ambalo limekuwa nyeti katika maisha ya kisasa ambapo, asasi ya ndoa imekumbwa na misukosuko mathalan ugomvi, vita, talaka na mauaji. Haya ni

mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za kisasa za jando za Wakamba. Suala la ugomvi katika ndoa halikumulikwa kupitia nyimbo za jando kabla ya majilio ya wakoloni. Utafiti huu ulibainisha awali kwamba, mwanamke alipoolewa, na kulipiwa mahari, alikuwa mali ya mumewe. Mume huyo alikuwa na uhuru wa kumwadhibu mkewe lakini wanawake hawakutarajiwa kupigana na waume zao kwa vyovyote vile. Walipaswa kunyamaza. Mfano wa nyimbo zinazosawiri mivurugano katika ndoa za kisasa ni wimbo (Na. 29) *Inaume witu ni mwimbu* na (Na. 29) *Mwana wa mwendya*. Kupitia nyimbo hizi, msanii analenga kuhamasisha wanaume kwamba, mwanamke wa kisasa ndiye chanzo cha mivurugano katika ndoa na wanapaswa kuchukua tahadhari wanapochagua wake.

Aidha, kashifa dhidi ya tohara za hospitalini ni swala ibuka. Baadhi ya wanajamii hasa wasomi huwapeleka wavulana wao hospitalini kutahiriwa. Haya ni mabadiliko kwani, nyimbo za jando za kabla ya ukoloni hazikusawiri maudhui haya. Kila mvulana alitahiriwa kwa kuzingatia mila na desturi za jamii ya Wakamba. Nyimbo (Na.25) *Mathisivitalina* (Na.30) *Ninoonie usenyozinakashifu* wanajamii wanaowapeleka wavulana wao kutahiriwa hospitalini. Tohara za hospitalini kama vile wimbo (Na. 30) unavyorai ni sawa na kubambuliwa maganda ya mti. Hazina manufaa yoyote kwa watahiriwa kutokana na sababu kwamba, mafunzo yaliyotiliwa maanani baada ya kutahiriwa hayapo katika jando za hospitalini. Lengo la mtunzi wa nyimbo hizi ni kukashifu na kuwakejeli wavulana waliotahiriwa hospitalini. Msanii anatumia kinaya kufananisha ndoa za hospitalini na kubabuliwa kwa ngozi la mti.

Pia, wimbo Na. 36 unaowarai vijana na wanajamii wengine kutumia njia za upangaji uzazi ni ibuka katika kipindi cha pili baada ya ukoloni. Maudhui kuhusu upangaji uzazi yametokana na mabadiliko ya kijamii yanayosababishwa na elimu ya kisasa, njia mpya za uzalishaji mali miongoni mwa mabadiliko mengine ya kijamii ambayo, yamesababisha maisha kuwa ghali. Ili kukabiliana na gharama ya maisha, wanajamii wanahimizwa kupata watoto wanaoweza kuwakimu.

Vilevile, nafasi ya dini katika maisha ya wanajamii yamebainishwa wazi katika baadhi ya nyimbo katika kipindi cha pili. Kadri maisha yanavyobadilika kutokana na hali za kidini, fasihi simulizi nayo imebadilika. Nyimbo za kisasa za jando zinatoa mwelekeo mpya ambapo maudhui sasa yamekuwa ni kumwabudu Mungu ili kuonyesha mwelekeo wa wanajamii hii kuhusu imani yao ya Kikristo. Utafiti huu umebainisha kuwa, Wakamba kabla ya majilio ya wakoloni walikuwa na dini. Waliamini kuwepo kwa Mungu mwenye uwezo mkubwa kupitia majina ya kimajazi waliompa. Wakamba walimpa Mungu nafasi kubwa katika maisha yao ya kila siku. Kabla ya kutekeleza lolote mathalani kula na kunywa, kinywaji na chakula kidogo kilimwagwa mchangani ili mizimu washiriki na kukibariki. Kabla ya kupanda, vifaa vya kilimo vilitolewa kafara ili Mungu avibariki, baada ya kuvuna, baadhi ya mazao yalipelekwa katika mahali pa maabadi maarufu kama *ithembo* na kuachiwa miungu. Kabla ya kwenda vitani, Wakamba walishiriki katika maombi ili kuombea ushindi vitani. Sherehe muhimu za kijamii nazo hususan, kuzaliwa kwa mtoto, tohara, harusi, mazishi miongoni mwa nyingine hazingefanywa kabla ya kutoa kafara. Baada ya majilio ya wakoloni, Wakamba

walipapia dini mpya ya kikristo na kupitia kwayo, baadhi ya nyimbo za jando za kisasa zinasawiri imani yao kuhusu uwezo wa Mungu katika maisha yao.

Katika kipindi cha baada ya ukoloni nyimbo za jando za Wakamba zimeanza kumulika suala la asasi ya dini ya Kikristo ili kuonyesha imani yao kuhusu uwezo wa Mungu katika jamii ya kisasa. Nyimbo (Na. 31) *Yesu ni ivia*, (Na.32) *Usyao wa matuku ayana* (Na. 33) *Ve musyi wonekaa* ni thibitisho kuhusiana na maudhui ya kidini katika nyimbo za kisasa za jando. Nyimbo hizi zinashadidia mabadiliko ya maudhui ya nyimbo za jando. Maudhui ya kidini ni ibuka katika nyimbo za jando za kisasa katika jamii ya Wakamba. Ni ithibati kwamba, jamii ya Wakamba inaenda sambamba na mabadiliko ya kijamii na wameshikilia dini ya Kikristo sawa na Waafrika wengine. Nyimbo zenye maudhui ya kidini zinashadidia kuwa, kwao, Mungu ana uwezo mkubwa wa kutibu, kuponya, analinda watu wake na baada ya maisha haya ya dhiki, Mungu huyo amewatayarishia wanaomtii makao bora ng'ambo ya pili baada ya mauti.

Kwa kuzingatia nadharia ya Ethnografia ya mawasiliano, utafiti huu umebainisha umuhimu wa muktadha, hadhira na utamaduni katika kuanisha lugha na matumizi yake katika nyimbo za jando za Wakamba. Vilevile, ya Uamali ilitumiwa katika kufafanua jinsi ambavyo maneno yametumiwa katika muktadha wa nyimbo za jando pamoja na viziada lugha ili kufaulisha mawasiliano yanayokusudiwa kupitia nyimbo za jando za Wakamba. Nadharia ya Uhalisia ilisadifu katika kubainisha kwamba, maudhui ya nyimbo za jando za jamii ya Wakamba yanabadilika kiwakati kulingana na mabadiliko ya kijamii. Kadri hali ya maisha inavyoendelea kubadilika kielimu, kiuchumi, kisiasa,

kijamii, kidini na takribani katika nyanja zote za maisha, nayo fasihi simulizi haswa nyimbo za jando zimechukua mwelekeo mpya ili kulandana na mabadiliko haya. Mabadiliko haya ya maudhui kiwakati yanayodhihirika katika nyimbo za jando za Wakamba yameelezwa kinadharia kwa kurejelea nadharia ya Uhalisia ambayo, huusawiri ulimwengu kama ulivyo wala siyo kama unavyofikiriwa kuwa.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

5.1 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza mabadiliko kimaudhui ya nyimbo za jando katika jamii ya Wakamba, kulingana na mabadiliko ya kijamii. Uchunguzi huu uliongozwa na nadharia za Ethnografia ya mawasiliano, Uamali na nadharia ya Uhalisia. Mihimili ya Ethnografia ya mawasiliano iliyoongoza utafiti huu ni muktadha, hadhira lengwa, lugha na mazingira. Ilibainika kwamba, mihimili hii ni vipengele vinavyozingatiwa na watunzi wa nyimbo za jando ili kuteua maudhui kwa mujibu wa wakati, ili nyimbo hizi ziweze kutekeleza wajibu wake ipasavyo. Mhimili wa nadharia ya Uamali kuhusu matumizi ya lugha na muktadha ulitusaidia kuchunguza uhusiano baina ya maneno, matumizi yake na fasili inayofanyiwa lugha husika kulingana na muktadha. Vilevile, nadharia ya Uhalisia kupitia mhimili wake unaosisitiza usanii wa matukio katika maisha ya kila siku ulitusaidia kuchanganua mabadiliko ya maudhui ya nyimbo za jando kwa mujibu wa wakati.

Katika juhudi za kushughulikia suala hili, tasnifu hii imegawika katika sura tano. Sura ya kwanza imefafanua usuli wa suala la utafiti. Aidha, sura hii imeangazia malengo na maswali yaliyoongoza utafiti pamoja na sababu zilizochochea uteuzi wa mada. Aidha, upeo na mipaka ya utafiti pamoja na nadharia zilizoongoza utafiti zimefafanuliwa.

Sura ya pili inahusu maandishina tafiti zinazohusiana na mada ya utafiti. Kupitia sura hii, historia na chimbuko la jamii ya Wakamba imefafanuliwa. Historia ya jamii ya Wakamba

ilitoa mwongozo wa kulinganisha maudhui ya nyimbo za jando katika vipindi tofauti vya kihistoria hadi leo. Aidha, itikadi, mila na desturi za Wakamba zimefafanuliwa katika sura hii, ikiwemo mila ya tohara ya jadi. Historia ya tohara ilikuwa muhimu kwani, iliwekea utafiti huu unaohusu nyimbo za jando msingi wa kugemea katika kuchunguza mabadiliko ya maudhui kwa mujibu wa wakati. Sehemu hii iliainisha tohara za jamii ya Wakamba. Ilibainika kuwa, zilikuwa za aina tatu. Kulikuwa na tohara ndogo, ambayo ilikuwa ya 'kukatwa' yaani; tohara halisi. Tohara kubwa nayo ilikuwa ya kutoa mafunzo na mawaidha kwa watahiriwa. Tohara ya kucheza ilikuwa na wajibu wa kuwafunza watahiriwa jukumu muhimu la kuilinda jamii kutokana na uvamizi wowote kutoka kwa maadui zao. Tohara hizi tatu zilikuwa na dhima kubwa katika jamii ya Wakamba hususan kuelimisha vijana kuhusiana na majukumu ya kiuana, maswala ya ndoa, siri na historia ya jamii miongoni mwa masuala mengine.

Kadhalika, kazi mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti huu zilihakikiwa katika sura hii. Kupitia uhakiki wa kazi hizi, ilibainika kuwa tafiti tangulizi zilizoshughulikia nyimbo za tohara zimejikita katika uhakiki wa maudhui, mtindo na lugha kama mada mahususi. Hakukuwa na utafiti uliozingatia mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za jando za Wakambaukiwa na nia ya kubainisha kuwa, maudhui ya nyimbo hizo hubadilika kulingana na mabadiliko ya kijamii. Hivyo basi, kazi hii ilifidia pengo hilo.

Sura ya tatu nayo ilianguzia mbinu za utafiti zilizotumiwa katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Aidha, ilianguzia sababu za kuchaguliwa kwa sehemu ya utafiti pamoja na kubainisha nyenzo na vifaa vilivyotumiwa katika ukusanyaji wa data.

Sura ya nne ilichanganua nyimbo za jando katika kipindi cha kabla na baada ya ukoloni. Katika kufanya hivi, nyimbo katika kila kipindi zilihakikiwa kulingana na malengo ya utafiti. Nyimbo za jando katika kipindi cha kabla na baada ya ukoloni ziliandikwa kwa lugha asili ya Kikamba, na kisha kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza iwapo maudhui ya nyimbo za jando katika jamii ya Wakamba yamebadilika, kulingana na mabadiliko ya kijamii. Baada ya kuchunguza nyimbo katika vipindi viwili ya utafiti, ilibainika kuwamaudhui yamebadilika. Mabadiliko haya husababishwa na mabadiliko ya kijamii kupitia matukio mahususi mathalan, elimu ya kisasa, dini ya kikristo, uchumi wa pesa, njia mpya za uzalishaji mali miongoni mwa matukio mengine ya kijamii.

Sura ya tano ni hitimisho, muhtasari wa tasnifu, matokeo na mapendekezo ya utafiti. Muhtasari wa kila sura umetolewa pamoja na masuala muhimu yaliyoibuka katika mijadala ya sura hizo. Matokeo ya utafiti yametolewa kwa mujibu wa malengo ya utafiti na misingi ya kinadharia iliyoongoza utafiti huu. Hatimaye, mapendekezo ya utafiti zaidi yametolewa katika nyanja za fasihi simulizi ya Kiafrika na hususan nyimbo na mabadiliko ya kimaudhui.

5.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu umehakiki mabadiliko kimaudhui ya nyimbo za jando za jamii ya Wakamba kulingana na mabadiliko ya kijamii. Baada ya kuchanganua nyiso hizi katika kipindi cha kabla na baada ya ukoloni, madhumuni ya utafiti huu pamoja na maswali yaliyoongoza utafiti yalijibiwa. Madhumuni ya kwanza yalikuwa ni kuchunguza maudhui ya nyimbo za

jando za Wakamba kabla ya maingiliano yao na wakoloni. Baada ya uchanganuzi wa maudhui ya nyimbo za kipindi cha kwanza cha utafiti, ilibainika kwamba nyimbo za kabla ya maingilio ya wakoloni zilikuwa na maudhui ya kitamaduni. Maudhui hayo yalilenga masuala mahususi yaliyoibuka kutokana na hali ya jamii na wakati wake. Hii ni kutokana na sababu kwamba, asasi za kitamaduni katika jamii hii zilikuwa imara na mwelekeo wa kitamaduni ulitawala shughuli zote za kijamii. Dhima kubwa ya nyimbo za jando katika jamii jadi ya Wakamba ilikuwa ni kuwatayarisha wavulana kwa majukumu ya baadaye kama viongozi wa jamii, walinzi, waume, baba wa watoto, wazalishaji mali miongoni mwa majukumu mengine. Kutokana na utamaduni huu, nyimbo za jando za kipindi hiki nazo zilitungwa zikiwa na maudhui yaliyosawiri mwelekeo huu wa kijamii. Maudhui ya nyimbo za jando katika kipindi cha kabla ya ukoloni yalikuwa mahususi na yalilenga masuala kama; umuhimu wa ujasiri wakati wa tohara, kukejeli waoga, kuonya na kukashifu tabia hasi katika jamii, kuelimisha watahiriwa kuhusu majukumu ya kiuana pamoja na kufafunza historia ya jamii. Kipengele cha usanii wa matukio kama yanavyoonekana katika jamii kiliongoza utafiti huu katika kumulika uhalisi wa maisha katika jamii ya jadi ya Wakamba.

Madhumuni ya pili ya utafiti huu yalikuwa kubainisha jinsi kipindi cha baada ya ukoloni kilivyoathiri maudhui ya nyimbo za jando za Wakamba. Baada ya maingilio ya wakoloni, utamaduni wa Wakamba uliathiriwa na dini ya kikristo pamoja na elimu ya kimagharibi. Utangamano baina ya Wakamba na wakoloni uliathiri maisha ya Wakamba. Kupitia nyimbo za jando za kisasa za Wakamba, imedhihirika wazi kuwa mtazamo wa jamii hii umebadilika. Nyimbo za jando za kisasa huangazia maswala ya maisha ya leo. Jamii ya

Wakamba hutumia nyimbo hizi kufunza na kuleta jamii pamoja na pia humulika maswala nyeti yanayoibuka katika jamii hii. Wajibu unaotekelezwa na nyimbo za jando za kisasa ni pamoja na kuelimisha vijana kuhusiana na maswala ibuka katika jamii inayobadilika kama ugonjwa wa ukimwi, kutahadharisha dhidi ya mapenzi yasiyo ya dhati, kuonya vijana kuhusiana na ndoa za jinsia moja zinazosababishwa na tabia ya ushoga na ubasha, kujichagulia wake wasiowaelewa vizuri, ugomvi katika ndoa, kukashifu wanajamii ambao wameasi mila na tamaduni za Wakamba za tohara za kiasili, kumulikia wanajamii kuhusu umuhimu wa ushirikiano wa kijamii, elimu ya kigeni, dini ya Kikristo miongonimwa masuala mengine muhimu ya kijamii. Maudhui ya nyimbo za jando za Wakamba katika vipindi viwili vya kihistoria yanaonyesha uhalisi wa maisha ya jamii husika kimpito wakati.

Madhumuni ya tatu yalikuwa ni kuainisha matukio ya kijamii yanayoathiri maudhui katika nyimbo za jando za Wakamba. Kupitia utafiti huu, ilibainika kuwa kuwepo kwa mfumo rasmi wa elimu, mifumo mipya ya uzalishaji mali, dini ya kikristo, maswala ya kiuchumi, maswala ya kijamii miongoni mwa mengine yameathiri maudhui ya nyimbo za jando za jamii ya Wakamba. Hii ni kutokana na sababu kwamba, mtunzi huongozwa na matukio na maendeleo ya kihistoria ili kuteua maudhui. Kigezo hiki cha mapisi humsaidia fanani kumulika mambo muhimu katika vipindi tofauti vya kihistoria. Imebainika kuwa, msanii hubadilisha maudhui ili kufanikisha mawasiliano ya ujumbe uliokusudiwa. Wasanii hubadilisha maudhui kwa mujibu wa maendeleo na mabadiliko katika jamii. Utafiti huu umegundua kuwa, msanii hufanya mabadiliko haya ya maudhui ili kuakisi na kusawiri matamania, matarajio na malengo ya wanajamii. Kipengele cha

nadharia ya uhalisia ambacho hushikilia kuwa uhalisia hutilia maanani matukio na mandhari ya kawaida yanayoweza kupatikana katika jamii kilisadifu katika kubainisha matukio ya kijamii huathiri maudhui ya nyimbo za jando za Wakamba.

Madhumuni ya nne yalikuwa ni kuchunguza mbinu za kisanaa zinazotumika na watunzi wa nyimbo za jando katika jamii ya Wakamba ili kubadilisha maudhui kwa mujibu wa wakati. Baada ya kuchanganua nyimbo za jando za Wakamba zilizoimbwa kabla na baada ya ukoloni, utafiti huu uling'amua kuwa msanii hutumia mbinu za sanaa katika nyimbo ili kuzua mawasiliano anayotarajia. Mbinu mahususi za kisanaa ambazo zilijitokeza katika nyimbo hasa za kipindi cha pili cha utafiti ni pamoja na mbinu ya istiari katika kulinganisha hali mbili tofauti, jazanda, taswira ambapo msanii anachora picha akilini kuhusiana na masuala nyeti yanayokumba jamii, maswali ya balagha, takriri ili kusisitiza suala fulani, tasfida ili kuficha makali ya lugha miongoni mwa mbinu nyingine za kisanaa. Nadharia ya Uamali ilitumika ili kushirikisha matumizi ya lugha kama nyenzo ya kufaulisha mawasiliano. Kupitia kwayo, utafiti huu ulizingatia muktadha na maana ya lugha ili kuelewa tamadhali za usemi zilizotumiwa na watunzi wa nyimbo hizi. Lugha hivyo basi imejitokeza kama matofali yanayojenga kazi ya fasihi. Matumizi ya lugha ndiyo yanayokuza na kupalilia mawasiliano kupitia maudhui ya nyimbo. Lugha ni muhimu katika kuelewa kazi yoyote ya kifasihi. Matumizi ya lugha hasa tamathali za usemi kwa mujibu wa utafiti huu ndiyo hujenga maudhui yanayojitokeza katika nyimbo za jando za Wakamba. Utafiti huu uligundua kuwa, lugha ndiyo nyenzo kuu ya fasihi simulizi za Kiafrika. Nyimbo za jando za Wakamba ni chombo muhimu kinachotumia lugha na kinachobeba mawazo ya wanajamii kuhusu nyanja mbalimbali za

kijamii mathalan kuhusu ndoa, dini, elimu, na mahusiano ya kijamii. Tamathali za usemi zinazobainika katika nyimbo za jando za Wakamba zinatokana na mazingira ya jamii hii.

Aidha, kazi hii iligundua kuwakatika utunzi wa nyimbo za jando, uteuzi wa maudhui huathiriwa sana na muktadha. Mtunzi hulazimika kuzingatia hadhira lengwa ya wimbo wake kwa sababu wanatarajiwa kupata ujumbe unaowalenga na uwe na athari kwao. Msanii huteua lugha wanayoielewa ili wimbo utimize malengo yake. Mtunzi wa wimbo huongozwa na matukio ya kihistoria ili kuteua maudhui yanayolandana na wakati, huku akitilia maanani kigezo cha mapisi ili yamuongoze katika kumulika mambo muhimu katika vipindi tofauti vya kihistoria. Huu ni ushahidi tosha kuwa sherehe za jando baina ya Wakamba si shughuli iliyopitwa na wakati. Imebainika kuwa, nyimbo nyingi za jando katika jamii ya Wakamba hunyumbuliwa na wasanii ambao huongozwa na matukio muhimu katika jamii ya Wakamba na nchi nzima kwa jumla.

Aidha, msanii hana budi kuzingatia namna ya kuuwasilisha wimbo wake. Uwasilishaji ni jambo la kimsingi mno katika utunzi na uimbaji wa nyimbo za jando za Wakamba. Hii ni kwa sababu namna ya kuwasilisha wimbo huathiri upokeaji na utendakazi wa wimbo husika. Msanii hana budi kuwa hodari na mbunifu anapotunga na kuimba nyimbo zake. Umahiri wa uwasilishaji wake unajitokeza kupitia kuukarabati na kuubadilisha wimbo wa zamani, kubuni nyimbo mpya, kuchopeka maneno mapya na yanayoathiri hadhira, kubadilisha sauti, kuigiza kucheka, kulia na kadhalika. Mambo haya husaidia katika kupitisha ujumbe unaokusudiwa.

Tasnifu hii imebainisha kuwa, hadhira katika nyimbo hizi huwa tendi. Nyimbo za jando katika jamii ya Wakamba hasa sehemu ya utafiti hushirikisha wanajamii wengi. Wanashiriki kwa kuimba, kupiga makofi, kunengua viungo, kupuliza ala za muziki mfano *ngungulu*(taz.Kiambatisho 1),kucheka na kushikana mikono.

Kadhalika, kazi hii katika kuongozwa na kipengele cha nadharia ya ethnografia ya mawasiliano ya Dell Hymes (1974) kuhusu umuhimu wa mazingira katika kuelewa kazi ya fasihi imebainisha kuwa, mazingira maalum yanayozingatiwa katika utunzi wa nyimbo za jando za Wakamba huzipa nyimbo hizo maana na majukumu teule. Lugha inayotumika katika nyimbo hizi huteuliwa kwa ustadi mno kwa kuzingatia muktadha, washiriki na hadhira lengwa. Watunzi na waimbaji wa nyimbo hizi hubadilisha lugha ili kuakisi na kusawiri maendeleo na mabadiliko yanayotokea katika jamii.

Pia kazi hiiuling'amua kuwa, ili kuelewa nyimbo za jamii fulani, inahitaji kuyaelewa maneno yaliyotumika katika nyimbo na pia kuyaelewa maisha ya watu katika jamii husika. Hii ni kwa sababu, lugha katika nyimbo za jando husaidia kuibua maudhui na dhamira zinazokusudiwa ili kuelewa yasemwayo katika kazi ya sanaa. Pia, ni sharti kuelewa lugha ya jamii husika. Nadharia ya Uamali ilisadifu katika kufasiri na kuchanganua maana ya maneno yaliyotumiwa katika nyimbo za jando za Wakamba, ili kuibua mawasiliano yaliyokusudiwa.

Kwa jumla, utafiti huu uling'amua kuwa nyimbo kama amali ya jamii ni kioo cha jamii, na haziwezi kwenda kinyume na mtazamowa ulimwengu wa jamii husika kuhusumasuala

kadha yamaisha. Vilevile, kazi hii ilig'amua kuwa, ili fasihi iwe na manufaa katika jamii, ni lazima iwe chombo kiaminifu cha jamii hiyo. Ni lazima iwe na jukumula kuieleza, kuichambua, kuikosa na kuiongoza jamii katika lengo lake la kufichua makosa yafanyikayokatika jamii. Kama nyenzo muhimu ya kupitisha elimu za kitamaduni, nyimbo za jando zimekuwa kiungo muhimu kwa Wakamba katika kuonya, kutahadharisha kuelimisha, kuadilisha na kupitisha maadili kwa vijana na wanajamii kwa jumla.

5.3 Mapendekezo Yanayotokana na Utafiti Huu

Utafiti huu unapendekeza kuwa, Almashauri ya uhifadhi wa mabo ya kitamaduni ya kitaifa itilie maanani uhifadhi wa nyimbo jadii zikiwemo za jando kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Pia, Serikali za Kaunti ziunde Almashauri ya uhifadhi wa mambo ya kitamaduni ili utamaduni wa kila jamii uweze kuhifadhiwa kwa manufaa ya wanajamii wake na wengine.

Kadhalika, utafiti huu unapendekeza serikali kuu pamoja na serikali za Kaunti kuwasajiri ngariba na kuwapa mafunzo kuhusiana na umuhimu wa usafi wa vifaa wanavyovitumia katika kutahiri ili kuzuia maabukizi ya magonjwa likiwemo gonjwa la Ukimwi.

5.4 Mapendekezo ya Maeneo ya Kufanyiwa Utafiti Zaidi

Utafiti huu ulizingatia kipera kimoja tu cha fasihi simulizi ya Wakamba hususan, nyimbo za jando kwa kuhakiki mabadiliko ya maudhui ya nyimbo hizi, kwa mujibu wa wakati. Kwa hivyo, ili kudumisha utamaduni wa jamii hii, inapendekezwa kwamba utafiti wa mabadiliko ya maudhui unaweza kufanywa katika vipera vingine vya fasihi simulizi ya Wakamba. Vipera hivi ni kama methali, vitendawili, majigambo, mafumbo katika kipera cha semi miongoni mwa vipera vingine. Utafiti kama huu unaweza kuongozwa na nadharia tofauti na zile zilizotumiwa katika utafiti huu.

Kipengele cha mabadiliko ya nyimbo za jando za Wakamba kimtindo kifanyiwe utafiti wa kina katika tafiti za baadaye. Kwa njia hii, mtazamo mpana wa itikadi ya tohara katika jamii ya Wakamba utaweza kujitokeza dhahiri zaidi.

Jamii ya Wakamba ina nyimbo za aina tofautitofauti jadiiya. Ni vyema kuzifanyia utafiti aina hizi nyingine za nyimbo hususan *kilumi, itheke, kinzena myali* miongoni mwa nyingine nyingi ili kubainisha iwapo kuna mabadiliko ya kimaudhui na kama nyimbo hizi jadiiya bado zina utendakazi katika ulimwengu huu unaobadilika.

Kwa sababu ya upeo wa utafiti huu, utafiti huu haukuweza kuchunguza iwapo nyimbo za unyago zipo na mabadiliko yake kimaudhui. Hivyo basi tungependekeza utafiti zaidi ufanywe ili kuangazia aina hizi za nyiso kwa kusudi la kuhifadhi utamaduni wa Wakamba wa nyimbo za unyago. Jamii iliyofanyiwa utafiti ni mojawapo ya jamii zilizoathiriwa zaidi na utamaduni wa kigeni. Utafiti huu unapendekeza kuwa utamaduni

hasa wa nyimbo za jando uhifadhiwe katika ukumbi wa kitamaduni kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Aidha, maendeleo ya kijamii na kidini yamechangia kubuniwa kwa nyimbo mpya za tohara katika jamii ya Wakamba zinazoakisi mabadiliko haya. Hii ni kwa sababu nyimbo ni sehemu ya utamaduni wa watu na mabadiliko yoyote hayana budi kuathiri fasihi simulizi ya jamii husika. Utafiti unaweza kufanywa kubainisha athari ya mabadiliko ya kidini na mazingira ya sherehe za tohara pamoja na nyimbo zinazoandamana na tohara hizo.

Utafiti huu unapendekeza utafiti zaidi ufanywe kuhusiana na tohara za hospitalini ili kuchunguza athari yake katika utamaduni wa Kiafrika.

Je, nyimbo za jando katika jamii ya Wakamba zina usemezano? Ni utafiti tu ambao unaweza kulijibu swali hili.

5.5Changamoto za Utafiti

Tatizo kuu lililokumbana utafiti huu ni upana wa maeneo ya utafiti. Tarafa ya Tseikuru ni pana mno. Barabara ni mbovu na aina za usafiri ni tatizo kubwa. Ilitubidi kutumia pikipiki maarufu kama *bodaboda* katika sehemu ya utafiti ambazo ndizo hutumiwa na wenyeji kusafiria. Malipo yalikuwa ghali mno. Hata hivyo, matatizo ya usafiri hayakuzuia kwa vyovyote kukamilisha kazi hii. Kutafsiri pia ilikuwa tatizo kubwa hasa

baadhi ya maneno ya kikale. Mtafiti alitafuta ushauri wa wazee wa *kivalo* na *kisuka*(taz.

Kiambatisho 1) ili wamsaidie kupata maana inayokusudiwa.

MAREJELEO

Abrams, M.H. (1988). *Definitions of Realism and Naturalism*.

www.lib.uci.edu/about/htm. Accessed on 19.5.2015

Agu, D.C. (1991). *Form and Analysis of African Music*. Enugu: New Generation Books.

Austin, J.L. (1962). *How to do things with Words*. London: Oxford University Press. Akivaga, S.K. & Odaga, A.B. (1982). *Oral Literature: A school Certificate Course*.

Nairobi: East African Educational Publishers.

Andrew, F. & Salvadori, S. (1980). *Peoples and Cultures of Kenya*. Nairobi: Primrose Sundries.

Bacon, M. (2012). *Pragmatism*. Oxford University Press.

Barry, V. (1983). *Philosophy*. California: Wadsworth Publishing Company.

Bible Society of Kenya. (1992). *Biblia. Habari Njema*. Nairobi: Bible Society of Kenya.

Bowman, W.D. (1998). *Philosophical Perspective on Music*. London: Oxford University Press.

Brake, M. (1980). *The Society of Youth Culture and Youth Subcultures: Sex, Drugs and Rock 'n' Roll?* London: Routledge and Kegan Paul.

Carston, R. (1988). *Implicature, Explicature, and Truth Theoretic Pragmatics*. Cambridge University Press.

Chacha, M.C. (1997). *Majigambo ya Kikuria. Mtazamo wa Kiisimu. Tasnifu ya Uzamili*. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Chesaina, C. (1991). *Oral Literature of the Kalenjin*. Nairobi: Printing Industries.

- Chiari, J. (1960). *Realism and Imagination*, London: Barrie and Rockliff Ltd.
- Coombes, H. (1953). *Literature and Criticism*. London: Penguin.
- Craig, D. (1975). *Marxists on Literature. An anthology*. Haddmordworth: Penguin.
- Crystal, D. (1977). *The Cambridge Encyclopedia of language*. Basil Blackwell:
Cambridge University Press.
- Dundes, A. (1965). *The Study of Folklore*: NJ Prentice Hall: Upper Saddle River.
- Dundes, A. (1980). *Who are the Folk*. In *Interpreting Folklore*. Bloomington: Indiana
University Press.
- Fasold, R. (1990). *The Sociolinguistics of Language*. Basil Blackwell: Cambridge
University press.
- Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. London: Oxford University Press.
- Finnegan, R. (1977). *Oral Traditions and Verbal Arts; Guide to Research*. London:
Routledge.
- Firth, R. (1968). *Modes of Meaning in Modes of Selected Papers of J.R. Firth*. London:
Indiana University Press.
- Foley, J. (1995). *The Singer of the Tales Performance*. Bloomington: Indiana University
Press.
- Foucault, M. (1972). *The Archeology of Knowledge and the Discourse of Language*. New
York: Routledge Publishers.
- Foucault, M. (1977). *Politics, Philosophy Culture: Interviews and other Writtings*.
London: Routledge.

- Gachiri, W.E. (2000). *Female Circumcision with Reference to Agikuyu of Kenya*.
Nairobi: Paulines Publication.
- Gibbe, A.G. (1978). *Fasihi na Jamii*. Katika *Kiswahili*. Juzuu 48. Chuo Kikuu cha Dar
es Salaam. TUKI. Uk. 18-21.
- Gregory, M. & Carroll , S. (1978). *Language and Situation. Language Varieties and
their Social Context*. London: Routledge and Kegan Paul.
- Grice, H.P. (1989). *Studies in the way of Words*. Cambridge, Mass: Harvard University
Press.
- Goodman, R. (2005). *Pragmatism. Critical Concepts in Philosophy*. London: Routledge.
- Gumperz, J. & Hymes, D. (1972). *Directions in Sociolinguistics: The Ethnography of
Communication*. Oxford: Blackwell Ltd.
- Guthrie, M. (1967). *The classification of Bantu Languages*. Famborough: The Gregg
Press.
- Halliday, M.A.K. (1964). *Learning How to Mean: Explorations in the Development of
Language*. London: Edward Arnold.
- Hegel, G.W. (1975). *Aesthetics*. New York: Oxford University Press.
- Hegel, G.W. (1979). *Introduction to Aesthetics*. London: Oxford University Press.
- Horn, L. (1990). *Pragmatic Theory*. Newmeyer: Cambridge University Press.
- Hudson, R.A. (1980). *Sociolinguistics*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Hymes, D. (1962). *Ethnography of Speaking. Anthropology and Human Behaviour*.
Washington D.C.
- Hymes, D. (1964). *Language in Culture and Society*. New York: Harper and Row Inc.

Hymes, D. (1974). *Foundations in Social Linguistics: An Ethnographic Approach*.

Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Indangasi, H. (1997). Gender Socialisation in the Maragoli circumcision Ceremony.

Katika W. Kabira. M, Masinjila and M. Obote (Wah) *Contesting Social*

Death:Essays on Gender and Culture. Nairobi: Kenya Oral Literature

Association. Uk 16-22.

James, C.V. (1973). *Soviet Socialist Realism: Origins and Theory*. London: Macmillan

Press.

Kabira, W. na Mutahi, H. (1988). *African Oral Literature*. Nairobi: Longman Kenya

Limited.

Kanake, A.K. (2001). Change and Continuity in the practice of Clitoridectomy: A case

study ofTharaka of Meru East.Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha

Kenyatta.(Haijachapishwa)

Kaplan, E.A. (1989). *Rocking Around the Clock: Music, Television. Postmodernism and*

Consumer Culture. London: Mathuen.

Karanja, W. (2008). Masuala ibuka katika Fasihi ya Watoto. Tasnifu ya Uzamili. Chuo

Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Kau, M. (2008). Usawiri wa Vijana katika Tamthilia teule za Kiswahili. Tasnifu ya

Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Kaviti, L.K. (2004). A Minimalist Perspective in Kikamba Morpho-Syntax. Tasnifu ya

Uzamifu. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

- Kavyu, P.N. (1980). *Traditional Musical Instrument of Kenya*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Kieti, M. (1999). Myali songs. Social Critique among the Kamba. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Kieti, M. na Coughlin, P. (1990). *Barking, U Will Be Eaten! The Wisdom of Kamba Oral Literature*, Nairobi: Phoenix Publishers.
- Kilauni, N.M. (2007). Usasa katika Nyimbo za *Itheke*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Kilonzi, L.A. (1992). Dance and movement: A Study of the factors affecting Step and Dance movement among the Kamba: Kinze: Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Kimilu, D. (1962). *Mukamba wa w'o*. Nairobi: East Africa Literature Bureau.
- Kinara, G. (2012). Maudhui ya Ukimwi katika Ua La Faraja na Kala Tufaha. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- King'ei, K. (1982). Uhakiki wa *Nthimo* (methali) za Kikamba kwa kufuatishamisingi ya methali za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa)
- King'ei, K. (1992). Language, Culture, and Communication. The role of Swahili Taarab Songs in Kenya from 1963-1990. Tasnifu ya Uzamifu, Washington D.C:Chuo Kikuu cha Howen. (Haijachapishwa)
- King'ei, K. na Kisovi, C. (2005). *Msingi Wa Fasihi Simulizi*. Nairobi : Kenya Literature Bureau.

- Kipury, N. (1983). *Oral Literature of the Maasai*. Nairobi: Heinemann.
- Kirumbi, P. (1975). *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Shungwaya Publishers.
- Kobia, M. (2008). Taswira za Kiuana katika Nyimbo za Tohara za Wanaume miongoni mwa Waigembe. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Kothari, C.R. (2004). *Research Methodology. Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International.
- Larkin, M. (1977). *Man and Society in the Nineteen Century Realism*. London: Macmillan Press.
- Leech, G. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman.
- Levinson, S. (1983). *Pragmatics*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Lomatoro, P.J. (2014). Viwango vya Uhalisi na Ubunifu katika Riwaya Teule za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Lukacs, G. (1963). *The meaning of Contemporary Realism*. London: Merlin Press.
- Lukacs, G. (1972). *Studies in European Realism. A Sociological Survey of Writings of Balzac, Stredhal, Zola, Tolistoy, Gorki & Others*. London. Marlin Press.
- Malenya, M. (2008). Matumizi ya Jazanda katika Nyimbo za Jacob Luseno. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Masinde, E.W. (2003). Ushairi wa Kiswahili: Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Matteru, L. B. (1981). Fasihi Simulizi na Uandishi. Makala ya semina ya waandishiwa Kiswahili. Dar es Salaam: TUKI.

- Matti, G.N. (1996). *Sanaa za Maonyesho za Kiafrika za jadi: Mfano wa Tohara ya Watharaka*.Tasnifu ya Uzamili, Eldoret: Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa)
- Mbaabu, I. (1985). *Utamaduni Wa Waswahili*. Nairobi: Kenya Publishing and Book Marketing.
- Mbarwa, H. (1989) *Your Oral Literature*. Nairobi: Kijabe Printing Press.
- Mbiti, J.S (1991). *Love and Marriage*. London: Longmans.
- Mbiti, J.S. (1969). *African Religion and Philosophy*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mbogo,S. (2008). *Mabadiliko ya Maudhui Kiwakati katika Nyimbo za Harusi za jamii ya Waembu*.Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Meena, R. (1992). *Gender in Southern Africa: Conceptual and Theoretical Issues*. Harare: Sapes Books.
- Mkimbo, M. (1981). *Song as a political weapon during 1974/75 General Elections in Lamu*.Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Mlacha, S. (1995). *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Dar es Salaam : Tasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- M’Ngaruthi, T.K. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi : Jomo Kenyatta Foundation.
- Mohamed, S.A. (1995). *Kunga za Nathari. Katika Kiswahili*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Momanyi, C. (1991). *Taswira kama Kielelezo cha Uhalisi katika Ujenzi wa Al-Inkishafi*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

- Momanyi, C. (1998). Usawiri wa Mwanamke Mwislamu katika jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika ushairi wa Kiswahili, Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Momanyi, C. (2001). Nafasi ya mwanamke katika ushairi wa Shaaban Robert. Katika *Kiswahili juzuu 64*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mosha, D. (2011). Matumizi ya Lugha katika Sherehe za Kumfunda Mwali Miongoni mwa Wazaramo. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Msokile, M. (1981). *Nafasi ya Nyimbo za Fasihi Simulizi katika Jamii inayobadilika*. Katika Makala za semina ya Fasihi Simulizi. Dar es Salaam : Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Msokile, M. (1993) *Misingi ya Uhakiki Wa Fasihi*. Nairobi : East African Educational Publishers.
- Mue, E. K. (2013). Maudhui na matumizi ya Lugha katika nyimbo za injili za Rose Muhando. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Mugenda, O. na Mugenda A. (1999). *Research Methods. Quantitative Approaches and Qualitative Approaches*. Nairobi: Acts Press.
- Mugenda, O. na Mugenda A. (2003). *Research Methods. Quantitative Approaches and Qualitative Approaches*. Nairobi: Acts Press.
- Mulokozi, M. (1989). Nafasi ya Nyimbo za Fasihi Simulizi katika Jamhuri Inayobadilika. Makala yaliyowasilishwa katika semina ya fasihi simulizi. *Jarida la*

- Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.* Dar es Salaam. Uk 21-33.
- Mulokozi, M.M. (2003). Utafiti wa fasihi simulizi, katikamakala ya semina ya *Kimataifa ya waandishi wa Kiswahili.* TUKI. Dar es Salaam. Uk 18-26.
- Musyimi, D.M. (2011). Maana za Majina ya Watu katika Jamii ya Wakamba. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishawa)
- Musyoka, E. (2012).Uhakiki wa Kimtindo wa Nyimbo za Mazishi Miongoni mwa Wakamba. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Mutegi, L. (2010). Maigizo Katika Fasihi Simulizi : Mfano wa Kirarie katika Nyimbo za Tohara ya Wameru.Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Mutembei, A.K. (2009). *Ukimwi Katika Fasihi ya Kiswahili 1982-2009.*Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.
- Mutwiri, G. (2005).Mitazamo ya utendakazi wa Nyiso katika jamii ya Watigania. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Mvumbi, F.N. (2008). *Journey into Islam.*Nairobi:Pauline Publications Africa.
- Mwai, K.W. (1997). ThePower of Song for Swahili Woman. Contesting socialDeath. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Mwamzandi ,Y. na Nkichabe, S. (2008). Udenguzi wa Maana katika Diskosi ya Kisiasa nchini Kenya: Mifano ya nyimbo pendwa. Katika Nathan Ogechi, Naomi Shitemi, Inyani Simala.(Wah.)*Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na lugha za Kiafrika.* MoiUniversity Press, Moi University Eldoret. Uk 307-317.

- Mwaniki, H. (1986). *Categories and Substance of Embu Traditional Songs and Dance*.
Nairobi: Kenya literature Bureau.
- Mwita, B.M. (2005). *Usawiri wa Mwanamke Katika Ichingiro za Wakuria*. Tasnifu ya
